**3 SEPTEMBA, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Sita – Tarehe 3 Septemba, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

### TAARIFA YA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuna Taarifa ya Spika chini ya Kanuni ya 39(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyokumbuka tarehe 28 Agosti, 2024, kwa niaba yenu nilitoa salamu za awali kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika, ushindi huu aliupata katika uchaguzi uliofanyika katika Mkutano Mkuu wa 74 wa Shirika la Afya Duniani *(WHO)*, tarehe 27 Agosti, 2024, nchini Congo Brazzaville, ambapo Wajumbe 25 kati ya 46 wa Mkutano huu walimchagua na kuwashinda wagombea wengine kutoka Niger na Senegal.

Waheshimiwa Wabunge, niliahidi akirejea nchini tutampa salamu zetu za pongezi, leo Mheshimiwa Dkt. Ndugulile yupo nasi hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hivyo kwa niaba yenu na kwa mara nyingine tena nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Ndugulile kwa heshima kubwa aliyoiletea nchi yetu. Ushindi huu umelipa Bunge letu sifa na Tanzania kwa ujumla, aidha, ushindi huu unaiweka nchi yetu vizuri kwenye siasa za kikanda na za kimataifa *(Geopolitics)*. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nirudie kusema kwamba, mambo haya hayawezi kufanikiwa kama hayaungwi mkono na Serikali, kwa namna ya pekee narudia kuipongeza sana Serikali yetu inayoongozwa na Mwanadiplomasia mahiri Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na timu ya kampeni ikiongozwa na Mheshimiwa Balozi Mohammed Thabiti Kombo, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Afya waliofanikisha ushindi huu mkubwa kupatikana.

Aidha, napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliotuwakilisha katika zoezi hili ambao ni Mheshimiwa Elibariki Emmanuel Kingu, Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mheshimiwa Shamsia Aziz Mtamba na Mheshimiwa George Ranwel Mwenisongole. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema hapa awali Mheshimiwa Dkt. Ndugulile tupo naye hapa Bungeni na baada ya kipindi cha maswali na majibu nitampa nafasi aje hapa mbele ili atoe neno la shukrani.

Imetolewa na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge na Spika, Tarehe 3 Septemba, 2024. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE NA URATIBU:**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 15 la Tarehe 12 Aprili, 2024;
2. Toleo Na. 16 la Tarehe 19 Aprili, 2024;
3. Toleo Na. 17 la Tarehe 26 Aprili, 2024;
4. Toleo Na. 18 la Tarehe 03 Mei, 2024;
5. Toleo Na. 19 la Tarehe 10 Mei, 2024;
6. Toleo Na. 20 la Tarehe 17 Mei, 2024;
7. Toleo Na. 21 la Tarehe 24 Mei, 2024;
8. Toleo Na. 22 la Tarehe 31 Mei, 2024;
9. Toleo Na. 23 la Tarehe 07 Juni, 2024;
10. Toleo Na. 24 la Tarehe 14 Juni, 2024;
11. Toleo Na. 25 la Tarehe 21 Juni, 2024;
12. Toleo Na. 26 la Tarehe 28 Juni, 2024;
13. Toleo Na. 27 la Tarehe 05 Julai, 2024;
14. Toleo Na. 28 la Tarehe 12 Julai, 2024;
15. Toleo Na. 29 la Tarehe 19 Julai, 2024;
16. Toleo Na. 30 la Tarehe 26 Julai, 2024;
17. Toleo Na. 31 la Tarehe 02 Agosti, 2024;
18. Toleo Na. 32 la Tarehe 09 Agosti, 2024;
19. Toleo Na. 33 la Tarehe 16 Agosti, 2024; na
20. Toleo Na. 34 la Tarehe 23 Agosti, 2024.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA**

Maelezo ya Waziri wa Viwanda na Biashara kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 *(The Fair Competition (Amendment) Bill, 2024)*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2024)*.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 *[The Fair Competition (Amendment) Bill, 2024]*.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2024)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali, tunaanza na Ofisi ya Rais. Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka.

Na. 88

**Ukarabati wa Kituo cha Afya Mjimwema**

**MHE. MARIAM M. NYOKA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Kituo cha Afya cha Mjimwema hasa Wodi ya Akina mama, Wanaume na *OPD* kwani kimechakaa sana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Mjimwema kilichopo katika Manispaa ya Songea kilijengwa mwaka 1982. Kituo hiki ni miongoni mwa vituo vya afya 202 vilivyofanyiwa tathmini kwa ajili ya ukarabati mkubwa na kuongeza miundombinu ili kuendana na mahitaji ya sasa ya utoaji wa huduma za Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023 na 2023/2024, Kituo cha Afya cha Mjimwema kilipelekewa shilingi milioni 35 kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri pamoja na wadau wa huduma rafiki kwa vijana kwa ajili ya ukarabati, ambapo majengo yaliyokarabatiwa ni wodi ya wanawake na watoto, jengo la huduma ya uzazi na mtoto *(RCH),* wodi ya wanaume na jengo la huduma za wagonjwa wa nje - *OPD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, kituo kimetenga shilingi milioni 28 kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa jengo la huduma za wagonjwa wa nje na wodi ya wanaume.  Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyoka.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, katika kituo hiki cha afya hakuna wodi ya wanaume na pia hakuna jokofu la kuhifadhia maiti. Swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka huduma hizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; Serikali ina mpango gani wa kukarabati Kituo cha Afya Namtumbo ikiwa ni

pamoja na wodi ya akina mama, jengo la *OPD* pamoja na vyumba vya matabibu? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kituo hiki cha afya kina upungufu wa baadhi ya miundombinu ikiwemo wodi za wanawake, wanaume na watoto na tayari Serikali imeshafanya tathmini ya vituo vyote chakavu kote nchini, jumla ya vituo 202 kikiwemo kituo hiki cha Mjimwema vimeorodheshwa na vinatafutiwa fedha kwa ajili ya ukarabati na kuongeza majengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kituo hiki tayari kinatafutiwa fedha na mara tutakapopata fedha hizo tutakwenda kukarabati na kujenga majengo ambayo yanapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tunavyo vituo vya afya vikongwe kikiwemo Kituo cha Afya cha Namtumbo ambacho Mheshimiwa Mbunge ameuliza. Nimhakikishie tu kwamba, katika orodha ya vituo 202, Kituo cha Afya cha Namtumbo pia kimo kwa ajili ya kutafutiwa fedha ya ukarabati. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante…

**NAIBU SPIKA:** Samahani sana. Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota.

Na 89

**Kukamilisha Ujenzi wa Kituo cha Afya Nyundo – Nanyamba**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Nyundo - Nanyamba kilichojengwa kwa Nguvu za wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Nyundo kilichopo katika Mji wa Nanyamba kilianza kujengwa kwa nguvu za wananchi. Mwezi Septemba, 2023, Halmashauri kupitia Shirika la Mafuta Tanzania *(TPDC)* ilipokea kiasi cha shilingi milioni 40 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la kutolea huduma kwa wagonjwa wa nje *(OPD)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Shirika la *TPDC* limetoa shilingi milioni 360 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la kutolea huduma kwa wagonjwa wa nje na kuanza kujenga miundombinu mingine inayopungua ikiwemo jengo la wazazi lenye huduma za upasuaji wa dharura. Ujenzi wa jengo la huduma za wagonjwa wa nje uko 70% na majengo mengine yapo hatua ya kuandaa eneo la ujenzi na kazi zinaendelea. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninalishukuru Shirika la *TPDC* kwa kuendelea kutoa mchango wa ujenzi wa Kituo hiki cha Afya cha Nyundo na nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; pamoja na jitihada hizi zinazofanywa na *TPDC* na Serikali tutakuwa na vituo vya afya vitano, tuna changamoto kubwa sana ya Watumishi wa Sekta ya Afya katika Halmashauri ya Mji wa Nanyamba, sasa hivi tuna 40% ya mahitaji yetu. Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuhakikisha tunapata watumishi wa kutosha katika Halmashauri ya Mji wa Nanyamba?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais, Mkoani Mtwara, Mheshimiwa Waziri wa Nchi,

Ofisi ya Rais, TAMISEMI, aliahidi kutoa fedha za ujenzi wa Kituo cha Afya Namtumbuka kilichopo kwenye Kata ya Namtumbuka. Je, fedha hizo sasa zitatolewa lini ili ujenzi uanze? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa hoja na namna ambavyo ameendelea kuwasemea wananchi wa Jimbo lake, nimhakikishie tu kwamba Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameweka kipaumbele cha hali ya juu katika kuboresha ikama za watumishi wa sekta ya afya katika mamlaka ya Serikali za Mitaa, lakini pia katika ngazi nyingine za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitatu Serikali hii ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeshaajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya zaidi ya 18,748 na hivi sasa kuna kibali cha watumishi wa kada mbalimbali za afya zaidi ya 9,400 na taratibu za ajira zinaendelea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Chikota naomba nikuhakikishie kwamba, kama ambavyo huko nyuma Serikali imeleta watumishi pale Nanyamba, katika ajira hizi pia tutatoa kipaumbele kuhakikisha kwamba mnapata watumishi wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kuhusiana na Kituo cha Afya cha Namtumbuka, ni kazi ambayo Serikali imeanza kuifanyia kazi baada ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais na nikuhakikishie tu kwamba tutakwenda kujenga kituo hiki cha afya. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Laini, Wilaya ya Itilima ina wakazi wengi na haina Kituo cha Afya. Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha afya katika Kata ya Laini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kujenga vituo vya afya katika Kata za kimkakati na Halmashauri zimepewa wajibu wa kuainisha Kata za kimkakati na kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwa hivyo, ikiwa Kata hii imeshatambuliwa na Halmashauri ya Itilima na imeshawasilishwa katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI kama Kata ya kimkakati, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda kujenga kituo cha afya kwa awamu. Kama haijafanyika hivyo, basi tathmini ifanyike ili kuona kama inakidhi vigezo ili iweze kuingizwa kwenye mpango wa ujenzi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nashukuru Mfuko wa Jimbo kwa Jimbo la Rungwe kwa kuwa Mbunge wa Jimbo ameweza kutoa fedha, lakini bado Kituo cha Afya cha Kiwira hakijamalizika. Je, ni lini Serikali itatuongezea fedha ili tuweze kumalizia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kiwira ilikuwa ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika ziara yake mwaka 2022 na Serikali imeshapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho. Tunafahamu kuna baadhi ya miundombinu haijakamilika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunakwenda kwa awamu na tutapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha miundombinu yote ambayo haijakamilika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea kwa swali la Mheshimiwa Tecla Mohamedi Ungele.

Na. 90

**Kituo cha Afya Kitomanga - Mchinga kuwa Hospitali**

**MHE. TECLA M. UNGELE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaboresha Kituo cha Afya cha kimkakati cha Kitomanga Mchinga kuwa Hospitali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Kitomanga kipo katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi umbali wa takribani kilometa 55 kutoka Makao Makuu ya Manispaa. Kituo hicho kinatoa huduma zote muhimu ikiwemo huduma za wagonjwa wa nje, upasuaji na kulaza wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mwongozo wa uanzishwaji wa hospitali nchini uliotolewa na Wizara ya Afya mwaka 2015, kila Halmashauri inapaswa kuwa na Hospitali moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi 2023/2024, Serikali imepeleka jumla ya shilingi bilioni 1.8 katika Manispaa ya Lindi kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri. Kwa kuwa Kituo cha Afya cha Kitomanga ni cha kimkakati, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu yake kadri itakavyohitajika ili kiendelee kutoa huduma kwa ufanisi zaidi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tecla.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Swali la kwanza; je, Serikali itapeleka lini *x-ray* kwa sababu Kituo hiki cha Afya Kitomanga hakina huduma ya *x-ray* kwa muda mrefu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Serikali ina mpango gani wa kujenga uzio Kituo cha Afya Kitomanga ili kuleta usalama kwa wagonjwa, lakini pia kwa watoa huduma za afya katika kituo kile? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekwishatoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba. Katika Halmashauri zote 184 katika mwaka huu wa fedha pekeyake kila Halmashauri imepata kati ya shilingi milioni 700 na zaidi hadi shilingi bilioni mbili kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba. Kwa hivyo kipaumbele mojawapo katika vifaatiba ni kununua *digital x-rays*. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumechukua hoja ya Kitomanga tutafanya ufuatiliaji na kuona uwezekano wa kupata *digital x-rays* kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusiana na uzio, tunafahamu tunahitaji kuwa na usalama katika maeneo ya vituo vyetu ni jambo la msingi, lakini safari ni hatua. Tunakamilisha kwanza miundombinu ile muhimu ya kutoa huduma, lakini pia Manispaa ya Lindi nitoe maelekezo haya waanze kutenga fedha kwa awamu angalau kuanza ujenzi wa uzio wakati Serikali inaendelea kukamilisha miundombinu mingine. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Kituo cha Afya cha Tandale pale Jimboni Kinondoni kwa muda mrefu kimekuwa kinahitaji kupanuliwa na lilikuwa ni ombi kwa Serikali kwamba tununue majengo yaliyokaribu na yanayozunguka jengo lile la Kituo. Je, ni lini Serikali itasaidia ununuzi wa majengo pale ili Kituo kile kiweze kupanuliwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Tandale kwanza kinahudumia wananchi wengi sana lakini kina eneo dogo na Serikali ilikwishatoa maelekezo tangu mwaka 2018/2019 kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni itenge fedha kwa ajili ya kufidia yale maeneo ya jirani ili tuweze kutanua kile kituo cha afya kwa sababu idadi ya wananchi inaongezeka, lakini eneo linabakia kama lilivyo. Kwa hiyo naomba nitumie nafasi hii lakini pia Kituo cha Afya cha Kigogo nacho kuna eneo ambalo tuliainisha kwa ajili ya kuchukuwa yale maeneo kwa ajili ya kufidia na kuhakikisha kwamba tunakuwa na eneo la uhakika kwa miaka mingi zaidi ya Kituo cha Afya cha Kigogo na Tandale.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi kumkumbusha na kumsisitiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni kufanya tathmini ili tuanze hatua za kufidia maeneo hayo ili vile vituo viweze kutoa huduma kwa muda mrefu zaidi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Assa.

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kama ilivyo kwa Kituo cha Afya cha Kitomanga na sisi Kigoma Kaskazini tuna Kituo cha Afya cha kule Kata ya Kagunga ambacho ni kituo cha kimkakati. Kituo kile kinahudumia kata nne za pembezoni mwa nchi yetu ambapo ni Kituo muhimu sana. Je, ni lini Serikali itaweza kuona umuhimu wa kutenga fedha ili Kituo kile kiweze kukamilishwa kwa haraka? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Kagunga ambacho kimeanza ujenzi takribani miaka miwili au mitatu iliyopita tunafahamu kimefikia hatua lakini bado kuna uhitaji wa baadhi ya miundombinu. Naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa

Jimbo la Kigoma kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kukamilisha majengo yale na tunaendelea kwa awamu tutapeleka fedha kukamilisha miundombinu ambayo imebaki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Jafari Chege.

Na. 91

**Ujenzi wa Soko la Kisasa - Rorya**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa soko la bidhaa za samaki na dagaa katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Rorya inahitaji Soko la Kisasa la Samaki na Dagaa kutokana na shughuli za uvuvi kuwa miongoni mwa shughuli Kuu za kiuchumi kwa wananchi wa Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza mpango huu, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali kupitia Halmashauri imetenga shilingi milioni 76, mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Soko la Dagaa, Mkengwa ambalo ujenzi wake hadi kukamilika utagharimu shilingi milioni 300.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha bidhaa zitokanazo na samaki na dagaa zinapata soko la uhakika, Serikali kupitia Halmashauri inatarajia kujenga soko kubwa na la kisasa eneo la Mpakani Kirongwe, ambapo hadi sasa tayari mkopo wa shilingi bilioni nne umeombwa kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa ajili ya ujenzi wa

soko hilo muhimu kwa Halmashari ya Wilaya ya Rorya na maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Rorya itaendelea kutenga fedha za Mapato ya ndani kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Soko la Kisasa la Samaki na Dagaa kwa maendeleo ya wananchi wa Rorya. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri na Serikali kwa ujumla kwa majibu mazuri na yenye matumaini kwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya. Pamoja na majibu mazuri nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kutokana na majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri tumeona kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Rorya tayari tumetenga shilingi milioni 76, lakini fedha hitajika ni zaidi ya shilingi milioni 300. Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu kupitia bajeti ya mwakani kutenga fedha iliyosalia kutokana kwamba mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Rorya ni madogo mtupe fedha kiasi kilichosalia ili tuweze kukamilisha ujenzi wa soko eneo hili la Mkengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa hakika Serikali inaona umuhimu wa kutenga fedha hii kwa mwaka ujao wa fedha na tutafanya hivyo kwa kadri itakavyowezekana ili tuongeze kasi ya ujenzi wa soko hili. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Tuliwasilisha michoro kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa soko la kisasa eneo la Madiira kule Arumeru Mashariki mwaka jana mwezi Novemba, je, ni lini ujenzi huu utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Halmashauri ya Arumeru na Jimbo la Arumeru Mashariki kupitia Mheshimiwa Dkt. Pallangyo waliwasilisha andiko la kimkakati la soko la kisasa. Nimhakikishie tu kwamba tayari ilishapitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI na ilishafanyiwa tathmini na tuko hatua za ngazi ya Wizara ya Fedha kuona uwezekano wa kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji. Kwa hiyo naomba uwe na imani kwamba Serikali inalifanyia kazi suala hilo na wananchi watambue kwamba tumelichukua na tunalishughulikia. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar.

Na. 92

**Manufaa ya Zanzibar kwenye Mifuko ya Kimataifa ya Mapambano ya Mazingira na Tabianchi**

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR** aliuliza:-

Je, fedha kiasi gani imepatikana Zanzibar kwa miaka mitatu iliyopita kupitia Mifuko ya Kimataifa ya Mazingira na mabadiliko ya tabianchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikipokea fedha kutoka kwenye Mifuko ya Kimataifa ya Mazingira na mabadiliko ya Tabianchi ikiwemo Mfuko wa Mazingira wa Dunia *(GEF)* na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi *(GCF)*. Fedha hizo zimekuwa zikitumika kutekeleza miradi mbalimbali ya hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa upande wa Zanzibar, jumla ya shilingi bilioni 5.3 zimepelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya za Wete, Micheweni, Kaskazini Pemba, Kaskazini A, Kaskazini B na Kaskazini Unguja. Miradi iliyotekelezwa kupitia fedha hizo ni pamoja na Mradi wa kurejesha ardhi iliyoharibika na kuongeza usalama wa chakula kwenye maeneo kame nchini yenye thamani ya shilingi bilioni 1.2. Aidha, Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia Mifumoikolojia Vijijijini – *EBARR* (shilingi bilioni 1.4); na Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Wakazi wa Pwani shilingi bilioni 2.7. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bakar.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili. Swali la kwanza; kwa kuwa athari hizi za mazingira na mabadiliko ya tabianchi zinaendelea kuathiri maeneo mbalimbali ya nchi yetu na kwa kuwa upatikanaji wa fedha hizi kupitia mifuko ya nje ya Kikanda na ya Kimataifa bado ni mdogo. Je, ni mkakati upi wa Serikali kuhakikisha kwamba wanapanua wigo zaidi wa upatikanaji wa fedha hizi za mashirika haya ya nje?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nilitaka kujua; je, Serikali sasa haioni ipo haja ya kuweka utaratibu maalum kwa maana ya f*ormula* maalum sasa ya ugawaji wa fedha hizi zinazopatikana kwenye mashirika haya kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara kuwe kama *formula* maalum? Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bakar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru na kumpongeza sana kwa juhudi zake za kuona namna ambavyo mabadiliko ya tabianchi yanapata sura nyingine kwa maana kwamba tunatatua hizo changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo jitihada za Serikali ambazo zimefanywa na bado tunaendelea kuzifanya kuhakikisha kwamba tunaongeza fedha kwenye huu Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi. Kwanza kuna maandiko mbalimbali ambayo tayari tumeshaandika. Tuna jumla ya maandiko takribani 13 ambayo yote yanakwenda kuomba fedha kwa ajili ya kupambana dhidi ya athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tumeshakaa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira pamoja na Sekretarieti za Mifuko inayoshughulika na kutoa fedha hii Mifuko ya Kimataifa kama ambavyo nimeitaja hapa ili lengo na madhumuni kuweza kupata fedha zitakazotusaidia. Tunapokaa nao mara nyingi huwa tunawaambia kwamba nchi zilizoendelea lazima zisaidie nchi zinazoendelea katika kukabiliana na hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine hivi ninavyoongea tayari Kamati ya Fedha ya Kudumu inayoshugulikia masuala ya mabadiliko ya tabianchi kuna kikao kinaendelea Arusha Mheshimiwa Makamu wa Rais alifungua jana. Yote hiyo ni namna bora na njia za kuomba fedha kwa ajili ya kupambana dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa swali la pili; fedha hizi zinapokuja kutoka kwa wahisani huwa zinakwenda pande zote mbili za Muungano na ndio maana tayari ipo miradi iliyofanywa Zanzibar na ipo miradi iliyofanywa kwa upande wa bara. Ipo miradi Kaskazini A na Kaskazini B, Unguja, ipo miradi Wete na Micheweni kwa pande wa Pemba, lakini ipo miradi ya kujenga kuta kwa upande wa Sipwese, Pemba na upande wa

Mikindani Bara. Kwa hiyo miradi hii fedha zinapokuja zinanufaisha pande zote mbili za Muungano, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Nishati Mheshimiwa Furaha Matondo.

Na. 93

**Fidia kwa Wananchi wa Kijiji cha Iseni – Misungwi**

**MHE. FURAHA N. MATONDO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawalipa fidia wananchi 74 wa Kijiji cha Iseni, Kata ya Usagara, Misungwi waliotoa maeneo yao kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TANESCO* imekamilisha zoezi la uthamini kwa ajili ya kutwaa eneo la Kituo cha kupoza umeme katika Kata ya Usagara ambapo wananchi 74 watalipwa jumla ya shilingi bilioni 1.2 kama fidia. Fidia hii inategemea kulipwa kuanzia Mwaka huu wa Fedha wa 2024/2025. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matondo.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Kuna mradi mkubwa wa ujenzi wa *line* kubwa ya umeme kutoka Bunda kupita Nansio, Wilaya ya Ukerewe ambao unachelewa kwa sababu ya wananchi kutokulipwa fidia. Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi wale ili mradi ule uweze kuendelea? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tunafahamu juu ya umuhimu wa mradi huu wa kujenga njia kubwa ya kusafirisha umeme kutoka Bunda, Nansio kwenda Ukerewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tunashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili tuweze kulipa fidia kwa wananchi katika maeneo haya na ili mradi huu uweze kuendelea. Kadri ambavyo mradi unaendelea, tunaendelea kuwasiliana na ku-*engage* na wananchi ili tuweze kukubaliana ili mradi uweze kuendelea taratibu taratibu huku tunasubiri fidia. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge suala hili linafanyiwa kazi na wananchi hawa watalipwa fidia yao kuanzia mwaka huu wa fedha. Ahsante

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Nyarukoba ya Kijiji cha Msege umeme ulifika Makao Makuu ya Kijiji lakini katika eneo hilo kuna wachimbaji wadogo ambao wako tayari kutoa fedha zao wapelekewe umeme ili kupunguza gharama ya uzalishaji wa dhahabu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kwenda kuwasikiliza wachimbaji wale kwa gharama zao ili wapate umeme wafanye kazi ya uchimbaji? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake. Katika Kata hii ya Nyarukoba tayari nilishamwelekeza Meneja wa *TANESCO,* Mkoa wa Mara afanyie kazi na tayari wameshaanza kupeleka umeme kwenye hilo eneo. Niwahakikishie wachimbaji hawa wadogo tutawafikishia umeme kwa ajili ya kuboresha shughuli zao za kiuchumi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hassan.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itawalipa fidia Wananchi wa Wilaya ya Tunduru waliopisha Mradi wa Gridi ya Taifa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tayari wenzetu wa Wizara ya Fedha wanafanyia kazi jambo hili. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuanzia mwaka huu wa fedha wananchi hawa wa Wilaya ya Tunduru watalipwa fidia kwa ajili ya mradi huu wa kupeleka gridi kutoka Songea kwenda Mtwara mpaka Masasi na Lindi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate

Na. 94

**Kuunganisha Mkoa wa Kagera kwenye Gridi ya Taifa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaunganisha Mkoa wa Kagera na Gridi ya Taifa ili kuondoa adha ya kukatika umeme mara kwa mara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya za Mkoa wa Kagera zilizounganishwa na Gridi ya Taifa ni Biharamulo na Ngara na katika Wilaya zilizobaki zinaendelea kupata umeme kutoka Nchi ya Uganda. Wilaya hizi zilizosalia zinategemewa kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa mara baada ya kukamilika kwa Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme ya Msongo wa Kilovolti 220 kutoka Benako hadi Kyaka ambapo Mtaalam Mshauri anaendelea na kazi ya kuandaa nyaraka kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi ambaye anatarajiwa kupatikana mwezi Desemba, 2024. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya

nyongeza. Kwanza nipongeze Serikali kwa juhudi hizo zinazoendelea kuunganisha Mkoa wa Kagera na Gridi ya Taifa. Swali langu la kwanza; Mkoa wa Kagera umekuwa ukipata adha kubwa sana ya kukatika kwa umeme ambao kwa siku unakatika zaidi ya mara nane na wananchi wameendelea kupata adha kubwa. Je, nini mkakati wa Serikali wakati tunasubiria mpango wa kuunganisha na Gridi ya Taifa kuweza kuondoa adha hii wanayoipata? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Wilayani Kyerwa tuna vitongoji 668 na ambavyo vina umeme ni 245. Je, nini mkakati wa Serikali wa kupeleka umeme kwenye vitongoji hivi ambavyo bado havijafikiwa na umeme? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge katika Wilaya za Kyerwa, Karagwe na Missenyi umeme unakatika katika na hii ni kwa sababu kituo cha kupoza umeme kimezidiwa. Serikali tumeshaliona jambo hili na tulishalifanyia kazi. Tumepeleka *transformer* Kyaka lenye ukubwa wa *MVA* 20. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kazi ya kufunga *transformer* hii inaendelea na wataalam wameniambia ifikapo mwishoni mwa mwezi Septemba, *transformer* hii itaanza kufanya kazi. Hivyo maeneo yote ya Kyerwa, Karagwe na Missenyi suala la kukatika katika kwa umeme litapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali la pili, la vitongoji 245 kuwa na umeme kati ya vitongoji 668, kwa sasa tumeshasaini mkataba wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 3,060 na mwaka huu wa fedha tunaenda kusaini mkataba pia wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 10,000. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge watu wa Kyerwa pia watanufaika na miradi hii mikubwa miwili ya kupeleka umeme kwenye vitongoji. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Tunza Issa Malapo kwa niaba yake Mheshimiwa Anatropia.

Na. 95

**Mtwara Kuunganishwa na Gridi ya Taifa**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST K.n.y. MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, lini Mkoa wa Mtwara utaunganishwa umeme kwenye Gridi ya Taifa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Mtwara utaunganishwa katika Gridi ya Taifa na kuufanya kuwa na umeme wa kutosha na wa uhakika mara baada ya kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovolti 220 kutoka Songea hadi Mahumbika kupitia Tunduru na Masasi. Mradi huu upo katika hatua za utekelezaji na unatarajiwa kukamilika katika Mwaka wa Fedha wa 2025/2026. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa huu Mkoa haujaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa kumekuwa na changamoto ya kukatikakatika umeme kama ilivyokuwa katika Mkoa wa Kagera. Changamoto ya kukatika kwa umeme imekuwa ikipelekea kuharibika kwa vifaa na kuungua kwa nyumba za watu. Natoa mfano kuna mwananchi wa Wilaya ya Kyerwa anaitwa Ramson Greshen ni Mwalimu wa Shule ya Msingi Mkombozi. Adha ya kukatika kwa umeme imesababisha kuungua kwa nyumba yake. Nataka kauli ya Serikali watu wanaopata adha ya kukatika kwa umeme kama huyu wanapewa fidia namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa sasa imepata taarifa kwamba waratibu wa *REA* maeneo mbalimbali ikiwepo Mkoa wa Kagera wamepewa barua za kusitisha

mikataba yao na kumaliza kazi. Nataka kujua hatma ya miradi ya *REA* wakati ambapo waliokuwa wanaratibu wamepewa barua ya kusitishiwa mikataba yao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu swali moja tu hili la fidia halimo katika swali la msingi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la fidia, wahanga wote ambao wanapata madhara yanayosababishwa na hitilafu za umeme utaratibu upo. Utaratibu ni kwamba *EWURA* wanashughulikia kupitia taasisi zao, kujiridhisha kama madhara hayo yanatokana na mifumo ya taasisi zetu na baada ya hapo kama inafanyika hivyo basi kuna taratibu za mwananchi kupatiwa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namshauri mwathirika huyu ambaye tunampa pole sana afuate taratibu za kisheria zilizopo na kama ana manufaa yake kwa majanga aliyopata basi tunamhakikishia ataweza kulipwa fidia kutokana na hasara aliyoipata, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa mkandarasi anayejenga hiyo *line* kutoka Songea hadi Masasi anafanya kazi kwa kusuasua kwa sababu ana madai ambayo hajalipwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kumwezesha haraka ili aendelee na ujenzi wa mradi huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mkandarasi anayepeleka umeme kutoka Songea hadi Mahumbika ni Kalpataru. Mkandarasi huyu tayari alikuwa *site*. Serikali tunafahamu umuhimu wa Mkoa wa Mtwara na Lindi kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa. Kwa hiyo, kwa umuhimu huo tunawasiliana kwa karibu na wenzetu wa Wizara ya Fedha

ambao hivi karibuni wametuhakikishia kwamba mkandarasi huyu atawezeshwa ili kazi iweze kufanyika kwa haraka zaidi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Mwakasaka Adamson, kwa niaba Mheshimiwa Rehema.

Na. 96

**Polisi Kujigeuza kuwa Mahakama**

**MHE. REHEMA J. MIGILA K.n.y. MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Je, polisi kujigeuza kuwa Mahakama siyo kuvunja sheria?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Majukumu ya Jeshi la Polisi yameainishwa kwenye Sheria ya Polisi na Polisi Wasaidizi Na. 322 kifungu cha 5, inayoeleza ni kulinda amani, kudumisha sheria, amri na utulivu, kuzuia na kugundua uhalifu, kukamata na kuwalinda watuhumiwa na kulinda mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa matakwa ya sheria, Jeshi la Polisi hupokea malalamiko, hufanya uchunguzi na upelelezi, hukamata wahalifu na kisha jalada la kesi hupelekwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa hatua ya kwenda Mahakamani. Hivyo, Jeshi la Polisi halifanyi kazi za Mahakama isipokuwa hushirikiana na Mahakama katika kutekeleza matakwa ya kisheria kama kusimamia amri za Mahakama. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rehema.

**MHE. REHEMA J. MIGILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, sina swali la nyongeza.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

Na. 97

**Huduma za Abiria wenye Mahitaji Maalum kwenye Viwanja vya Ndege**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kushughulikia huduma za abiria wenye mahitaji maalum na wagonjwa kwenye viwanja vya ndege?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa inaweka miundombinu na vifaa wezeshi ili kuhakikisha huduma kwa abiria wenye mahitaji maalum na wagonjwa wanapata huduma stahiki katika viwanja vya ndege. Hii ni pamoja na kusanifu na kujenga majengo ya abiria sambasamba na miundombinu wezeshi kama vile maliwato maalum *(disabled toilet),* ngazi za mjongeo *(ramp),* usimikaji wa ngazi za umeme *(lift escalators)* na kuhakikisha kuwa kunakuwepo na vifaa maalum vya kuwahudumia abiria wenye mahitaji maalum pamoja na wagonjwa katika viwanja vya ndege kama vile viti vya magurudumu *(wheelchair);* pia, katika kuhakikisha uwepo wa watoa huduma wanaowahudumia watu wenye mahitaji maalum na wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa watu wenye mahitaji maalum pamoja na wagonjwa katika foleni za ukaguzi wa abiria *(screening)* na foleni za kuingia ndani ya ndege *(boarding)* kuufanya usafiri wa anga kuwa rafiki kwao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itaongeza viti mwendo vya umeme katika viwanja vyetu vya ndege na stesheni zetu, hasa *SGR* kwa kuwahudumia watu wenye mahitaji maalum?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa tumeshuhudia watu wenye mahitaji maalum wanapata shida sana wakisafiri hasa kwenye stesheni zetu za *SGR*. Je, ni lini Serikali itatoa mafunzo maalum kwa wahudumiaji wa watu hawa wanaposafiri katika stesheni zetu za *SGR* na viwanja vya ndege na vituo vya mabasi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi anavyopigania haki ya watu wenye mahitaji maalumu katika viwanja vyetu katika *SGR,* treni na usafiri mwingine wa mabasi. Serikali inayo nia na imekuwa ikifanya hivyo. Kama ambavyo nimesema kwenye swali la msingi, ujenzi wowote unaojengwa katika viwanja vyote unazingatia watu wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tayari tuna vitimwendo vya umeme ambavyo vinasimamiwa na watoa huduma katika maeneo mbalimbali ikiwemo *Swissport* na wengine. Pia, hata kwenye upande wa *SGR* au hata kwenye ndege unapokwenda kupanda usafiri huu wako watu wenye mafunzo, si tu pale unapokuwa unapanda lakini pia wapo na madaktari pamoja na fani mbalimbali katika afya ambao kama kutakuwa na changamoto yoyote wako tayari kwa ajili ya kuja kuhudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, tunapokea ushauri wake. Tutaendelea kuongeza ubora katika viwanja vyetu kulingana na mahitaji ya watu wenye mahitaji maalum hatua kwa hatua.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hili ni swali la msingi na hasa ukitazama *SGR* sasa imeanza kazi na inafanya kazi vizuri. Abiria wengi wenye ulemavu wanapata shida. Kwa hiyo, mchukue *action* ya haraka sana kuhakikisha huduma ya mahitaji ya watu wenye mahitaji maalumu wanapata usafiri salama na bora. Ahsante.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Abubakari Damian.

Na. 98

**Fidia kwa Wananchi Waliopisha Upanuzi wa Barabara ya Kidatu – Ifakara**

**MHE. ABUBAKAR D. ASENGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali italipa fidia kwa wananchi waliopisha upanuzi wa barabara ya Kidatu kwenda Ifakara kilometa 67?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la ulipaji wa fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi wa Barabara ya Kidatu – Ifakara yenye urefu wa kilomita 67 lilifanyika mwaka 2007 kwa kuzingatia Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007. Jumla ya wananchi 142 waliopisha ujenzi wa barabara hii walilipwa fidia ya jumla ya shilingi 2,576,081,789. Kwa wananchi ambao nyumba zao zipo ndani ya hifadhi ya barabara ya mita 22.5 kutoka katikati ya barabara hawakustahili fidia kwa mujibu wa sheria. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKAR D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naishukuru Serikali kwa fidia ya zaidi ya shilingi bilioni 2.5 ambayo wameitoa kwa wananchi wetu. Swali langu dogo ni kwamba; je, ni lini wananchi waliobakia bila kulipwa nje ya mita

22.5 watapewa majibu yao baada ya kupitiwa na Kamati ya Mheshimiwa *DC* na Meneja wa *TANROADS* mkoa ambayo waliiunda baada ya kuonekana kuna malalamiko ya baadhi ya wananchi hawajalipwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Asenga kuhusu fidia ya wananchi ambao wako kwenye nje ya mita 22.5. Cha kwanza kabisa naomba niweke rikodi sawa. Mwananchi yeyote ambaye yuko ndani ya mita 22.5 mwenye X nyekundu kwa mujibu wa sheria hastahili kulipwa fidia, lakini wananchi ambao wako kwenye mita 7.5 kila upande wa barabara kwa Sheria Namba 13 ya Mwaka 2007 tuliongeza upana wa barabara kutoka mita 45 kwenda mita 60, 7.5 kila upande wananchi hao huwa tunawawekea alama ya X ya kijani. Maana yake ni kwamba tutakapoanza kujenga barabara wananchi hao wanastahili fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nawaomba wale ambao wana alama ya X ya kijani tutakapoanza ujenzi, basi tutatoa fidia kwa mujibu wa sheria.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saputu.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika Barabara ya Mianzini – Sambasha – Ngaramtoni tunaishukuru sana Serikali kwa niaba ya wananchi kwa kulipa fidia baadhi nya wananchi zaidi ya shilingi bilioni 1.7, lakini kuna wananchi ambao bado hawajakamilishiwa fidia zao katika barabara hiyo. Nataka kujua ni lini Serikali itakamilisha kuwalipa fidia hao wananchi waliobaki ili barabara hiyo iendelee kwa sababu kwa sehemu fulani imesimama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimwagize Meneja wa *TANROADS,* Mkoa wa Arusha kuhakikisha

wananchi hawa wanaostahili malipo kwa mujibu wa sheria kama wanastahili basi walete Wizarani mara moja ili tuweze kufikisha Hazina kwa ajili ya mchakato wa malipo. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Shekilindi.

Na. 99

**Upanuzi wa Barabara ya Mombo hadi Lushoto**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanya upanuzi wa Barabara ya Mombo hadi Lushoto kwa kuwa ni nyembamba kiasi cha magari makubwa kushindwa kupita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami na upanuzi wa Barabara ya Mombo hadi Lushoto yenye urefu wa kilometa 31.36. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa barabara hiyo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Swali la kwanza; Wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa nini sasa Serikali isiruhusu magari machache kupita ili kupunguza gharama ya vifaa ambayo inasababishwa na gharama ya usafiri?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; eneo la Kwai lina kona ambayo ni kali sana na mara nyingi husababisha magari kufeli. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja katika eneo hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Shabani Shekilindi kuhusu maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu magari machache kupita, *concern* ya Mheshimiwa Mbunge tumeipokea. Nimwagize Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Tanga kufanya tathmini kwa kushirikiana na vyombo vingine ili kuona kama hili linawezekana kwa sababu *concern* yetu ni kuhakikisha watumia barabara wanakuwa salama. Kwa hiyo, kama itakuwa salama kwa mujibu wa tathmini tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kuweka daraja kwenye kona kali, kama nilivyosema Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia hili na tumefanya usanifu wa kina na tumekamilisha. Kwa hiyo, kwa kadri fedha zitakavyopatikana ujenzi wa daraja hili utakuwa ni kipaumbele. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tuna…, nani Mnzanda?

**MBUNGE FULANI:** Liseme jina lako.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa…

**NAIBU SPIKA:** Mbunge wa Lushoto.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni Mnzava

**NAIBU SPIKA:** Mnazava Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Moja ya njia ya kutatua changamoto ya barabara iliyoulizwa kwenye swali la msingi ni kutumia barabara mbadala ambayo ni ya kutoka Korogwe kupita Dindila – Bumbuli mpaka Soni. Kwenye bajeti Mheshimiwa Waziri aliahidi kuanza ujenzi wa

barabara hii kwa kiwango cha lami. Mpaka leo kuna ukimya, ni ipi kauli ya Serikali juu ya jambo hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakiri Mheshimiwa Mnzava amekuwa akifuatilia barabara hii ambayo ni mbadala kama alivyosema. Ni kweli na kwenye bajeti hii ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, tumetenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mnnzava pamoja na wananchi wake, kwamba kwa vile tumeiweka kwenye bajeti maana yake ni kipaumbele kwa upande wa Serikali na tuko kwenye hatua za kutekeleza bajeti hii. Kwa hiyo, fedha zitakapopatikana tutaijenga barabara hii ili iweze kuwahudumia wananchi lakini pia iwe kama mbadala wa ile barabara ya kwenda Bumbuli kutokea Lushoto. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Florence.

Na. 100

**Fidia kwa Wananchi wa Muhambwe**

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawalipa fidia wananchi wa Muhambwe waliopisha ujenzi wa Barabara ya Kibondo – Mabamba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha tathmini ya mali za wananchi zitakazoathiriwa na Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kibondo - Mabamba yenye urefu wa kilometa 47.925. Katika tathmini hiyo jumla ya wananchi 724 wakiwemo wananchi wa Muhambwe wanastahili kulipwa fidia yenye jumla

ya shilingi bilioni 1.29. Kwa sasa Serikali inakamilisha taratibu za malipo ya fidia kwa wananchi hao. Mara baada ya zoezi hilo kukamilika wananchi hao watalipwa fidia. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Dkt. Florence.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri. Hata hivyo, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Ujenzi wa Barabara hii ya lami ya kutoka Kibondo mpaka Mabamba umekwishaanza; na kama ilivyooneshwa kwenye majibu ya msingi, wananchi 724 wa Kata nne za Bitare, Misezero, Bunyanbo na Mabamba hawajalipwa fidia. Je, ni lini Serikali itaharakisha utaratibu huu ili wananchi hawa 724 waweze kupata fidia yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ujenzi wa barabara ya kilomita 25 ya Kibondo Mjini kwa jina la Kibondo *Town Link* kutoka *roundabout* ya Iheba mpaka Nduta *Junction* unasuasua mno kwa madai kwamba mkandarasi hajalipwa pesa na ameshatoa mitambo *site,* amepumzika anasubiri malipo. Je, ni lini Serikali itamlipa malipo yake ili aweze kurudi *site?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt. Florence kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fidia ya wananchi 724, kwanza nampongeza Dkt. Florence amekuwa akifuatilia fidia hii pamoja na miradi mingine ya barabara kwenye jimbo lake. Nimhakikishie, kwamba tumeshawasilisha maombi ya fidia Hazina na Wizara ya Ujenzi tutaendelea kufuatilia ili kuhakikisha haraka iwezekanavyo wananchi wanapata malipo hayo ya fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Kibondo Town Link* mkandarasi kucheleweshewa fedha, kwanza nimwagize mkandarasi asisimamishe ujenzi wa barabara hii. Sisi upande wa Wizara ya Ujenzi tumekwishawasilisha mahitaji ya malipo ya mkandarasi huyu Hazina. Kwa hiyo, tutaendelea kuweka jitihada

kuhakikisha mkandarasi hasimami. Pia ninamwelekeza aendelee na kazi wakati akisubiri malipo kwa *certificates* ambazo amewasilisha. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpembenwe.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara ya Bungu – Nyamisati tathmini imeshafanyika na wananchi wanasubiri kulipwa ili sasa shughuli nyingine za ujenzi wa barabara ile ziweze kuendelea. Je, Serikali ina kauli ipi katika kuweza kuwalipa wananchi wale wa Bungu Nyamisati fidia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Yahya pamoja na wananchi kwamba natambua barabara hii ya Bungo Nyamisati. Mheshimiwa Yahya amekuwa akiifuatilia sana na hata jana alikuja ofisini kufuatilia fidia hizi za wananchi na tunatambua barabara hii pia ni muhimu kwa wananchi wa Mafia. Kwa hiyo, Serikali inatambua umuhimu huu na tutafanya kila jitihada kuhakikisha fidia inalipwa ili kuweza kuruhusu ujenzi wa barabara hii kwa mujibu wa mipango yetu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kuna baadhi ya wananchi wa jimbo langu waliopisha ujenzi wa Barabara ya Bunda – Kisorya, bado hawajalipwa. Je, ni lini Serikali itakamilisha malipo yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kajege kuhusu fidia ya wananchi wa Barabara ya Bunda – Kisorya. Nimelichukua, tutafanya kila aina ya jitihada ili malipo ambayo tumeya-*process* kwa ajili ya fidia yaweze kufanyika. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Deo Sanga, kwa niaba yake, Mheshimiwa Getere.

Na. 101

**Ujenzi wa *One Stop Center* – Makambako**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE K.n.y. MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa *One Stop Center* Makambako?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi huu, kwa sasa, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili ujenzi wa mradi huu uweze kuanza. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Makambako wanaishukuru Serikali kwa kulipa fidia ya eneo la Idofya, lakini ni lini sasa kituo hiki cha *Stop Centre* kitajengwa katika eneo la Idofya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Mheshimiwa Waziri amekuwa ni Waziri wa nne kufika katika Barabara ya Sanzate – Nata na alipofika pale mara ya mwisho alisema hiyo barabara itamalizika mwezi Septemba mwaka huu; mpaka sasa hiyo barabara haijamalizika na ni kero kubwa kwa wananchi wa Bunda. Je, ni lini barabara hii itamalizika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili yaliyoulizwa na Mheshimiwa Getere kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu lini, kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi upembuzi yakinifu na usanifu wa kina tumekamilisha na ni hatua muhimu katika maendeleo ya kuanza kwa ujenzi. Kwa hiyo, nimhakikishie, fedha itakapopatikana kwa vile tumeshajua gharama, basi tutajenga huu mradi pale Makambako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la pili; Barabara ya Sanzate – Nata, kwanza nampongeza Mheshimiwa Getere amekuwa akifuatilia, lakini nakiri kulikuwa kuna changamoto za mkandarasi huyu; na miradi yake kwenye mikoa ambayo ana kazi imekuwa ikisuasua. Serikali kwa maana ya Wizara tumechukua hatua, kuna miradi tumemnyang'anya ili aweze ku-*concentrate* na miradi michache huku tukimweka kwenye uangalizi, ukiwemo huu Mradi wa Sanzate – Nata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Getere pamoja na wananchi kuwa Serikali tuko kazini tutamsimamia mkandarasi huyu ili barabara hii iweze kukamilika. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Jimbo la Manyoni Mashariki kuna ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi wa Magari *(One-stop Inspection Centre)*. Ujenzi huu ulikuwa umefikia 60%, lakini ulisimama tangu 2016, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wanakamilisha ujenzi huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Chaya amekuwa akifuatilia jambo hili na nakiri Wizara ya Ujenzi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha tunafanya tathmini ya kuhakikisha miradi hii inakamilika na kulikuwa kuna changamoto

ambazo zilisababisha kukwama kwa miradi hii ya *One-stop Inspection Centre*. Kwa hiyo, namhakikishia Mbunge, Serikali tuko mbioni kuifufua hii miradi ili iweze kukamilika kwa sababu uhitaji wake bado ni muhimu tena ni muhimu zaidi kuliko ilivyokuwa huko mwanzoni. Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kassim Iddi.

**MHE. IDDI KASSIM IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini sasa Kituo cha Isaka kitaboreshwa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, umemwelewa?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijamwelewa vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kassim, rudia tena swali lako.

**MHE. IDDI KASSIM IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeuliza ni lini sasa Kituo cha *Stop Centre* cha Isaka kitaboreshwa? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Kassim Iddi, Barabara ya Kahama – Kakola kwa kweli amepambana sana. Nafurahi sasa hivi mkandarasi yuko *site* anaendelea na kazi. Kuhusu swali la pale Isaka naomba Mheshimiwa Iddi nikaangalie kwenye mipango yetu na baada ya hapa nitakaa na yeye ili nihakikishe nampa majibu sahihi ya kituo hiki. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Jacqueline Kainja.

Na. 102

**Ujenzi wa Viwanja vya Michezo Nchini**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Viwanja vya Michezo nchini katika ngazi ya Wilaya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la ujenzi wa miundombinu ya michezo ni la Serikali kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Michezo zikiwemo taasisi, mashirika, watu binafsi na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika kuhakikisha kuwa kila Wilaya inakuwa na viwanja vya michezo, hivi karibuni Serikali itazielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga mafungu katika bajeti zao ili kutekeleza miradi ya ujenzi wa viwanja vya michezo kwa maeneo yao. Tayari kuna halmashauri zimeanza utekelezaji huu ambazo ni:-

Halmashauri za Wilaya za Kinondoni (Uwanja wa *KMC*), Bukoba Mjini (Uwanja wa Kaitaba), Nyamagana (Uwanja wa Nyamagana) na Namungo (*Majaliwa Stadium*). Aidha, Halmashauri ya Wang'ing'ombe inajenga Kijiji cha Michezo ambacho kitakapokamilika kitakuwa na viwanja vya michezo ya soka, *volleyball*, *Netball* na *Basketball*. Pia, Halmashauri ya Sengerema, Mkoani Geita imeandaa '*Concept Design*' kwa ajili ya kituo cha michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali ipo kwenye ukarabati mkubwa wa viwanja vya Uhuru na Benjamin Mkapa. Hata hivyo, Serikali inaendelea na ujenzi wa Uwanja wa Arusha (*Arusha Stadium*) na ukarabati wa viwanja vingine vitano vya mazoezi kwa ajili ya mashindano ya *CHAN* 2024 na *AFCON* 2027. Hivyo basi, nitoe rai kwa halmashauri, wilaya na mikoa ambayo haijaguswa na miradi ya *AFCON* 2027 kuanza kuunga mkono jitihada za Serikali kwa kujenga viwanja vya kisasa vya michezo ili pia wapate vyanzo vipya vya makusanyo ya maduhuli katika maeneo yao. Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza; tuna taasisi kubwa ambayo imewekeza katika wilaya zote za nchi hii viwanja vizuri vya mpira lakini ni chakavu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inashirikiana na taasisi hii ili kuboresha viwanja hivi hasa katika halmashauri ambazo hazina mapato ya kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; tuna wilaya 139 katika nchi hii na ambazo Waziri mejibu katika swali langu ambazo zimeanza kufanya marekebisho ni wilaya sita. Je, wameshafanya tathmini ya kuangalia bajeti ya Wilaya zote, ukarabati wa viwanja ni kiasi gani ili wanapoelekeza halmashauri ziweze kukusanya fedha kwa ajili ya ukarabati huu? Je, kila halmashauri inahitaji fedha kiasi gani hasa katika Halmashauri ya Wilaya ya Urambo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kama ambavyo nilishajibu kipindi cha nyuma, bado Serikali inafanya majadiliano na taasisi husika ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja kuhusu namna ambavyo tunaweza kufanya ukarabati na namna fedha ambazo tutazitumia zitaweza kurudishwa kwenye mfuko wa umma ambao tutazitoa. Hata hivyo, lengo hasa ni kwa Serikali kuutumia Mfuko wa Maendeleo ya Michezo ambao kwa sasa unapata asilimia tano ya mapato kutoka kwenye *sports betting*. Lengo letu ni kuutunisha Mfuko ule kwa kuuongezea vyanzo vipya vya mapato ili kuhakikisha unakwenda kuleta athari chanya hasa kwenye maendeleo ya michezo nchini ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya michezo. Kwa hiyo, tutakapokuwa tayari, hata majadiliano na taasisi ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja tutawapa taarifa na namna ambavyo tunakwenda kulitekeleza jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa sasa kwa mpango huu tulionao ambapo mamlaka husika tulizozitaja, mikoa, halmashauri na manispaa zinajenga viwanja vyake vya michezo, wajibu wa kupata gharama halisi ya kukarabati miundombinu hii bado

unabaki kwa mamlaka husika. Kwa ufahamu wangu, gharama zinatofautiana kutoka mamlaka moja mpaka nyingine, lakini tutakapokuwa tayari na hasa tutakapotaka kuzisaidia halmashauri ambazo hazina uwezo mkubwa wa kifedha kutengeneza viwanja hivi, tutaingia moja kwa moja pamoja na mambo mengine, kufanya tathmini ya kiasi gani kinahitajika kwa kila miundombinu ya michezo. Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Ikungi ni wilaya mpya kwa maana haina uwanja wa michezo na kwa sababu ni eneo ambalo linatoa wanamichezo wengi ikiwemo wanariadha na kwa sababu kulikuwa na mpango wa kujenga kiwanja cha ndege katika Kata ya Unyahati, Shule ya Sekondari Unyahati, ni lini sasa Serikali itatekeleza mpango huu wa kutujengea uwanja ambao mimi na wewe tulishawahi kufanya mazungumzo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**: Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimetangulia kujibu, kwa sasa hivi Serikali imejielekeza sana kwenye ujenzi wa miundombinu ambayo itatumika kwa ajili ya *CHAN* 2025 na *AFCON* 2027. Hata hivyo, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ametangulia kusema tumeshajadiliana mimi na yeye na miongoni mwa mipango ambayo Serikali inayo ni kuimarisha miundombinu ya michezo kila mahali. Hamu yangu ni kuona kwamba kila Wilaya, ikibidi kila Jimbo, liwe na miundombinu bora kabisa ya michezo, ni ile tu kwamba rasilimali fedha hairuhusu kwa sasa, lakini mipango bado ipo na kama ambavyo nimetangulia kusema huu Mfuko wa Maendeleo ya Michezo unaweza kutumika kutengeneza viwanja vingi nchini hasa kwenye halmashauri mpya na zisizo na uwezo kama ya Ikungi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, swali langu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwa nini Serikali isitoe maelekezo mahsusi kwa halmashauri za manispaa zote nchini kufikia mwaka 2027 ziwe zimejenga viwanja vya michezo ambavyo angalau vinabeba watu 5,000, 10,000 ili kuondokana na uhaba wa viwanja nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**: Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nilijibu wakati najibu swali la msingi, ni kwamba nitazielekeza Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutenga mafungu katika bajeti zao ili kuimarisha miundombinu ya michezo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, yuko mle mle ambako tulikuwa tumejibu kwenye swali la msingi kuhusiana na mpango wa Serikali kuzielekeza mamlaka hizi. Ni jambo ambalo linahitaji muda na kufuata utaratibu rasmi kabisa ili mamlaka hizi ziwe na wajibu wa kutekeleza wakati Serikali itakapotoa maelekezo haya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya Serikali siku zote yamekuwa ni mazuri, yanavutia, lakini utekelezaji umekuwa ni sifuri. Nataka kujua mkakati wa Serikali kujenga viwanja vizuri kwenye Mkoa wa Songwe kwa sababu changamoto imekuwa ni kubwa sana. Ni upi mpango wa Serikali ili tuone hiki inachokisema kinatekelezeka? Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**: Mheshimiwa Naibu Spika, nitajibu jibu hili hili kwa kila swali ambalo linahusiana na ujenzi wa miundombinu ya michezo, kwa sababu ukweli ni kwamba kwa sasa tumejielekeza kwenye miundombinu ya michezo kwenye viwanja vitakavyotumika kwa *CHAN* 2025 na *AFCON* 2027. Hayo mengine ni kwamba tunajipanga kutoa maelekezo kwa mamlaka za mikoa, halmashauri na manispaa ili zianze kujenga viwanja na miundombinu mingine ya michezo

kwenye maeneo yao kwa kadri ambavyo wataweza na Serikali itawasaidia hasa zile halmashauri ambazo hazitakuwa na uwezo mkubwa wa kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo nimejibu hapo awali ni kwamba lengo letu ni kutengeneza miundombinu ya michezo katika kila eneo, kila Jimbo, kila halmashauri na kila mkoa, lakini kwa sasa rasilimali fedha haituruhusu kufanya hivyo kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, tutakwenda taratibu kwa *phases* na tutafikia halmashauri ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja. Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Maida Hamad.

Na. 103

**Kuanzisha Mfumo wa Mafunzo kwa Vijana Maeneo ya Karibu na Kambi**

**MHE. MAIDA H. ABDALLAH** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha Mfumo wa Mafunzo yanayohusu uzalendo, ufundi, kilimo na ufugaji kwa vijana wanaoishi karibu na Kambi za Jeshi/ JKT?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Kujenga Taifa lilianzishwa chini ya kifungu namba 3(2) cha Sheria Na. 16 ya Mwaka 1964 kwa lengo la kuwajengea vijana moyo wa uzalendo, misingi ya kujitegemea na malezi kwa vijana wa Kitanzania pamoja na kuwafundisha umoja, mshikamano, ukakamavu na kuwa tayari kulitumikia Taifa lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua uhitaji wa sasa wa vijana kupewa mafunzo ya ukakamavu na stadi za kazi imeamua kufanya tathmini ya kina juu ya uwezo wa makambi yetu kuchukua idadi kubwa ya vijana, imeundwa Kamati ya Tathmini ambayo imeanza kazi na itakamilisha tathmini yake Juni, 2025 ambapo hata hili la vijana wanaozunguka makambi litakuwa ni miongoni mwa mambo yatakayofanyiwa kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maida.

**MHE. MAIDA H. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba niishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri ya Serikali inayoongozwa na Amiri Jeshi Mkuu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali ipo tayari kuongeza bajeti ya JKT ili kuwezesha vijana wengi zaidi kuchukuliwa kujiunga na JKT? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Serikali haioni kwamba mpango huu utawezesha vijana walio wengi kujifunza katika fani tofauti kwa masuala ya ulinzi karibu na jeshi na maeneo mengine? Pia, kuongeza ajira ikiwa ni njia mojawapo ya kukuza uchumi wa Taifa letu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la bajeti kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, sasa tumeunda timu maalum ya tathmini ili kuangalia uwezo wa makambi haya katika kuchukua vijana wengi zaidi na hili litakwenda sambamba na kuangalia uwezekano wa bajeti kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni kweli kwamba mpango wa kuongeza nafasi za vijana kujiunga na jeshi ni mpango ambao unaweza kuleta matokeo makubwa sana

kwenye kuwajengea uwezo hawa vijana, lakini kama nilivyosema, acha tumalize hii tathmini itakayotupa mwelekeo mzuri wa namna ambavyo tutachukua idadi kubwa zaidi ya vijana na hapo Serikali itazingatia vilevile ongezeko la bajeti na kadhalika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Monni.

Na. 104

**Skimu za Umwagiliaji – Chemba**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaendeleza Skimu za Umwagiliaji katika Kijiji cha Takwa na Kidoka vilivyopo katika Jimbo la Chemba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kukamilisha tathmini ya ukarabati wa Skimu za Umwagiliaji za Kidoka yenye ukubwa wa ekari 75 na Takwa yenye ukubwa wa ekari 500 ambayo kwa sasa inatumia miundombinu ya asili. Aidha, ujenzi wa skimu hizi utaanza Mwaka huu wa Fedha wa 2024/2025. Kukamilika kwa Skimu za Kidoka na Takwa zitawanufaisha wakulima 170 na 200 mtawalia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini

nina swali moja tu la nyongeza. Tulikuwa na mpango wa ujenzi wa mabwawa mawili kwenye Wilaya ya Chemba, Bwawa la Ndoroboni na Bwawa la Babayu, naomba kujua sasa ujenzi wake utaanza lini? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Monni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kama Serikali tunatangaza jumla ya mabwawa 100 kwa ajili ya kufanya usanifu na kila usanifu unavyokamilika tutakuwa tunatangaza bwawa hilo katika mwaka huo wa fedha au mwaka mwingine wa fedha. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge, mimi na yeye tuonane baadaye tuangalie haya mabwawa mawili kama yamo ndani ya mabwawa 100 ambayo yametangazwa kwa ajili ya kufanyiwa usanifu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kuishukuru Serikali ya Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutenga fedha kiasi cha shilingi 3,000,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa skimu ambayo imeharibika zaidi ya miaka 40, Kijiji cha Nyamgogwa, Kata ya Shabaka, Wilaya ya Nyangh'wale. Je, ni lini Serikali itatangaza zabuni ya ujenzi wa skimu hiyo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ukanda wa *Lake Victoria* kuanzia Mara, Simiyu, Geita na Mwanza sasa hivi wataalam wetu wanafanya kazi ya usanifu kwa ajili ya kuziangalia skimu na mabwawa ambayo yalishajengwa huko mwanzo na yakaharibika; na kwa kuwa, skimu hii ilipangwa kujengwa mwaka

huu wa fedha, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba usanifu ukikamilika tu itatangazwa kwa ajili ya kuanza kujengwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupitishia bajeti ambayo inajenga mabwawa matatu; Bwawa la Ari, Bwawa la Dirim. Je, ni lini wametangaza mabwawa haya ili yaweze kujengwa na wananchi wa Mbulu Vijijini wapate kumwagilia mashamba yao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Flatei, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni miongoni mwa mabwawa 100 ambayo yametangazwa katika Mkoa wa Manyara na nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa usanifu ukikamilika tu, mabwawa haya 100 ambayo yametangazwa sasa yataingia kwenye ujenzi. Tunatarajia usanifu utachukua kipindi cha miezi sita ili uweze kukamilika *and then* tuanze kutangaza mabwawa hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga.

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuniwekea bajeti kwenye Skimu ya Isebya – Mgelele, lakini pia kuna Skimu nyingine iliyoko Bukombe mpakani Bugerenga ambayo tuna-*share* na Naibu Waziri Mkuu. Sasa ni lini Serikali itatoa pesa ili kusudi kazi ziende kufanyika? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Maganga na ninamwomba kupitia Bunge lako Tukufu akubali mpango wa Serikali kutekeleza kwanza skimu hizi mbili za kwanza halafu na Jimbo la Bukombe tunazo skimu ambazo tunazitekeleza katika mwaka huu wa fedha. Tutaichukua skimu hii kuiingiza katika mpango wa mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza Skimu ya Umwagiliaji wa Bonde la Eyasi, Wilayani Karatu, wenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 38 ambao hadi sasa utekelezaji wake unasuasua? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli Eyasi kulitokea tatizo na msingi wa tatizo ulitokana na *design* ya awali, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali iko *committed* kuhakikisha kwamba tunajenga Skimu ya Eyasi na bwawa lake. Sasa hivi wameshafanya *review* ya *design* na mkandarasi atarudi *site* kwa ajili ya kuanza utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Mbunge na Mbunge wa Karatu kwa jitihada alizozifanya kufuatilia changamoto zilizotokea katika ujenzi wa Skimu ya Eyasi, nimhakikishie kwamba mkandarasi atarudi *site* na kuendelea na ujenzi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naishukuru Serikali kwamba imeweka kwenye bajeti hii tunayoendelea nayo ujenzi wa Skimu ya Metrom, Makeresho na Bwawa la Bolutu. Ni lini sasa Serikali itaanza kujenga skimu hizi

ambazo ni muhimu sana kwenye uzalishaji wa kilimo ndani ya Jimbo la Hai? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli skimu mbili pamoja na bwawa zimeshatangazwa, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa taarifa nilizonazo mimi kama Waziri, tumeshatangaza Skimu ya Makeresho na hiyo nyingine itatangazwa muda si mrefu, Makeresho imeshatangazwa sasa hivi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Kasulu ipo Miradi ya Umwagiliaji katika Kata ya Titye na Rungwe Mpya. Miradi hiyo ilianza, lakini miundombinu yake haijakamilika kutokana na ukosefu wa pesa. Je, ni lini Serikali itapeleka pesa ili kukamilisha miradi hiyo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tu nimjibu Mheshimiwa Genzabuke kwamba, nimezipokea hizi *scheme* mbili alizozitaja, nitaenda kuzifanyia kazi na nitampa majibu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba, tunahitaji hizi *scheme* za umwagiliaji kwa manufaa makubwa, lakini hivi karibuni kumekuwa na matukio ambayo yanasababisha kuwapoteza ndugu zetu na hasa watoto. Imetokea kule Nzega, lakini na Rorya tulipoteza watoto sita. Sasa, nataka kujua mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba, miundombinu ya mabwawa haya inaboreshwa *either* kwa kuweka uzio ikiambatana na alama za kuonesha kwamba, ni eneo hatarishi ili tusiendelee kupoteza ndugu zetu ikiwepo

sambamba na kujenga bwawa pembeni la kuchota maji au watoto wanavyoenda kwa *recreation* zozote zile? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, mabwawa yote tunayojenga sasa hivi, tunayajengea *fence,* kwa maana ya kuwa na uzio wa kuzunguka katika maeneo yote. Mabwawa yote tunayoyajenga tunatengeneza *spill over,* kwa maana ya kwamba, maji yakijaa yanaenda kwenye bwawa dogo ambalo litakuwa linatumika vilevile, kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *design* ya mabwawa mengi sasahivi tunabadilisha, kwa ajili ya siyo tu kulinda usalama wa watu pekeyake, lakini vilevile kulinda usalama wa matuta ya yale mabwawa ili yaweze kuishi kwa muda mrefu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru Wizara kuingiza kwenye bajeti Bwawa la Nyanzwa, kwa ajili ya umwagiliaji, lakini swali langu ni *Scheme* ya Ruaha Mbuyuni, bwawa lilibomoka muda mrefu na Mheshimiwa Waziri unafahamu. Ni lini sasa tutawasaidia wale wananchi kwa sababu, hali inazidi kuwa mbaya na mvua inakaribia? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Kamonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *Scheme* ya Ruaha Mbuyuni kila mwaka imekuwa ikibomoka na kila wakati tumekuwa tukienda kufanya *rehabilitation* ndogondogo kufanya watu wafanye kazi. Kwa hiyo kama Wizara tumeamua tu kufanya usanifu wa kina, kwa ajili ya ile *scheme* yote na pale pana maji mengi, ili tuweze kuijenga *complete,* kama ambavyo tumefanya mkombozi badala ya kuendelea kupoteza fedha kufanya *repair*

ndogondogo. Kwa hiyo, nawaomba wananchi wa eneo lile na wananchi wa Mkoa wa Iringa watuvumilie, usanifu unaendelea, ukikamilika tu itatangazwa, ili ijengwe *properly* tuondokane na hili tatizo la kujirudia kila wakati.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Shigongo.

Na. 106

**Ahadi Kuwakatia Maeneo Wananchi wa Maisome**

**MHE. ERIC J. SHIGONGO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatimiza ahadi ya kuwakatia eneo la Hifadhi Wananchi wa Kisiwa cha Maisome kwa kuwa idadi ya wakazi imeongezeka?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Msitu wa Maisome ilianzishwa mwaka 1955 kupitia Tangazo la Serikali Na. 355, ikiwa na ukubwa wa hekta 12,191.02. Kufuatia wananchi wa Kisiwa cha Maisome wanaoishi ndani ya hifadhi kuwa na uhitaji wa eneo, kwa ajili ya matumizi kwa shughuli mbalimbali za kijamii, Kisiwa cha Maisome kiliingizwa kuwa sehemu ya utatuzi wa migogoro ya vijiji 975 ambapo Baraza la Mawaziri liliridhia jumla ya hekta 2,871.782 zimegwe kutoka kwenye hekta 12,191.02 za eneo la hifadhi na hivyo, kufanya hifadhi kubakiwa na hekta 9,319.238.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tayari Wizara imekamilisha zoezi la kupitia mpaka wa hifadhi na kupima upya eneo lililobaki na tayari ramani mpya ya eneo hilo imeandaliwa. Aidha, Wizara imewasilisha Rasimu ya Tangazo la Serikali (Notisi ya Kusudio la Kutangaza Mabadiliko ya Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Maisome ya Mwaka 2024) kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ajili ya upekuzi ili kukamilisha taratibu za Kisheria za mabadiliko hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Eric.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Mwaka 1955 wakati hifadhi hii inaanzishwa Wananchi wa Vijiji vya Maisome walikuwa wakiishi mahali pale. Kwa sasa hivi eneo lililopo haliwatoshi kwa sababu, idadi ya watu imeongezeka. Mwaka jana wakati wa bajeti Wizara ilitoa siku 90 peke yake, ingekuwa imekamilisha mchakato huu. Swali la kwanza; sasa, wananchi wa Kata ya Maisome pamoja na Buhama wanataka kujua Serikali inatoa siku ngapi tena ili suala hili liweze kukamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa sababu, sasa hivi wananchi wakienda kusenya kuni msituni wanakamatwa na Maafisa wa *TFS*. Je, Serikali kabla mchakato huu haujakamilika, iko tayari kuwaruhusu wananchi waendelee kusenya kuni badala ya kukamatwa wanapokwenda kufanya kazi hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shigongo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipojibu swali kama hili Bunge lililopita, tulisema Serikali inakamilisha taratibu hizi ambazo nimezisema sasa kwamba, zimekamilika. Tunasubiria sasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ipitishe mabadiliko yale, ili tangazo rasmi litoke. Wakati ule nilisema tangazo lile likitoka, ndipo ambapo wananchi watapewa siku 90 za kuweza kueleza *either* kukubaliana na mabadiliko yale au kama wana hitaji lolote la nyongeza. Kwa hiyo, siku 90 ni baada ya tangazo kutolewa ndipo ambapo wananchi watapata muda huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, kuhusiana na wananchi kuruhusiwa kuokota kuni. Nataka nimhakikishie tayari mpango huo upo na sasahivi wananchi hawazuiliwi kukusanya kuni, kwa ajili ya matumizi yao ilimradi wanafuata utaratibu uliopangwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Je, ni lini Wizara ya Maliasili na Utalii itafika Jimbo la Momba kufanya ziara ili kushuhudia changamoto ya wananchi wa Mbao, Itumbula, *Moravian*, Tontela pamoja na Mbalwa. Changamoto ambazo wanazipitia baada ya kukosa sehemu ya kulima na hata sehemu ya kuokota kuni kwa sababu, wamezungukwa na hifadhi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ipo tayari kwenda kufanya ziara hiyo mara baada ya kuahirishwa kwa Bunge hili. Tutakaa na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kupanga kipindi sahihi cha kwenda kufanya ziara hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Nyatwali yenye Vijiji vitatu, Tamau, Serengeti na Nyatwali, imekuwa katika mgogoro mrefu wa kusubiria malipo, lakini vilevile wamekuwa wakiilaumu Serikali kwamba, wanataka kulipa fidia ndogo, tathmini wamefanya zaidi ya mwaka na tunasikia kuanzia Tarehe 05 wana mpango wa kuwalipa. Wanataka kujua wanalipwa kwa fidia ipi? Ileile ya malalamiko, mbali ya kwamba, wamekiuka taratibu zaidi ya miezi sita na hawajawalipa? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za fidia zinafahamika kwa mujibu wa Sheria. Uthaminishaji unapofanyika wananchi wanapaswa kulipwa kwa vigezo hivyo, lakini kama malipo yatakuwa yamechelewa zaidi ya miezi sita, upo utaratibu wa

kuwalipa pamoja na riba, kwa ajili ya kufidia muda uliopotea. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na imani kwamba, wananchi watapatiwa haki yao kama vile wanavyostahili. *(Makofi)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja ya Dharura.

**NAIBU SPIKA:** Kaa chini.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Wageni waliokaa Jukwaa la Spika:-

Wageni sita wa Mheshimiwa Spika, Wahitimu wa Shahada ya Uzamili katika Chuo cha St. Agustine, Tawi la Dar es Salaam, Kitivo cha Elimu, Mwalimu Emmy Kapulu, Mwalimu Shaibu Shaibu, Mwalimu Anastazia Kiria, Mwalimu Yasin Lukanga, Mwalimu Helena George Kilimo na Mwalimu Elizabeth Oscar. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Said Jafo, Waziri wa Viwanda na Biashara, hawa ni Viongozi kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo, Ndugu Needpeace Wambura, Kaimu Katibu Mkuu, Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Aggrey Mlimuka, Mwenyekiti wa Bodi Tume ya Ushindani, Ndugu William Erio, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushindani na Ndugu Hanifa Mohamed, Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Wageni 10 wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Hawa ni Viongozi kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Dkt. Anna Makakala, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji; *DCI* Gharibu Suleiman, Mwakilishi wa Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar; *CI* Gerald Kihinga, Kamishna wa Pasipoti na Uraia; *CI* Hamza Shaban, Kamishna wa Fedha na Utawala; *CI* Novaita Mrosso, Kamishna wa Huduma za Sheria; *CI* Angela Shija, Kamishna wa Vibali, Visa na Pasi; *DC*. Joseph Mtenga, Mkuu wa Kitengo cha Mipango; Ndugu Seperatus Fella, Katibu wa Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Biashara

Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu; Ndugu Alexander Lupilya, Katibu Msaidizi wa Sekretarieti; na Ndugu Ally Mussa Makame, Katibu Msaidizi wa Sekretarieti Zanzibar. Karibuni.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni tisa wa Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu kutoka Shirika la Kusaidia Watoto Tanzania, wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Ndugu Noelah Msuya. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo Wageni 30 wa Mheshimiwa Omary Juma Kipanga, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Viongozi na Wajumbe wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Mafia. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Wageni watatu wa Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga ambao ni Wahamasishaji na Waelimishaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura kutoka Jimbo la Mbogwe, Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, huyu ni mpiga kura wake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Oliver Semguruka ambaye ni mdogo wake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, ambao ni familia yake kutoka Mkoa wa Singida. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, hawa ni mama zake wadogo kutoka Mkoa wa Simiyu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah ambaye ni mpigakura wake kutoka Jimbo la Lindi Mjini, Mkoa wa Lindi. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, marafiki zake kutoka Shirika la Reli Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa ambao ni wapigakura wake kutoka Mkoa wa Geita. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 41 wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, hiki ni kikundi cha vijana wa Kijiwe Nongwa kutoka Mkoa wa Shinyanga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 175 wa Mheshimiwa Muharami Mkenge, ambao ni wanafunzi 165 na Walimu 10 wa Shule ya St. Theresa, Mapinga, Jimbo la Bagamoyo, Mkoa wa Pwani. Karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni 26 wa Mheshimiwa Assa Nelson Makanika, Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Kigoma na Madiwani wa Vyama vyote kutoka Jimbo la Kigoma Kaskazini wakiongozwa na Mbunge Mstaafu wa Jimbo hilo na Mwenyekiti wa Chama, Ndugu Halimeshi Mayonga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo:-

Wageni wanne ambao ni Kikundi cha Maombi cha Sayuni kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, semina iliyokuwa ifanyike jana, Tarehe 02 Septemba, kuhusu Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410. Sheria ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura ya 103 na Matumizi ya Takwimu, iliyoandaliwa na Ofisi ya Taifa ya takwimu, itakayotolewa na Wizara ya Fedha, itafanyika leo Tarehe 03 katika Ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa saba Mchana, mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, wakati natoa matangazo ya Timu ya Kampeni ya Bunge iliyokwenda Brazzaville kuongeza nguvu na ku-*support* uchaguzi wa Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, kwa bahati mbaya jina la Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama liliachwa na yeye ndiye alikuwa Kiongozi Mkuu wa Bunge kutafuta kura za mgombea wetu. Mheshimiwa Dkt. Kizito anafahamika kwa uwezo wake wa kampeni na kwa bahati, mwenzetu anazungumza Kifaransa, anazungumza Kireno, anazungumza Kijerumani. Kwa hiyo, Wajumbe wote kule, kura zilipatikana, kwanza kwa nguvu za Rais wetu Dkt.  Mama Samia na yeye akawa na mchango wake katika hili.

Sasa, ninamwita, kwa heshima na taadhima, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge, Daktari, Mkurugenzi Mkuu Bara lote la Afrika… *(Makofi)*

Waheshimiwa sijamaliza bado, mambo bado yapo mazito. Mwanachama, Mkereketwa Mkuu wa *Simba Sports Club,* Mnyama na sasa Simba inakwenda Afrika. Karibu hapa mbele Mheshimiwa Dkt. Ndugulile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, karibu.

**SHUKRANI**

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu muweza wa yote na kwa zawadi ya uhai, ambaye ameweza kutufikisha hapa siku ya leo. Pili, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na kumshukuru kwa kuridhia kwake na kuniruhusu kugombea nafasi hii ya Mkurugenzi wa Shirika la Afya, Kanda ya Afrika, lakini la pili, kwa *support* yake katika mchakato mzima wa safari hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampeni hii Mheshimiwa Rais aliibeba na ilikuwa ni ajenda yake ya kudumu pale alipokuwa anakutana na viongozi mbalimbali wa nchi, pale alipokuwa anasafiri na wale waliokuwa wanakuja ndani ya nchi. Kwa hiyo,

kwa njia ya kipekee kabisa napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa kufuatilia kwa karibu kampeni hii, pamoja na salamu zao za pongezi na kunitakia kheri. Mheshimiwa Waziri Mkuu na wewe nakushukuru sana na ninaomba unifikishie salamu zangu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia ya kipekee napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi ya kuja kushukuru katika Bunge lake hili, lakini kwa kuniunga mkono na *support* yake. Mheshimiwa Spika amefanya kazi kubwa sana ya kuwasiliana na Waheshimiwa Maspika wenzake kuhakikisha kwamba pale ambapo tulikuwa tunapata ugumu katika baadhi ya nchi, Mheshimiwa Spika aliwasiliana na Waheshimiwa Maspika wa nchi hizo husika na kutuombea kura. Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini haikutosha, Mheshimiwa Spika naye aliruhusu Waheshimiwa Wabunge wake kuweza kushiriki katika kampeni hii. Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mheshimiwa Elibariki Kingu, Mheshimiwa Neema Lugangira, Mheshimiwa Shamsia Mtamba, Mheshimiwa Mwenisongole. Pia kuna Wabunge wengine nao walishirikiana na mimi ambao wapo katika *forum* mbalimbali ambao wana mawasiliano na Wabunge mbalimbali katika Bara la Afrika nao kwa njia moja au nyingine nao nawatambua na kuwashukuru sana kwa mchango wao mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Katibu wa Bunge na Watumishi wa Bunge. Nao katika safari hii kwa kweli nao walinipa ushirikiano mkubwa sana, katika mchakato huu ilibidi wakati mwingine nisishiriki vikao vya Kamati na vya Bunge, lakini Katibu wa Bunge alikuwa anafuatilia kwa karibu na kunipa *support* kubwa sana, natumia nafasi hii naye kumshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri nao nilipata meseji nyingi sana kabla ya uchaguzi na baada ya uchaguzi kunipongeza. Vilevile, hapa niwashukuru sana na hili nataka niliseme, tulienda na Mawaziri wawili Congo Brazzaville. Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Mahmoud Thabit Kombo akiwa na wiki tatu tu tangu kuteuliwa kuwa Waziri lakini kazi aliyoifanya ilikuwa kazi kubwa sana, naomba kumpongeza sana Waziri wa Mambo ya Nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Waziri wa Afya, Mheshimiwa Jenista Mhagama. Ninaomba huyu tumpigie makofi makubwa sana, alikuwa ana wiki mbili tu tangu ateuliwe kuwa Waziri wa Afya, lakini akiwa pale Congo Brazzaville ilikuwa kana kwamba ana muda wa miaka mitano, maana yake Mawaziri wote aliwavaa. Kwa hiyo, ninakushukuru sana Mheshimiwa Jenista Mhagama. Pia ninamshukuru sana Mheshimiwa Stergomena Tax na yeye alitumia *influence* yake kubwa sana tukiwa Harare kuzifikia Nchi mbalimbali za *SADC*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Stergomena Tax, naye namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Mawaziri waliopita, waliohudumu katika Wizara ya Mambo ya Nje. Mheshimiwa January Makamba, Mheshimiwa Ummy Mwalimu nao katika hatua za awali kampeni hii waliibeba sana kwa hiyo nao napenda kuwashukuru sana kwa mchango wao mkubwa. Niwashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara: Wizara ya Mambo ya Nje, Wizara ya Afya na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kweli nao walinipa ushirikiano mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, timu yetu ya kampeni ilikuwa na wawakilishi kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Wizara ya Afya ikiongozwa na Wenyeviti wenza Balozi Robert Kahendaguza na Naibu Katibu Mkuu, Grace Magembe. Kwa kweli nawashukuru sana kwa kazi kubwa ambayo waliifanya, Mabalozi wetu wote wa Tanzania wanaotuwakilisha nje ya nchi, wote walishiriki kuhakikisha kwamba jambo letu hili linakwenda vizuri, nao nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jambo ambalo lilituunganisha Watanzania lilikuwa ni mchakato wangu. Hakuna *comment* mbaya ambayo niliiona kwenye mtandao, nao nataka kuwashukuru sana Watanzania wote na vijana wote ambao walihakikisha kwamba tunafanya kampeni ya kistaarabu na katika mitandao nao nawashukuru sana vijana wote. Pia Wana-Kigamboni nawashukuru, walinibeba miaka kumi na tano kama mwakilishi wao na wameni-*support* sana na mpaka sasa hivi wanaendelea kunipa *support* katika utumishi huu. Vilevile, niwashukuru Mawaziri wa Afya wa Bara Zima la Afrika kwa kuniunga mkono na kunichagua kuwa Mkurugenzi katika nafasi hii ya Kanda. Nafasi hii si ya kwangu, nafasi hii ni ya Nchi ya Tanzania vilevile nafasi hii ni ya Bara zima la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaposimama hapa ninakuwa Mtanzania wa kwanza kushika nafasi hii lakini vilevile ninakuwa Mwanaafrika Mashariki wa kwanza kushika nafasi hii. Nafasi hii nakwenda kuwa Kiongozi Mkuu wa Sekta ya Afya katika Nchi 47 katika Bara la Afrika, nafasi hii nakwenda kuwahudumia Waafrika bilioni 1.5, nafasi hii ni ya miaka mitano na endapo nitafanya vizuri basi unaweza ukachaguliwa tena kwa muda wa miaka mitano kwa hiyo jumla ni miaka kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha kazi kitakuwa Congo Brazzaville na wengi wamekuwa wananiuliza lini ninaanza kazi? Utaratibu wa Taasisi za kimataifa toka uchaguzi mpaka unaanza kazi unapewa miezi sita. Kwa hiyo natarajia kuanza kazi mwishoni mwa mwezi Februari, 2025 au Machi 2025. Sasa wale waliokuwa wanahoji kwamba Jimbo la Kigamboni liko wazi, hapana bado lina Mbunge, bado nipo nipo na nawashukuru sana wote wenye nia njema na ambao hawakuwa na nia njema wote waliniunga mkono na walikuwa na dua zao katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bara la Afrika lina mafanikio makubwa katika sekta ya afya lakini lina changamoto. Tumebakiza miaka sita kuelekea mwisho wa maendeleo endelevu *SDGs* na katika hili tunahitaji sasa kuwa na uongozi imara, uongozi mwenye maono katika kuhakikisha kwamba Bara la Afrika tunaweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nime-*campaign* katika sura ya kuonesha kwamba Bara la Afrika linahitaji mtu ambaye ana uwezo katika masuala ya kitaaluma, mwenye uwezo katika masuala ya kiuongozi. Kwa maana ambaye ameshawahi kushika nafasi za kiuongozi, lakini mtu ambaye vilevile ana sifa za kisiasa, ambazo zitakwenda kumweka mwananchi wa kawaida katika Bara la Afrika kama ni kiungo kikuu katika utoaji wa huduma wa afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishindana na watu ambao ni wabobevu na wazoefu katika hii Taasisi ya *WHO* lakini nashukuru kwamba Mawaziri wa Afya walituelewa kwamba ni aina gani ya uongozi ambao tunahitaji katika bara letu. Maeneo makubwa manne ambayo tuliyaongelea ni kwamba tunataka tuhakikishe kwamba huduma za afya zinapatikana kwa wananchi wa Bara la Afrika, lakini Bara la Afrika linajiandaa vizuri katika majanga makubwa ambayo yanajitokeza kama vile *COVID-19* na sasa hivi tuna baa la *Mpox.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunakwenda kuimarisha mashirikiano ya taasisi mbalimbali ambazo zinafanyika katika Bara la Afrika na kwa njia ya kipekee nilikuwa nanong'ona na Mheshimiwa Spika, Mabunge tumekuwa tunayaacha mbali sana. Katika uongozi wangu Mabunge ya Afrika yatakuwa ni sehemu ya kazi ambazo tutakuwa tunazifanya nikiwa kiongozi, lakini tunakwenda kuiboresha *WHO* kuhakikisha kwamba inakuwa imara na kusimama sekta ya afya katika Bara la Afrika na kuhakikisha kwamba nchi zinanufaika kutokana na nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi naendelea kujipanga, nimepewa miezi sita ya kujipanga kuiangalia taasisi, kuiangalia jinsi gani inavyofanya kazi, kuandaa maono yangu na kuhakikisha kwamba tutakapoanza kazi mwezi Machi, mwakani basi tunakwenda vizuri. Nia ya kufanya hivyo ninayo, sababu ya kufanya hivyo ninayo na uwezo wa kufanya hivyo ninao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge waendeleze sala na dua kwangu, jukumu hili ni kubwa

sana limebeba maono ya nchi yetu, lakini limebeba maoni ya Waafrika, Waafrika wana mategemeo makubwa sana. Kwa hiyo, kwa unyenyekevu mkubwa sana nimalizie kwa kuwashukuru sana sana sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano chini ya Mheshimiwa Rais na Serikali nzima na Waheshimiwa Wabunge kwa kuniunga mkono katika safari hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwepo katika kipindi hiki cha mpito, tunapokea maoni na ushauri. Kwa hiyo, nimalizie kwa kulishukuru sana sana Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusimama hapa mbele yenu na kutoa salamu zangu na shukurani zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache nikushukuru sana kwa kunipatia fursa ya kuja kushukuru. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, kila la kheri. *(Makofi)*

Ahsanteni.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mwongozo wa Spika…

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni.

Katibu.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mwongozo wa Spika…

**NAIBU SPIKA:** Kaa chini. *(Kicheko)*

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 *(The Fair Competition (Amendment) Bill, 2024)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Waziri wa Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nichukue fursa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 *(The Fair Competition (Amendment) Bill, 2024)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa malengo, ujasiri na uzalendo wa hali juu. Ninaomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wenzangu kuendelea kumwombea…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, subiri. Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge ninaomba utulivu ndani ya Bunge, Waheshimiwa Wabunge Bunge liko *live,* naomba utulivu ndani ya Bunge. Mheshimiwa Waziri, endelea.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuingoza nchi yetu kwa malengo, ujasiri na uzalendo wa hali juu. Ninaomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wenzangu kuendelea kumwomba Mwenyezi Mungu amjalie Rais wetu kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, ninaomba kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniteua na kuniamini kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara ninamhakikishia kuwa nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa weledi, uaminifu na ufanisi mkubwa ili kuliletea Taifa letu maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati; na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao vyote vya mijadala ndani ya Bunge letu Tukufu kwa umahiri na kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoongoza Bunge letu hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo majukumu yao ya Kikatiba kwa kutunga Sheria pamoja na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote na Manaibu Mawaziri wote walioteuliwa hivi karibuni na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Wizara mbalimbali za kisekta. Pia nampongeza Mheshimiwa Hamza Saidi Johari kwa kuteuliwa na kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kushika nafasi hii adhimu ya kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza pia Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu ya kikazi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ikiwemo kuandaa Muswada huu ambao ulisimamiwa kwa

karibu na Bwana Onorius Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria akishirikiana na Waandishi wa Sheria wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ninatambua na kuwashukuru kwa mchango wao mkubwa, tutazidi kuwaombea waendelee kutekeleza majukumu yao kwa weledi, ufanisi na kwa kuweka mbele maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie shukurani zangu za dhati kwa kuishukuru Kamati yetu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo inayoongozwa na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika kwa ushirikiano na ushauri ambao wameendelea kutupatia. Pia napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa mtangulizi wangu aliyekuwa Waziri wa Viwanda na Biashara kipindi hicho Dada yangu Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji kwa kusimamia Muswada huu akiwa kama Waziri wa Viwanda na Biashara. Vilevile naomba nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Ndugu yetu Dkt. Faustine Ndugulile amepewa dhamana kubwa katika Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024. Marekebisho hayo yanayopendekezwa yanakusudia kutatua changamoto mbalimbali zilizobainika katika utekelezaji wa masharti ya Sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria inapendekeza kufanyiwa marekebisho kwa ujumla kwa kufuta maneno "*court of competent*" na "*jurisdiction*" na "*court*" na badala yake kuweka maneno "*Commission*". Madhumuni ya marekebisho yaliyopendekezwa ni kuipa Tume mamlaka ya kipekee ya kushughulikia masuala ya kumlinda mlaji. Aidha, Sheria inarekebishwa kwa ujumla kwa kufuta maneno "*intentionally or* "*negligently*" popote inapoonekana kwenye Sheria. Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kuwa watu wanaotenda makosa yanayohusu ushindani hawakwepi adhabu kwa kisingizio cha kuwa hawakuwa na nia ovu wakati makosa ya ushindani ni dhahiri kulikuwa na nia ovu pia yanakuwa na yanaelekea kuharibu soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 2 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuboresha baadhi ya tafsiri za misamiati iliyotumika katika Sheria na kuongeza baadhi ya fasili ili kutoa tafsiri sahihi ya misamiati iliyotumika katika Sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 5 na cha 8 vinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuanzisha dhana ya "Hodhi ya Pamoja" na kuongeza viwango vya hodhi ya soko kutoka "asilimia 35 hadi 40". Madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa ni kuweka vikwazo dhidi ya matumizi mabaya ya hodhi ya soko inayohusisha mtu zaidi ya mmoja na kuendana na mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo yanayofanyika katika ngazi za kitaifa, kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 9 kinapendekezwa kurebishwa kwa kuanzisha kosa la ugawaji wa soko au wateja. Madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa ni kuwazuia washindani kugawana soko au wateja miongoni mwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 9A kinapendekezwa kuanzishwa ili kuweka masharti kwa ajili ya kuratibu, "Uratibu nafuu wa adhabu" ambao utahusisha utoaji nafuu ya adhabu kwa watu waliohusika katika kupanga au kutekeleza mipango ya vitendo vinavyolenga kufifisha ushindani, watakaojitokeza kutoa taarifa juu ya utendaji wa vitendo vyao. Madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa ni kusaidia Tume kugundua mipango ya vitendo vilivyolenga kufifisha ushindani, kurahisisha mchakato wa uchunguzi na kukuza ushirikiano katika kupambana na vitendo vinavyolenga kufifisha ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 10 pamoja na Jedwali la Marekebisho katika aya ya (a) kinapendekezwa kurebishwa kwa kuorodhesha mienendo isiyoruhusiwa kwa watu wenye hodhi ya soko. Madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza uwazi wa masoko ya matumizi mabaya ya hodhi ya soko kwa ajili ya utekelezaji ubora wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 10A kinapendekezwa ili kuweka masharti yanayozuia makubaliano baina ya watu walio

katika ngazi tofauti katika mnyonyoro wa uuzaji wa bidhaa. Madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha kuwa washindani wanashindana kwa haki na watumiaji wananunua bidhaa au huduma kwa bei ya ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 11A kinapendekezwa kuongezwa ili kuiruhusu Tume ya Ushindani kuidhinisha muungano wa kampuni yenye manufaa makubwa kwa umma. Vilevile, sehemu iliyopendekezwa inatoa vigezo vinavyounda manufaa hayo ya umma, madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha kuwa nchi inanufaika kutokana na muungano wa kampuni kwa maslahi mapana ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 17 pamoja na Jedwali la Marekebisho katika aya (b), inapendekezwa kufutwa kwa kuandikwa upya kwa kuweka sharti ya uuzaji wa bidhaa au huduma unao onesha bei ya kila bidhaa au huduma. Pia, kifungu hiki kinaweka masharti yanayozuia wauzaji wa bidha au huduma kutoza wateja bei zaidi ya ile iliyoainishwa kuwa ndiyo bei halisi ya bidhaa au huduma. Madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa ni kulinda walaji dhidi ya kutoza zaidi na kuhakikisha kuwa uhakika wa bei ya bidhaa au huduma kwa walaji kabla ya kununua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 33, 58 na 59 pamoja na Jedwali la Marekebisho katika aya ya (c), kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuendana na masharti mengine ya sheria yaliyofanyiwa marekebisho. Lengo la marekebisho ni kuhakikisha uwiano wa masharti ya Sheria. Vilevile, Kifungu cha 60 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha adhabu za jumla zitakazotumika katika Sehemu ya Sita na Saba ya Sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha uwiano wa masharti ya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 83 pamoja na Jedwali la Marekebisho katika aya (d), kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuainisha muda wa kuhudumu kwa wajumbe wa Baraza la Ushindani kwa kuzingatia msingi wa kupishana. Madhumuni ya

marekebisho hayo ni kudumisha kumbukumbu ya kitaasisi na urithishanaji mzuri wa ujumbe kwa utekelezaji bora wa majukumu kwa Baraza la Ushindani. Vilevile, marekebisho haya yatasaidia kuwa na mwendelezo wa shughuli za Baraza kutokana na muda wa Wajumbe kutoisha kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 61 na 84 vinapendekezwa kurekebishwa ili mtu ambaye hajaridhika na maamuzi ya Baraza la Ushindani aweze kukata rufaa katika Mahakama ya Rufaa ambayo itasikilizwa. Lengo la marekebisho hayo ni kutoa fursa kwa mtu ambaye hajaridhika na maamuzi ya Baraza kuweka au kutafuta haki yake katika chombo cha juu cha utoaji wa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 78 na 87 pamoja na Jedwali la Marekebisho katika aya (e), vinapendekezwa kurekebishwa ili kuliongeza Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania miongoni mwa taasisi zitazochangia Bajeti ya Tume na Baraza. Lengo la marekebisho yaliyopendekezwa ni kuongeza na kutambua vyanzo vya mapato vya Tume na Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 91 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa usitishaji wa moja kwa moja wa utekelezaji wa amri za Tume wakati wa rufaa za Baraza na badala yake usitishaji wa utekelezaji utafanyika baada ya kufanyika maombi. Madhumuni ya marekebisho haya yanapendekezwa ili kuzuia mashauri yanayolenga kuchelewesha utekelezaji wa amri za Tume na kuharakisha maamuzi ya uamuzi wa Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 96 kinapendekezwa kurekebishwa ili kutambua Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania Sura ya 415. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuanisha masharti ya utekelezaji wa Sheria ya Ushindani na Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena naomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ushindani ya mwaka 2024 *(The Fair Competition (Amendment) Bill, 2024),* pamoja na Jedwali la

Marekebisho yake na kuupitisha katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe Sehemu ya Sheria ya Nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MAELEZO YA MHESHIMIWA DKT. SELEMANI SAIDI JAFO (MB.) WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA, AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHINDANI WA MWAKA 2024 KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 (The Fair Competition Amendment Bill, 2024).

**Mheshimiwa Spika**, napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza Nchi kwa malengo, ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wenzangu kuendelea kumwomba Mwenyezi Mungu amjaalie Rais wetu kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, kwa heshima na taadhima, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniteua na kuniamini kuwa Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara. Ninamhakikishia kuwa, nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa weledi, uaminifu na ufanisi mkubwa ili kuliletea Taifa letu maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, ninawapongeza Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kupongeza Mawaziri wote na Manaibu Mawaziri wote walioteuliwa hivi karibuni na Mhe. Rais wa Jamhuri wa Tanzania katika Wizara za kisekta. **Pia,** nampongeza Mhe. Hamza Said Johari kwa kuteuliwa na kuaminiwa na Mhe. Rais kushika nafasi hii adhimu ya kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nawapongeza pia watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria mkuu wa Serikali kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ikiwemo kuandaa Muswada huu ambao ulisimamiwa kwa karibu na Bw. Onorius J. Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria akishirikiana na Waandishi wa Sheria wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tunatambua na tunashukuru kwa mchango wao mkubwa, tunazidi kuwaomba waendelee kutekeleza majukumu yao kwa weledi, ufanisi na kwa kuweka mbele maslahi ya Nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati yako ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo inayoongozwa na Mhe. Deodatus Philip Mwanyika kwa ushirikiano na ushauri ambao wameendelea kutupa. Pia napenda Kutoa shukrani kwa mtangulizi wangu katika Wizara ya Viwanda na Biashara Dkt. Ashatu Kijaji kwa kusimamia muswada huu akiwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka

2023. Marekebisho yanayopendekezwa yanakusudia kutatua changamoto mbalimbali zilizobainika katika utekelezaji wa masharti ya Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa ujumla kwa kufuta maneno "court of competent jurisdiction" na "court" na badala yake kuweka maneno "Commission". Madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa ni kuipa Tume mamlaka ya kipekee ya kushughulikia masuala ya kumlinda mtumiaji. Aidha, Sheria inarekebishwa kwa ujumla kwa kufuta maneno "intentionally or negligently" popote yanapoonekana kwenye Sheria. Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kuwa watu wanaotenda makosa yanayohusu ushindani hawakwepi adhabu kwa kisingizio cha kuwa hakuwa na nia ovu wakati makosa ya ushindani ni dhahiri kulikuwa na nia pia yanakuwa au yanaelekea kuharibu soko.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 2 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuboresha baadhi ya tafsiri za misamiati iliyotumika katika Sheria, na kuongeza baadhi ya fasili ili kutoa tafsiri sahihi ya misamiati iliyotumika katika Sheria hiyo.

Vifungu vya 5 na 8 vinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuanzisha dhana ya "Hodhi ya Pamoja" na kuongeza kiwango cha hodhi ya soko kutoka "asilimia 35 hadi 40". Madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa ni kuweka vikwazo dhidi ya matumizi mabaya ya hodhi ya soko inayohusisha mtu zaidi ya mmoja na kuendana na mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo yanayofanyika katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 9 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuanzisha kosa la "ugawanaji wa soko au wateja". Madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa ni kuwazuia washindani kugawana soko au wateja miongoni mwao.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 9A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti kwa ajili ya " Utaratibu wa nafuu

ya adhabu" ambao unahusisha utoaji wa nafuu ya adhabu watu waliohusika katika kupanga na kutekeleza mipango au vitendo vinavyolenga kufifisha ushindani, wanaojitolea kutoa taarifa juu ya utendekaji wa vitendo hivyo. Madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa ni kusaidia Tume kugundua mipango au vitendo vinavyolenga kufifisha ushindani, kurahisisha mchakato wa uchunguzi na kukuza ushirikiano katika kupambana na vitendo vinavyolenga kufifisha ushindani.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 10 pamoja na Jedwali la Marekebisho katika aya „A" kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuorodhesha mienendo isiyoruhusiwa kwa watu wenye hodhi ya soko. Madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza uwazi wa makosa ya matumizi mabaya ya hodhi ya soko kwa ajili ya utekelezaji bora wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 10A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti yanayozuia makubaliano baina ya watu walio katika ngazi tofauti katika mnyororo wa uuzaji wa bidhaa. Madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha kuwa washindani wanashindana kwa haki na watumiaji wananunua bidhaa au huduma kwa bei shindani.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 11A kinapendekezwa kuongezwa ili kuiruhusu Tume ya Ushindani kuidhinisha muungano wa kampuni wenye manufaa makubwa kwa umma. Vilevile, sehemu inayopendekezwa inatoa vigezo vinavyounda manufaa hayo ya umma. Madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha kuwa nchi inanufaika kutokana na muungano wa kampuni kwa maslahi mapana kwa umma.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 17 pamoja na Jedwali la Marekebisho katika aya „B" kinapendekezwa kufutwa na kuandikwa upya kwa kuweka sharti la wauzaji wa bidhaa au huduma kuonesha bei ya kila bidhaa au huduma. Pia, kifungu hiki kinaweka masharti yanayowazuia wauzaji wa bidhaa au huduma kutoza wateja bei zaidi ya ile iliyobainishwa kuwa ndiyo bei halisi ya bidhaa au huduma. Madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa ni kulinda walaji dhidi ya kutozwa zaidi na

kuhakikisha uhakika wa bei ya bidhaa au huduma kwa walaji kabla ya kununua.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 33, 58 na 59 pamoja na Jedwali la Marekebisho katika aya "C" kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kuendana na masharti mengine ya Sheria yaliyofanyiwa marekebisho. Lengo la marekebisho ni kuhakikisha uwiano wa masharti ya Sheria. Vilevile, kifungu cha 60 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kubainisha adhabu za jumla zitakazotumika katika Sehemu ya VI na VII ya Sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha uwiano wa masharti ya Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 83 pamoja na Jedwali la Marekebisho katika aya "D" kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuainisha muda wa kuhudumu kwa wajumbe wa Baraza la Ushindani kwa kuzingatia msingi wa kupishana. Madhumuni ya marekebisho hayo ni kudumisha kumbukumbu ya kitaasisi na urithishanaji mzuri wa ujumbe kwa utekelezaji bora wa majukumu wa Baraza la Ushindani. Vilevile, marekebisho haya yatasaidia kuwa na muendelezo wa shughuli za Baraza kutokana na muda wa wajumbe kutokuisha kwa pamoja.

**Mheshimiwa Spika,** vifungu vya 61 na 84 vinapendekezwa kurekebishwa ili mtu ambaye hajaridhika na maamuzi ya Baraza la Ushindani aweze kukata rufaa Mahakama Kuu ambayo itasikilizwa na majaji watatu. Lengo la marekebisho haya ni kutoa fursa kwa mtu ambaye hajaridhika na maamuzi ya Baraza kuweza kutafuta haki kwenye chombo cha juu zaidi cha utoaji haki.

**Mheshimiwa Spika**, vifungu vya 78 na 87 pamoja na Jedwali la Marekebisho katika aya "E" vinapendekezwa kurekebishwa ili kuliongeza Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania miongoni mwa taasisi zinazochangia bajeti ya Tume na Baraza. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza na kutambua vyanzo vya mapato ya Tume na Baraza.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 91 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa usitishaji wa moja kwa moja wa utekelezaji wa amri za Tume wakati wa rufaa kwa Baraza na badala yake usitishaji wa utekelezaji utafanyika baada ya kufanyika maombi. Madhumuni ya marekebisho yanayopendekezwa ni kuzuia mashauri yanayolenga kuchelewesha utekelezaji wa amri za Tume na kuharakisha uamuzi wa rufaa na Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 96 kinapendekezwa kurekebishwa ili kutambua Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania Sura ya 415. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwianisha masharti ya utekelezaji wa Sheria ya Ushindani na Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena naomba Bunge lako tukufu liujadili Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ushindani ya mwaka 2024 (The Fair Competition (Amendment) Bill, 2024) pamoja na Jedwali la Marekebisho yake na kuupitisha katika hatua ya kusomwa kwa mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe Sehemu ya Sheria za Nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, NAOMBA KUTOA HOJA.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa, namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 *(The Fair Competition (Amendment) Act, 2024)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza wakati wa Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge, Tarehe 15 Februari, 2024, baada ya kusomwa, uliamua kuuleta kwetu Muswada huu kwenye Kamati, ili uweze kufanyiwa kazi ikiwa ni utekelezaji wa Mamlaka uliyopewa chini ya Kanuni ya 97(1) ikisomwa kwa pamoja na Kanuni 136(14) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 97(1) ya Kanuni za Bunge niliyoirejea awali, inaweka masharti kwa Kamati iliyopangiwa Muswada wa Sheria kuujadili Muswada husika mapema iwezekanavyo. Kwa kutambua masharti hayo, Kamati ilifanya kazi ya kuchambua Muswada husika katika wiki ya kwanza ya vikao vya Kamati vilivyoanza Tarehe 12 hadi 16 Agosti, 2024, ikiwa ni utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Kamati kuchambua Muswada huu ni kupitia maudhui ya mapendekezo ya marekebisho ya sheria husika kwa kuzingatia maslahi ya Taifa na kutoa ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilianza kujadili na kufanya uchambuzi wa Muswada na baadaye kupokea na kujadili maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo, Mbunge, Siku ya Jumanne, tarehe 13 Agosti, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuzingatia masharti ya Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati iliwaalika wadau kuwasilisha maoni kuhusu Muswada huu kwa njia ya kielektroniki au kufika katika Kikao cha Kamati kilichofanyika Siku ya Jumatano, tarehe 14 Agosti, 2024. Katika kikao hicho, Kamati ilipokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Taasisi ya Sekta Binafsi, Kampuni ya Sigara Tanzania, Kampuni ya Tanzania *Breweries,* Kampuni za *cement* za Tanga na Simba, Lodhia *Group*, *ZIOTIO TRI, Cemex Ventures* na Maestro *Builders.* Maoni hayo pamoja na taarifa mbalimbali zilizopokelewa

zimeiwezesha Kamati kufanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu na kutoa mapendekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupokea ufafanuzi wa maelezo ya Serikali na kufanya uchambuzi wa Muswada, Kamati ilibainisha hoja mbalimbali ambazo iliziwasilisha Serikalini kama zilivyoainishwa katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa Muswada. Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024, unapendekeza kurekebisha Sheria ya Ushindani, Sura 285. Kamati ilielezwa kuwa, dhumuni la marekebisho yanayokusudiwa ni kutatua changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa sheria husika. Katika kujadili maudhui yake, Kamati ilifanya uchambuzi wa Ibara zote za Muswada na kutoa ushauri wa kuboresha baadhi ya Ibara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipitia Ibara zote za Muswada kwa kufanya uchambuzi wa kina. Kamati ilikubaliana kwa sehemu kubwa ya mapendekezo ya Muswada huo na kutoa maoni na ushauri katika baadhi ya Ibara kwa lengo la kuuboresha. Uchambuzi huo ikujumuisha maoni kwa baadhi ya Ibara ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 1 inataja jina la Sheria inayofanyiwa marekebisho ambayo itasomwa kwa pamoja na Sheria Kuu ambayo ni Sheria ya Ushindani, Sura ya 285.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 2 inapendekeza kurekebisha vifungu mbalimbali vya Sheria kwa lengo la kuiondolea Mahakama kushughulika na masuala ya ulinzi wa mtumiaji wa bidhaa na badala yake Tume ya Ushindani ishughulikie masuala hayo moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wa Kamati, kuliibuka mashaka juu ya uwezo wa Tume kushughulikia masuala hayo kwa nchi nzima kwa kuzingatia kuwa, kwa sasa Tume haina ofisi katika Mikoa yote. Vilevile, wadau waliibua mashaka kuhusu mgongano wa maslahi kwa Tume ya Ushindani kwa kuwa itakuwa

ikichunguza na kuchukua hatua moja kwa moja kwa masuala iliyoyachunguza yenyewe. Hata hivyo, wakati wa majadiliano na Serikali, Kamati ilijulishwa kuwa kulingana na aina ya makosa yaliyotajwa katika Ibara hizo, Tume itakuwa na uwezo wa kushughulikia masuala hayo kwa weledi na kwa ufanisi. Ni rai ya Kamati kuwa Tume ijipange ipasavyo katika kuhakikisha inaongeza uwezo katika kusimamia sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Tume kuwa na mgongano wa maslahi, ilionekana kuwa katika tasnia ya ushindani, mtindo wa Tume kuchunguza na kuchukua hatua ndiyo mtindo unaokubalika katika nchi nyingi. Vilevile, ikiwa mtu hataridhika na amri ya Tume, anayo nafasi ya kukata rufaa. Aidha, Ibara hii pia inarekebisha vifungu 8, 9, 10 na 11 vya sheria kwa kuweka makosa ya kiushindani yaliyopo katika vifungu hivyo kuwa makosa yasiyohitaji kuthibitishwa kwa kupima dhamira ya mkosaji *(intention)*. Lengo la marekebisho ni kuwezesha usimamizi thabiti wa Sheria ya Ushindani katika kuhakikisha wakiukaji wa sheria hii hawakwepi adhabu kwa kisingizio cha kutenda makosa hayo bila kudhamiria. Uchambuzi wa Kamati ulikubaliana na mapendekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 3 inarekebisha Kifungu cha 2 cha Sheria kwa kuboresha tafsiri ya neno mlaji kwa lengo la kuendana na uhalisia uliopo katika tasnia ya ushindani. Vilevile, marekebisho yanakusudia kuongeza tafsiri ya misamiati mipya iliyotokana na marekebisho yaliyopendekezwa. Uchambuzi wa Kamati kutokana na maoni ya wadau ulibaini kuwa, kumekuwepo na baadhi ya misamiati iliyotumika katika mapendekezo ya marekebisho lakini haijatafsiriwa. Misamiati hiyo ni pamoja na *unfair purchase, unfair selling prices, refusal to deal* na *tying and bundling* yaliyotumika katika Ibara ya 8 katika kueleza masuala ambayo yanahesabiwa ni matumizi mabaya ya hodhi ya soko *(abuse of dominance*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokutafsiriwa kwa maneno haya kunaweza kusababisha utata katika utekelezaji wa sheria hiyo na hivyo kudhoofisha usimamizi wake. Kamati iliishauri Serikali kuwa

misamiati hiyo itafsiriwe ili kuwezesha utekelezaji wa masharti ya sheria ya ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 4 na 5 inarekebisha vifungu vya 5(6) na 8(3) mtawalia kwa kusudio la kuongeza sifa za kuhodhi soko kuwa inaweza kuhusisha mtu mmoja au zaidi na kuongeza kiwango cha asilimia ya kuhodhi soko kutoka 35% au zaidi na kuwa 40% au zaidi. Kamati ilielezwa kuwa, kiwango kinachoongezwa kitachochea uwekezaji nchini na kwamba kinaendana na nchi nyingine zinazoendelea kutokana na mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo yanayofanyika katika ngazi ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Kamati ilikubaliana na maelezo ya mapendekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 6 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 9 cha sheria kwa kuongeza mikataba ya kibiashara inayolenga kuweka vikwazo vya kiushindani miongoni mwa washindani na kugawana soko au wateja katika maeneo mbalimbali ya nchi ili kudhoofisha ushindani katika biashara kuwa ni miongoni mwa mikataba isiyoruhusiwa. Kamati katika uchambuzi wake, ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 7 inapendekeza kuongeza Kifungu Kipya 9A ili kuweka utaratibu wa kikanuni utakaowezesha kutoa msamaha au unafuu wa adhabu kwa mtu aliyetenda kosa, lakini akatoa taarifa inayofichua uwepo wa mikataba, vitendo au mipango inayodhoofisha ushindani wa soko. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kifungu hiki kikitekelezwa ipasavyo, kitaisaidia Tume kwenye uchunguzi wa makosa ya kiushindani na hivyo kurahisisha usimamizi wa sheria. Kamati inashauri kuwa katika kutekeleza kifungu hiki, Tume izingatie masharti ya sheria zinazomlinda mtoa taarifa ili kuweza kupata ushirikiano wa wadau katika kupambana na vitendo vinavyolenga kudhoofisha ushindani wa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 8 inarekebisha Kifungu cha 10 kwa lengo la kuainisha baadhi ya mienendo isiyoruhusiwa katika kuhodhi soko. Mienendo hiyo ni pamoja na kuweka vigezo na masharti katika biashara ili kuwabagua wateja, kuzuia kiwango

cha uzalishaji na uuzaji wa bidhaa, kudhoofisha uvumbuzi na uwekezaji na kukiuka masharti ya ubunifu. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa baadhi ya maneno katika Ibara hii yanaweza kuleta utata na hivyo kushauri kuwa, maneno hayo yawekewe tafsiri kulingana na muktadha wake kama ilivyo katika Ibara ya 3 ya uchambuzi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 9 inapendekeza kuongeza Kifungu Kipya 10A. Kifungu hicho kinaweka masharti kwa watu wa ngazi tofauti katika mnyororo wa uuzaji wa bidhaa kutoingia katika makubaliano yenye lengo la kudhoofisha ushindani katika biashara. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, kifungu hiki kitawezesha walaji kununua bidhaa kwa bei shindani na hivyo kukidhi matakwa ya Sheria ya Ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 10 na 12 inarekebisha vifungu 11(1) na 13(1)(a) mtawalia, ili kuweka kwenye sheria misamiati inayotumika katika tasnia ya ushindani. Misamiati hiyo ni pamoja na *substantially lessens competition* badala ya maneno *creates or strengthens a position of dominance,* yaliyotumika katika sheria kwa sasa. Kamati katika uchambuzi wake ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 11 inapendekeza kuongeza Kifungu Kipya 11A ili kuweka vigezo na masharti ya upendeleo katika kuwezesha muunganiko wa kampuni ambazo kwa kawaida usingeruhusiwa, lakini kutokana na muunganiko kuwa huwa na manufaa kwa umma, unaweza kuruhusiwa. Kamati inashauri kuwa, Serikali isimamie vigezo vilivyoainishwa ipasavyo ili kuilinda jamii na madhara ya muunganiko unaoweza kutumika vibaya katika kuhodhi soko la bidhaa na huduma badala ya kuinufaisha jamii hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 13 inafuta Kifungu cha 17 cha Sheria na kukiandika upya kwa lengo la kuweka masharti ya wauzaji wa bidhaa na huduma kuonesha bei za bidhaa na huduma *(price indication or display)* badala ya bei husika kutamkwa na muuzaji. Vilevile imeelezwa kuwa, kosa la kukiuka

masharti hayo kwa watu wa kawaida ni kutozwa faini isiyopungua shilingi laki tatu na isiyozidi shilingi milioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati katika uchambuzi wake ilipata wasiwasi kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki hasa kwa wajasiriamali wadogo ikiwemo wauzaji wa chakula katika maeneo yasiyo rasmi maarufu mama lishe, watembeza bidhaa maarufu machinga, wafanya usafirishaji maarufu kama bodaboda, bajaji na wauzaji wa bidhaa ndogondogo magengeni. Wasiwasi ulionekana zaidi kwenye faini iliyopendekezwa kwa kuona inawezekana kuwaondoa sokoni wafanyabiashara wadogo badala ya kuwalinda na kuwakuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilishauri kwamba, kwa wauzaji wa bidhaa au huduma wenye mtaji usiozidi shilingi milioni nne, adhabu yao kwa kosa la kutoonesha bei ya bidhaa au huduma iwe ni faini isiyozidi shilingi elfu hamsini. Serikali ilikubali ushauri huo kwa kuahidi kufanya marekebisho kupitia jedwali na kuweka kiwango cha adhabu kuwa faini isiyopungua shilingi elfu kumi na isiyozidi Shilingi Milioni Moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeishauri Serikali kuwa Tume yenyewe ndio ihusike katika usimamizi wa kifungu hiki kutokana na kuwa na utalaam wa kipekee katika masuala ya ushindani. Vilevile imeshauri kuwa, katika kutekeleza kifungu hiki, Wizara itunge kanuni au mwongozo kuhusu utekelezaji wake ili kuepusha matumizi mabaya ya mamlaka yanayoweza kutendeka na baadhi ya watumishi wasio waaminifu, kwa kuwatoza wafanyabiashara wadogo faini kubwa kinyume na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwepo kwa masharti yanayoweka sharti la kuonesha bei ya bidhaa na huduma, Kamati ilielezwa kuwa madhara ya kutokuonesha bei ya bidhaa ni makubwa kwa walaji ukiwianisha na manufaa ya kuonesha bei yake. Kwa msingi huo, ni vema kuanza kuliko kuacha hali kama ilivyo sasa. Ni rai ya Kamati kuwa elimu ya kutosha itatolewa kabla ya kuanza kutekelezwa kwa kifungu hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 14 inarekebisha Kifungu cha 33 cha Sheria kwa kufuta maneno "hukumu" na badala yake kuweka maneno "amri" ili kuwianisha na marekebisho yaliyopendekezwa katika Kifungu cha 2 cha sheria. Kamati katika uchambuzi wake ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 15 inarekebisha Kifungu cha 58 cha Sheria kwa lengo la kuiwezesha Tume kuwa na mamlaka ya kusimamia masharti yanayohusu vigezo visivyowekwa wazi *(implied conditions)* katika mikataba ya walaji na wajibu wa wazalishaji wa bidhaa kadri yalivyoelezwa katika Sehemu ya Sita na Saba ya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Ibara inarekebisha Kifungu cha 58(5) ili kuiwezesha Tume kuwa na mamlaka ya kuamuru mali au hisa zilizopatikana kiasi cha kusababisha kuhodhi soko kurudishwa kwa muuzaji au kufuta ununuzi wa hisa au mali hizo katika muda wowote, tofauti na sasa ambapo Tume ina ukomo wa muda wa miaka mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kutambua lengo la marekebisho haya kuwa zuri, Kamati ilitathmini kwa mapana mapendekezo haya na kubaini kuwa, kukosekana kwa ukomo kunaweza kusababisha madhara hasi katika ukuaji wa uchumi. Mojawapo ya madhara ni kuweka mazingira magumu ya kufanikisha ukuaji wa biashara, kudhoofisha bidii ya kuvutia wawekezaji na ukuaji wa ubia. Kwa msingi huo basi, Kamati ilipendekeza ukomo wa Tume kuwa na mamlaka hayo uwe miaka kumi. Katika mashauriano, Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati ambayo yatazingatiwa kwenye jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 16 na 17 inarekebisha Kifungu cha 59 na 60 mtawalia kwa lengo la kuiwezesha Tume ya Ushindani kuwa na mamlaka ya kupokea maombi ya kulipwa fidia kutoka kwa watu walioathirika na ukiukwaji wa masharti yaliyopo katika Sehemu ya Sita na Saba ya sheria pamoja na kutoza faini kwa watu wanaotenda makosa yaliyoainishwa katika sehemu hiyo. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa marekebisho

haya yanakusudia kuwalinda walaji na hivyo kukubaliana na mapendekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 18 na 21 zinapendekeza kurekebisha Kifungu cha 61 na 84 mtawalia kwa lengo la kutoa haki ya kukata rufaa ndani ya siku thelathini kwenda Mahakama Kuu chini ya jopo la Majaji watatu, kwa mtu ambaye hataridhika na uamuzi wa Baraza la Ushindani. Tathmini ya Kamati ilionesha kuwa, mapendekezo haya yanalenga kutekeleza misingi ya utawala bora kwa kuwa Mahakama ndiyo chombo chenye kauli ya mwisho katika utoaji wa haki nchini kwa mujibu wa Ibara ya 107A ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa mapendekezo ya kifungu hiki yameainisha muda pekee wa kukata rufaa kuwa siku thelathini na kutoainisha taratibu nyingine. Kutokuweka namna na taratibu za rufaa zitakavyokuwa, kunaweza kusababisha wadau kushindwa kuitumia haki ya kukata rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, Kamati ilishauri kuwa Kifungu husika kiweke sharti la Waziri mwenye dhamana kutunga kanuni zitakazoweka taratibu za kukata rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mashauriano na Serikali, Kamati ilielezwa kuwa, katika kutekeleza ushauri huu, Waziri atatunga kanuni husika kwa kutumia kifungu kinachompa Waziri mamlaka ya jumla ya kutunga kanuni mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 20 inarekebisha Kifungu 83 kwa lengo la kumwezesha Mwenyekiti na Wajumbe wawili wa Baraza la Ushindani kukaa madarakani kwa kipindi cha miaka minne na Wajumbe wengine watatu kukaa madarakani kwa muda wa miaka mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, kupishana kwa muda huo na kuwepo kwa Wajumbe

wenye uzoefu kutawezesha Baraza la Ushindani kufanya kazi muda wote na kubadilishana uzoefu na hivyo kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 22 inarekebisha Kifungu cha 87(1)(c) kwa kuingiza maneno *'The Tanzania Shipping Agencies Corporation'* katika maneno *'Aviation Authority'* na *'and as such other'* yaliyopo kwenye aya (c). Kamati katika uchambuzi wake ilibaini kuwa mabadiliko yaliyopendekezwa yapo katika Kifungu cha 87(1)(d) na siyo Kifungu cha 87(1)(c) kama ilivyoelezwa kwenye Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vilevile, Kamati ilibaini kuwa neno *'such'* lililopo katika Muswada liangaliwe upya kwa maneno yaliyopo kwenye Kifungu cha 86(1)(d) cha sheria ni *'and other'* na siyo *'and such other'* kama ilivyoandikwa katika Muswada. Serikali iliukubali ushauri wa Kamati kufanya marekebisho ya Ibara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 23 inarekebisha kifungu cha 91 cha Sheria ili kuondoa masharti ya moja kwa moja ya kisheria ya kusitisha utekelezaji wa amri za Tume pale kunapokuwa na rufaa dhidi ya amri za Tume kwenye Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 24 inarekebisha kifungu cha 96 cha sheria kwa lengo la kuijumuisha Sheria ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania *(TASAC)* kuwa miongoni mwa Sheria ambazo zinaruhusiwa kukinzana na Sheria ya Ushindani. Uchambuzi wa Kamati ulikubaliana na mapendekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri; kutokana na uchambuzi wa maudhui na masharti mbalimbali katika Muswada huu, Kamati inayo maoni na ushauri kama ifuatavyo: -

(a) Mara baada ya mapendekezo ya Muswada huu kuridhiwa na Bunge hili, Sheria ya Ushindani Sura ya 285 ifanyiwe urekebu ili kujumuisha marekebisho haya katika urekebu huo. Kufanya hivyo, kutarahisisha usomaji, kueleweka na kupatikana kwa sheria hiyo katika uhalisia wake na hivyo kuchochea utekelezaji wake;

(b) Kwa kuwa wauzaji wa bidhaa na huduma watalazimika kuanza kuonyesha bei ya bidhaa na huduma, Serikali itoe elimu juu ya jambo hili kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, vikao vya wadau ikiwemo vyama vya walaji na wafanyabiashara ili jambo hilo liweze kueleweka kwa wauzaji na wanunuzi na hivyo kurahisisha utekelezaji wa Sheria;

(c) Waziri mwenye dhamana na masuala ya ushindani atunge kanuni ndani ya muda wa miezi sita baada ya kuanza kutumika kwa marekebisho ya Sheria hii ili kuwezesha utekelezaji wa masharti ya sheria yanayohitaji kanuni. Masharti hayo ni pamoja na taratibu za kukata rufaa kutoka Baraza la Ushindani kwenda Mahakama Kuu na taratibu kuhusu nafuu ya adhabu kwa mtu atakayefichua uwepo wa vitendo vya mikataba au mipango inayodhoofisha ushindani wa haki na

(d) Uwezo wa Tume ya Ushindani uzingatiwe ikiwemo kuongezewa watumishi na kuongeza Ofisi za Kanda na maeneo mengine nchini kulingana na mahitaji ili iweze kutekeleza majukumu yanayopendekezwa katika marekebisho yaliyowasilishwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni haya, yanatokana na matokeo ya Uchambuzi uliofanyika. Aidha, yamezingatia muafaka uliofikiwa kati ya Serikali na Kamati baada ya uchambuzi na mashauriano. Kwa ujumla, matokeo ya uchambuzi, makubaliano ya Kamati na Serikali na maoni ya Kamati, vitawezesha kuboresha Sheria itakayopitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; kwa mara nyingine tena ninakushukuru kwa uamuzi wako wa kuuleta Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Haki katika Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. Uzoefu wa Wajumbe katika Sekta ya Biashara umekuwa na mchango wa kutosha wakati wa uchambuzi. Aidha, utayari wa Wajumbe kupokea na kusikiliza maoni ya Wadau umesaidia kupata

mawazo yenye tija katika uzingatiaji wa maslahi ya umma wakati wa kujadili Muswada huu. Kwa hatua hii ninawashukuru tena Wadau mbalimbali waliotoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa ushirikiano mkubwa waliokuwa nao wakati wa uchambuzi wa Muswada. Weledi walionao na umahiri waliouonesha wakati wa uchambuzi umesaidia kufanikisha kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kwa taarifa hii Bunge litakuwa katika nafasi nzuri ya kuamua kwa kuzingatia maslahi ya Umma. Aidha, kwa kutambua mchango wa Wajumbe, ninaomba majina yao kama yalivyoainishwa yaingizwe katika kumbukumbu rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninaomba kumshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo; Naibu Waziri, Mheshimiwa Exaud Kigahe; wataalam wote wa Wizara na taasisi husika kwa ufafanuzi walioutoa wakati wa uchambuzi wa Muswada. Maelezo ambayo yamesaidia kufanikisha kazi ya uchambuzi wa Muswada huu kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninamshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc*, kwa kuwezesha na kuongoza kikamilifu shughuli za Sekretarieti katika kuratibu uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**3 SEPTEMBA, 2024**

## MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO KUHUSU MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHINDANI WA MWAKA 2024 KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo Kuhusu **Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 (The Fair Competition (Amendment) Act, 2024)**. Muswada huu ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza wakati wa Mkutano wa Kumi na Nne (14) wa Bunge, tarehe 15 Februari, 2024. Baada ya kusomwa, uliamua kuuleta Muswada huu kwenye Kamati ili uweze kufanyiwa kazi ikiwa ni utekelezaji wa Mamlaka uliyopewa chini ya Kanuni ya 97 (1) ikisomwa kwa pamoja na Kanuni 136 (14) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 97 (1) ya Kanuni za Bunge niliyoirejea awali, inaweka masharti kwa Kamati iliyopangiwa Muswada wa Sheria kuujadili Muswada husika mapema iwezekanavyo. Kwa kutambua masharti hayo, Kamati ilifanya kazi ya kuuchambua Muswada husika katika wiki ya kwanza ya vikao vya Kamati vilivyoanza tarehe 12 hadi 16 Agosti, 2024, ikiwa ni utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** lengo la Kamati kuchambua Muswada huu ni kupitia maudhui ya mapendekezo ya marekebisho ya sheria husika kwa kuzingatia maslahi ya Taifa na kutoa ushauri.

### 1.2 Mbinu zilizotumika kuchambua Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilianza kujadili na kufanya uchambuzi wa Muswada na baadae kupokea na kujadili Maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada yaliyowasilishwa na Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Selemani Saidi Jafo (Mb.), siku ya Jumanne, tarehe 13 Agosti, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuzingatia masharti ya Kanuni ya 97 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati iliwaalika wadau kuwasilisha maoni (Public Hearing) kuhusu Muswada huu kwa njia ya kielektroniki au kufika katika kikao cha Kamati kilichofanyika siku ya Jumatano tarehe 14 Agosti, 2024. Katika kikao hicho, Kamati ilipokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Taasisi ya Sekta Binafsi (Tanzania Private Sector Foundation-TPSF), Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC PLC), Kampuni ya Tanzania Breweries Ltd (TBL), Tanga Cement, Simba Cement, Lodhia Group, ZIOTIO TRI, Cemex Ventures Ltd na Maestro Builders. Maoni hayo pamoja na taarifa mbalimbali zilizopokelewa zimeiwezesha Kamati kufanya uchambuzi wa kina wa Muswada huu na kutoa mapendekezo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupokea ufafanuzi wa maelezo ya Serikali na kufanya uchambuzi wa Muswada huu, Kamati ilibainisha hoja mbalimbali ambazo iliziwasilisha Serikalini, kama zilivyoainishwa katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024, unapendekeza kurekebisha Sheria ya Ushindani, Sura ya 285(The Fair Competition (Amendment) Bill, 2024). Kamati ilielezwa kuwa, dhumuni la marekebisho yanayokusudiwa ni kutatua changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa sheria husika. Katika kujadili maudhui yake, Kamati

ilifanya uchambuzi wa Ibara zote za Muswada na kutoa ushauri wa kuboresha baadhi ya Ibara kama ifuatavyo.

## 2.2 Uchambuzi wa Maudhui ya Ibara za Muswada

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia Ibara zote za Muswada kwa kufanya uchambuzi wa kina kuhusu marekebisho yanayopendekezwa. Baada ya uchambuzi huo, Kamati ilikubaliana kwa sehemu kubwa na mapendekezo ya Muswada huu na kutoa maoni na ushauri katika baadhi ya Ibara kwa lengo la kuuboresha. Uchambuzi huo ikujumuisha maoni kwa baadhi ya Ibara hizo ni kama ifuatavyo: -

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 1 inataja jina la Sheria inayofanyiwa marekebisho ambayo itasomwa kwa pamoja na Sheria Kuu ambayo ni Sheria ya Ushindani, Sura ya 285.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 2 inapendekeza kurekebisha vifungu mbalimbali vya Sheria kwa lengo la kuiondolea Mahakama kushughulika na masuala ya ulinzi wa mtumiaji wa bidhaa na badala yake Tume ya Ushindani ishughulikie masuala hayo moja kwa moja.

Katika uchambuzi wa Kamati, kuliibuka mashaka juu ya uwezo wa Tume kushughulikia masuala hayo kwa nchi nzima kwa kuzingatia kuwa, kwa sasa Tume haina ofisi katika mikoa yote. Vilevile wadau waliibua mashaka kuhusu mgongano wa kimaslahi kwa Tume ya Ushindani kwa kuwa itakuwa ikichunguza na kuchukua hatua moja kwa moja kwa masuala iliyoyachunguza yenyewe. Hata hivyo, wakati wa majadiliano na Serikali, Kamati ilijulishwa kuwa kulingana na aina ya makosa yaliyotajwa katika Ibara hizo, Tume itakuwa na uwezo wa kushughulikia masuala hayo kwa weledi na kwa ufanisi. **Ni rai ya Kamati kuwa Tume ijipange ipasavyo katika kuhakikisha inaongeza uwezo wake wa kusimamia sheria hii.**

Kuhusu Tume kuwa na mgongano wa kimaslahi, ilionekana kuwa katika tasnia ya ushindani, mtindo wa Tume kuchunguza na kuchukua hatua ndio mtindo unaokubalika na kutumika katika

nchi nyingi. Vilevile, ikiwa mtu hataridhika na amri ya Tume, anayo fursa ya kukata rufaa.

Aidha, Ibara hii pia inarekebisha vifungu 8, 9, 10 na 11 vya sheria kwa kuweka makosa ya kiushindani yaliyopo katika vifungu hivyo kuwa makosa yasiyohitaji kuthibitishwa kwa kupima dhamira ya mkosaji (intention). Lengo la marekebisho ni kuwezesha usimamizi thabiti wa sheria ya ushindani katika kuhakikisha wakiukaji wa sheria hii hawakwepi adhabu kwa kisingizio cha kutenda makosa hayo bila kudhamiria. Uchambuzi wa Kamati ulikubaliana na mapendekezo ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 3 inarekebisha kifungu cha 2 cha Sheria kwa kuboresha tafsiri ya neno mlaji (consumer) kwa lengo la kuendana na uhalisia uliopo katika tasnia ya ushindani. Vilevile marekebisho yanakusudia kuongeza tafsiri ya misamiati mipya iliyotokana na marekebisho yaliyopendekezwa.

Uchambuzi wa Kamati kutokana na maoni ya wadau ulibaini kuwa kumekuwepo na baadhi ya misamiati iliyotumika katika mapendekezo ya marekebisho lakini haijatafsiriwa. Misamiati hiyo ni pamoja na unfair purchase, unfair selling prices, refusal to deal na tying and bandling yaliyotumika katika Ibara ya 8 katika kueleza masuala ambayo yanahesabiwa ni matumizi mabaya ya hodhi ya soko (abuse of dominance). Kutokutafsiriwa kwa maneno haya kunaweza kusababisha utata katika utekelezaji wa sheria na hivyo kudhoofisha usimamizi wake. **Kamati iliishauri Serikali kuwa misamiati hiyo itafsiriwe ili kuwezesha utekelezaji wa masharti ya sheria ya ushindani.**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 4 na 5 inarekebisha vifungu 5(6) na 8(3) mtawalia kwa kusudio la kuongeza sifa ya kuhodhi soko kuwa inaweza kuhusisha mtu mmoja au zaidi, na kuongeza kiwango cha asilimia ya kuhodhi soko kutoka asilimia thelathini na tano (35%) au zaidi na kuwa asilimia arobaini (40%) au zaidi. Kamati ilielezwa kuwa kiwango kinachoongezwa kitachochea uwekezaji nchini na kwamba kinaendana na nchi nyingine zinazoendelea kutokana na mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo yanayofanyika katika ngazi ya Kitaifa, Kikanda na

Kimataifa. Kamati ilikubaliana na maelezo ya mapendekezo ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 6 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 9 cha sheria kwa kuongeza mikataba ya kibiashara inayolenga kuweka vikwazo vya kiushindani miongoni mwa washindani na kugawana soko au wateja katika maeneo mbalimbali ya nchi ili kudhoofisha ushindani katika biashara kuwa ni miongoni mwa mikataba isiyoruhusiwa. Kamati katika uchambuzi wake, ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 7 inapendekeza kuongeza kifungu kipya 9A ili kuweka utaratibu wa kikanuni utakaowezesha kutoa msamaha au unafuu wa adhabu kwa mtu aliyetenda kosa lakini akatoa taarifa inayofichua uwepo wa mikataba, vitendo au mipango inayodhoofisha ushindani wa haki. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kifungu hiki kikitekelezwa ipasavyo, kitaisaidia Tume kwenye uchunguzi wa makosa ya kiushindani na hivyo kurahisisha usimamizi wa sheria. **Kamati inashauri kuwa katika kutekeleza kifungu hiki, Tume izingatie masharti ya sheria zinazomlinda mtoa taarifa ili kuweza kupata ushirikiano wa wadau katika kupambana na vitendo vinavyolenga kudhoofisha ushindani wa haki.**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 8 inarekebisha kifungu cha 10 kwa lengo la kuainisha baadhi ya mienendo isiyoruhusiwa katika kuhodhi soko. Mienendo hiyo ni pamoja na kuweka vigezo na masharti katika biashara ili kuwabagua wateja, kuzuia kiwango cha uzalishaji na uuzaji wa bidhaa, kudhoofisha uvumbuzi na uwekezaji na kukiuka masharti ya ubunifu. **Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa baadhi ya maneno katika Ibara hii yanaweza kuleta utata na hivyo kushauri kuwa maneno hayo yawekewe tafsiri kulingana na muktadha wake kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 3 ya uchambuzi huu.**

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 9 inapendekeza kuongeza kifungu kipya 10A. Kifungu hicho kinaweka masharti kwa watu wa ngazi tofauti katika mnyororo wa uuzaji wa bidhaa kutoingia katika makubaliano yenye lengo la kudhoofisha ushindani katika

biashara. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kifungu hiki kitawezesha walaji kununua bidhaa kwa bei shindani na hivyo kukidhi matakwa ya sheria ya Ushindani.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 10 na 12 inarekebisha vifungu 11(1) na 13(1) (a) mtawalia ili kuweka kwenye sheria misamiati inayotumika katika tasnia ya ushindani. Misamiati hiyo ni pamoja na "substantially lessens competition" badala ya maneno "creates or strengthens a position of dominance" yaliyotumika katika sheria kwa sasa. Kamati katika uchambuzi wake, ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 11 inapendekeza kuongeza kifungu kipya 11A ili kuweka vigezo na masharti ya upendeleo katika kuwezesha muunganiko wa kampuni ambao kwa kawaida usingeruhusiwa, lakini kutokana na muunganiko huwa kuwa na manufaa kwa umma, unaweza kuruhusiwa. **Kamati inashauri kuwa Serikali isimamie vigezo vilivyoainishwa ipasavyo ili kuilinda jamii na madhara ya muunganiko unaoweza kutumika vibaya katika kuhodhi soko la bidhaa na huduma badala ya kuinufaisha jamii hiyo.**

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 13 inafuta kifungu cha 17 cha Sheria na kukiandika upya kwa lengo la kuweka masharti ya wauzaji wa bidhaa na huduma kuonyesha bei za bidhaa na huduma (price indication or display) badala ya bei husika kutamkwa na muuzaji. Vilevile imeelezwa kuwa, kosa la kukiuka masharti hayo kwa watu wa kawaida ni kutozwa faini isiyopungua shilingi laki tatu na isiyozidi shilingi milioni moja.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika uchambuzi wake ilipata wasiwasi kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki hasa kwa wajasiriamali wadogo ikiwemo wauzaji wa chakula katika maeneo yasiyo rasmi maarufu mama lishe, watembeza bidhaa maarufu machinga, bodaboda na wauzaji wa bidhaa ndogondogo magengeni. Wasiwasi zaidi ulionekana kwenye faini inayopendekezwa kwa kuona inaweza kuwaondoa sokoni wafanyabiashara wadogo badala ya kuwalinda na kuwakuza. **Kamati ilishauri kwamba kwa wauzaji wa bidhaa au huduma wenye mtaji usiozidi shilingi milioni**

**nne, adhabu yao kwa kosa la kutokuonyesha bei ya bidhaa au huduma iwe ni faini isiyozidi shilingi elfu Hamsini.** Serikali ilikubali ushauri huo kwa kuahidi kufanya marekebisho kupitia jedwali na kuweka kiwango cha adhabu kuwa faini isiyopungua shilingi elfu kumi na isiyozidi shilingi Milioni Moja.

**Mheshimiwa Spika, Kamati imeishauri Serikali kuwa Tume yenyewe ndio ihusike katika usimamizi wa kifungu hiki kutokana na kuwa na utalaamu wa kipekee katika masuala ya ushindani. Vilevile imeshauri kuwa katika kutekeleza kifungu hiki, Wizara itunge kanuni au mwongozo kuhusu utekelezaji wake ili kuepusha matumizi mabaya ya mamlaka yanayoweza kutendeka na baadhi ya watumishi wasio waaminifu kwa kuwatoza wafanyabiashara wadogo faini kubwa kinyume na ushauri wa Kamati.**

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusu kuwepo kwa masharti yanayoweka sharti la kuonyesha bei ya bidhaa na huduma, Kamati ilielezwa kuwa madhara ya kutokuonyesha bei ya bidhaa ni makubwa kwa walaji ukiwianisha na manufaa ya kuonyesha bei yake. Kwa msingi huo, ni vyema kuanza kuliko kuacha hali kama ilivyo sasa. **Ni rai ya Kamati kuwa elimu ya kutosha itatolewa kabla ya kuanza kutekelezwa kwa kifungu hiki.**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 14 inarekebisha kifungu cha 33 cha Sheria kwa kufuta maneno "hukumu" na badala yake kuweka maneno "amri" ili kuwianisha na marekebisho yanayopendekezwa katika kifungu cha 2 cha sheria. Kamati katika uchambuzi wake ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 15 inarekebisha kifungu cha 58 cha Sheria kwa lengo la kuiwezesha Tume kuwa na mamlaka ya kusimamia masharti yanayohusu vigezo visivyowekwa wazi (implied conditions) katika mikataba ya walaji na wajibu wa wazalishaji wa bidhaa kadri yalivyoelezwa katika sehemu ya Sita na Saba ya Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Ibara inarekebisha kifungu cha 58(5) ili kuiwezesha Tume kuwa na mamlaka ya kuamuru mali au

hisa zilizopatikana kiasi cha kusababisha kuhodhi soko kurudishwa kwa muuzaji au kufuta ununuzi wa hisa au mali hizo katika muda wowote, tofauti na sasa ambapo Tume ina ukomo wa muda wa miaka mitatu.

**Mheshimiwa Spika**, Licha ya kutambua lengo la marekebisho haya kuwa zuri, Kamati ilitathmini kwa mapana mapendekezo haya na kubaini kuwa, kukosekana kwa ukomo kunaweza kusababisha madhara hasi katika ukuaji wa uchumi. Mojawapo ya madhara ni kuweka mazingira magumu ya kufanikisha ukuaji wa biashara, kudhoofisha bidii za kuvutia wawekezaji na ukuaji wa ubia. **Kwa msingi huo, Kamati ilipendekeza ukomo wa Tume kuwa na mamlaka hayo uwe miaka kumi. Katika mashauriano, Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati ambayo yatazingatiwa kwenye jedwali la marekebisho**.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 16 na 17 inarekebisha kifungu cha 59 na 60 mtawalia kwa lengo la kuiwezesha Tume ya Ushindani kuwa na mamlaka ya kupokea maombi ya kulipwa fidia kutoka kwa watu walioathirika na ukiukwaji wa masharti yaliyopo katika sehemu ya Sita na Saba ya sheria pamoja na kutoza faini kwa watu wanaotenda makosa yaliyoainishwa katika sehemu hiyo. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa marekebisho haya yanakusudia kuwalinda walaji na hivyo kukubaliana na mapendekezo ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 18 na 21 zinapendekeza kurekebisha kifungu cha 61 na 84 mtawalia kwa lengo la kutoa haki ya kukata rufaa ndani ya siku thelathini kwenda Mahakama Kuu chini ya jopo la Majaji watatu kwa mtu ambaye hataridhika na uamuzi wa Baraza la Ushindani. Tathmini ya Kamati ilionesha kuwa mapendekezo haya yanalenga kutekeleza misingi ya utawala bora kwa kuwa Mahakama ndio chombo chenye kauli ya mwisho katika utoaji wa haki nchini kwa mujibu wa Ibara ya 107A ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa mapendekezo ya kifungu hiki yameainisha muda pekee wa kukata rufaa kuwa siku thelathini, na kutokuainisha taratibu nyingine. Kutokuweka namna na taratibu za rufaa zitakavyokuwa, kunaweza kusababisha wadau kushindwa kuitumia haki ya kukata rufaa. Kwa msingi huo, **Kamati ilishauri kuwa kifungu husika kiweke sharti la Waziri mwenye dhamana kutunga kanuni zitakazoweka taratibu za kukata rufaa. Katika mashauriano na Serikali, Kamati iliielezwa kuwa katika kutekeleza ushauri huu, Waziri atatunga kanuni husika kwa kutumia kifungu kinachompa Waziri mamlaka ya jumla ya kutunga kanuni mbalimbali**.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 20 inarekebisha kifungu cha 83 cha Sheria kwa lengo la kumuwezesha Mwenyekiti na Wajumbe wawili wa Baraza la Ushindani kukaa madarakani kwa kipindi cha miaka minne na Wajumbe wengine watatu kukaa madarakani kwa muda wa miaka mitatu. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, kupishana kwa muda huo na kuwepo kwa wajumbe wenye uzoefu kutawezesha Baraza la ushindani kufanya kazi muda wote na kubadilishana uzoefu na hivyo kuongeza ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 22 inarekebisha kifungu cha 87(1)(c) kwa kuingiza maneno "the Tanzania Shipping Agencies Corporation" katikati ya maneno "Aviation Authority" na "and such other" yaliyopo kwenye aya (c). **Kamati katika uchambuzi wake ilibaini kuwa mabadiliko yanayopendekezwa yapo katika kifungu cha 87(1)(d) na si kifungu cha 87(1)(c) kama ilivyoelezwa kwenye Muswada.**

Vilevile Kamati ilibaini kuwa neno **"such"** lililopo katika Muswada liangaliwe upya kwani maneno yaliyopo kwenye Kifungu cha **86(1)(d) cha Sheria ni "and other"** na siyo **"and such other"** kama ilivyoandikwa katika Muswada**.** Serikali iliukubali ushauri wa Kamati kwa kufanya marekebisho ya Ibara hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 23 inarekebisha kifungu cha 91 cha Sheria ili kuondoa masharti ya moja kwa moja ya kisheria ya kusitisha utekelezaji wa amri za Tume pale kunapokuwa na rufaa dhidi ya amri za Tume kwenye Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 24 inarekebisha kifungu cha 96 cha sheria kwa lengo la kuijumuisha sheria ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) kuwa miongoni mwa Sheria ambazo zinaruhusiwa kukinzana na Sheria ya Ushindani. Uchambuzi wa Kamati ulikubaliana na mapendekezo ya Serikali.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI

### 3.1 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na uchambuzi wa maudhui na masharti mbalimbali katika Muswada huu, Kamati inayo maoni na ushauri kama ifuatavyo: -

(a) Mara baada ya mapendekezo ya Muswada huu kuridhiwa na Bunge hili, Sheria ya Ushindani Sura ya 285 ifanyiwe urekebu ili kujumuisha marekebisho haya katika urekebu huo. Kufanya hivyo, kutarahisisha usomaji, kueleweka na kupatikana kwa sheria hiyo katika uhalisia wake na hivyo kuchochea utekelezaji wake;

(b) Kwa kuwa wauzaji wa bidhaa na huduma watalazimika kuanza kuonyesha bei ya bidhaa na huduma, Serikali itoe elimu juu jambo hili kupitia vyombo vya Habari, mitandao ya kijamii, vikao vya wadau ikiwemo vyama vya walaji na wafanyabiashara ili jambo hilo liweze kueleweka kwa jamii ya wauzaji na wanunuzi na hivyo kurahisisha utekelezaji wake;

(c) Waziri mwenye dhamana na masuala ya ushindani atunge kanuni ndani ya muda wa miezi sita baada ya kuanza kutumika kwa marekebisho ya sheria hii ili kuwezesha utekelezaji wa masharti ya sheria yanayohitaji kanuni. Masharti hayo ni pamoja na taratibu za kukata rufaa kutoka Baraza la Ushindani kwenda Mahakama Kuu na taratibu kuhusu nafuu za adhabu kwa mtu

atakayefichua uwepo wa vitendo vya mikataba au mipango inayodhoofisha ushindani wa haki; na

(d) Uwezo wa Tume ya Ushindani uzingatiwe ikiwemo kuongezewa watumishi na kuongeza Ofisi za Kanda na maeneo mengine nchini kulingana na mahitaji ili iweze kutekeleza majukumu yanayopendekezwa katika marekebisho yaliyowasilishwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Maoni haya, yanatokana na matokeo ya Uchambuzi uliofanyika. Aidha, yamezingatia muafaka uliofikiwa kati ya Serikali na Kamati baada ya uchambuzi na mashauriano. Kwa ujumla, matokeo ya uchambuzi, makubaliano ya Kamati na Serikali na maoni ya Kamati, vitawezesha kuboresha Sheria itakayopitishwa na Bunge lako Tukufu.

**SEHEMU YA NNE**

**4.0 HITIMISHO**

**4.1 Shukrani**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine tena nakushukuru kwa uamuzi wako wa kuuleta Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Haki katika Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. Uzoefu wa Wajumbe katika Sekta ya Biashara umekuwa na mchango wa kutosha wakati wa uchambuzi. Aidha, utayari wa Wajumbe kupokea na kusikiliza maoni ya Wadau umesaidia kupata mawazo yenye tija katika uzingatiaji wa maslahi ya Umma wakati wa kujadili Muswada huu. Kwa hatua hii nawashukuru tena Wadau mbalimbali waliotoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kwa ushirikiano mkubwa waliokuwa nao wakati wa uchambuzi wa Muswada. Weledi walionao na umahiri waliouonesha wakati wa uchambuzi, umesaidia kufanikisha kukamilisha Taarifa hii. Ninaamini kwa taarifa hii, Bunge

litakuwa katika nafasi nzuri ya kuamua kwa kuzingatia maslahi ya Umma. Aidha, kwa kutambua mchango wa Wajumbe, naomba majina yao kama yalivyoainishwa yaingizwe katika Taarifa za Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb | M/Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Job Yustino Ndugai, Mb, | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Prof. Sospeter M. Muhongo, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Tauhida Cassian Galos, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Dkt. Medard M. Kalemani, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Daud Silanga Njalu, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Francis Isack Mtinga, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Lucy John Sabu, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Prof. Patrick Alois Ndakidemi, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Janejelly James Ntate, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Yustina Arcadius Rahhi Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Toufiq Salim Turky, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Atupele Fredy Mwakibete, Mb | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mb | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Mohamed Said Issa, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia kumshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara - Mhe. Seleman Said Jafo, Mb, Naibu Waziri - Mhe. Exhaud S. Kigahe, Mb na Wataalamu wote kutoka Serikalini, kwa ufafanuzi walioutoa wakati wa uchambuzi wa Muswada. Maelezo ambayo yamesaidia kufanikisha kazi ya uchambuzi wa Muswada huu kwa wakati.

Namshukuru pia Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi, ndc, kwa kuwezesha na kuongoza kikamilifu shughuli za Sekretarieti katika kuratibu uchambuzi wa Muswada huu.

## 4.2 Wasilisho

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb,
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**
**3 SEPTEMBA, 2024**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.2 wa Mwaka 2024 *(The Written Laws [Miscellaneous Amendment No.2] Bill, 2024)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali; jiandae Mwenyekiti.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kwa mara nyingine tena kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.2 wa Mwaka 2024 *(The Written Laws [Miscellaneous Amendments No.2] Bill, 2024)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu kwa mara nyingine tena kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri kwa nchi yetu. Ninaomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na

wananchi wenzangu kuendelea kumwomba Mwenyezi Mungu amjaalie Rais wetu kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza Mheshimwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati pamoja na Mawaziri wote kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa uzalendo na uaminifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya marekebisho ya Sheria mbalimbali kama yanavyoonekana kwenye Muswada huu ni ushahidi tosha wa mwendelezo wa jitihada za Mheshimiwa Rais na Viongozi wengine Wakuu wa Nchi katika kuendelea kuboresha Sheria za Nchi ili kuongeza ufanisi wa Serikali katika kutekeleza shughuli zake kwa maslahi mapana ya nchi na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huu, ninawashukuru Mawaziri wote kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, ninapenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Spika na kukushukuru wewe Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge pamoja na Wabunge wote, kwa jinsi mnavyotekeleza majukumu yenu na kuliwezesha Bunge kuisimamia Serikali hususan katika eneo la utungaji wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi *(ndc)* na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipotambua na kushukuru kwa dhati kazi kubwa iliyofanywa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini

ya uongozi wa Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba; na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge. Ushahidi wa kazi hiyo unajidhihirisha kwenye Jedwali la Marekebisho la Serikali ambalo kwa kiasi kikubwa ni matokeo ya ushauri wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.2 wa Mwaka 2024 kama ulivyowasilishwa, unapendekeza marekebisho katika Sheria Kuu Nane zifuatazo:

(1) Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432 *(The Anti-Trafficking in Persons Act, Cap. 432)*;

(2) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20 *(The Criminal Procedure Act, Cap. 20)*;

(3) Sheria ya Serikali Mtandao, Sura ya 273 *(The e-Government Act, Cap. 273)*;

(4) Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54 *(The Immigration Act, Cap. 54)*;

(5) Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 *(The Land Act, Cap. 1 13)*;

(6) Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70 *(The Medical Stores Department Act, Cap. 70)*;

(7) Sheria ya Viwango, Sura ya 130 *(The Standards Act, Cap. 30;)* na

(8) Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 127 *(The Planning Commission Act, Cap. 127)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tisa. Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha Jina la Sheria inayopendekezwa

kutungwa na namna ambavyo sheria mbalimbali zimerekebishwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432. Sheria hii ilitungwa mwaka 2008 na mpaka sasa Sheria hiyo imeshafanyiwa marekebisho mara tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kutatua changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa vifungu mbalimbali vya Sheria hii na kuboresha vifungu hivyo ili kuimarisha nyanja zote za kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya msamiati '*Secretariat*'. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa matumizi ya msamiati huo kama ulivyotumika katika sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 17 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuhamisha jukumu la kutoa ushauri nasaha kutoka kwa Kamishna wa Ustawi wa Jamii na badala yake jukumu hilo litekelezwe na Afisa Ustawi wa Jamii. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kwamba waathirika wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu wanapokea huduma za ushauri nasaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 24A kinapendekezwa kuongezwa ili kuanzisha *Secretariat* na kubainisha majukumu yake kulingana na muundo wa kiutendaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Lengo la marekebisho haya ni kubainisha na kufafanua majukumu ya *Secretariat* ili kuwezesha utekelezaji bora wa majukumu hayo pamoja na kuongeza majukumu ya Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu ili kuondoa muingiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa kuzingatia maoni ya Kamati, kifungu hiki kimeboreshwa kupitia Jedwali la Marekebisho ya Serikali ili kuiongezea *Secretariat* jukumu la kuishauri Kamati ya

Kitaifa ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu utekelezaji wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya 24B, 24C na 24D ambavyo vinaweka masharti ya uteuzi wa Katibu na Naibu Makatibu pamoja na ajira kwa watumishi wapya wa *Secretariat*. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza uwezo wa *Secretariat* kwa kuhakikisha kuwa ina nguvu kazi ya kutosha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 30 kilikuwa kinapendekezwa kurekebishwa ili kuipa Kamati mamlaka ya kuteua *Secretariat* ambayo itaisaidia katika utekelezaji wa majukumu yake kutoka miongoni mwa watumishi wa Wizara baada ya kushauriana na Waziri. Hata hivyo, baada ya mashauriano na Kamati, kifungu hicho kinarekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho ili *Secretariat* iweze kuratibu shughuli zote na vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumuondoa Mkurugenzi wa Uhamiaji na badala yake kumuweka Kamisha Jenerali wa Uhamiaji. Lengo la marekebisho haya ni kuleta mfanano katika matumizi ya maneno kama yanavyotumika katika Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 32 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta baadhi ya majukumu ya uendeshaji ya Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu kwa kuwa majukumu hayo sasa yanapendekezwa kutekelezwa na *Secretariat*. Lengo la marekebisho haya ni kutofautisha majukumu ya *Secretariat* na majukumu ya Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekezwa kufanya marekebisho katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20. Sheria hii ilitungwa mwaka 1985 na mpaka sasa imeshafanyiwa marekebisho mara

35. Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuleta ufanisi katika uandaaji wa ripoti ya Uchunguzi wa Kiforensiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 205A kinapendekezwa kurekebishwa na Jedwali la Tano linapendekezwa kuongezwa kwa kuainisha namna na muundo wa kuandaa ripoti ya Uchunguzi wa Kiforensiki kwa njia ya mtandao. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha mfumo wa uandaaji wa ripoti ya Uchunguzi wa Kiforensiki pamoja na kuongeza thamani ya ushahidi wa ripoti hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Serikali Mtandao, Sura ya 273. Sheria hii ilitungwa mwaka 2019 na mpaka sasa haijafanyiwa marekebisho. Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuweka uwiano wa adhabu na kosa lililotendeka na kuzuia watu kutenda au kujaribu kutenda kosa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 57 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza adhabu kwa kosa la kuondoa, kuharibu au kubadili *data*, kumbukumbu za kielektroniki na mfumo au vifaa vya kielektroniki. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha adhabu zinazowekwa kwenye Sheria zinawekwa kwa kuzingatia uzito wa makosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54. Sheria hii ilitungwa mwaka 1995 na hadi sasa imefanyiwa marekebisho mara 12. Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuondoa upungufu uliojitokeza wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Sheria hii inapendekezwa kurekebishwa kwa ajili ya kuweka masharti yanayohusu hadhi maalum kwa raia wa nchi nyingine mwenye asili ya Tanzania. Hata hivyo, kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho ya Serikali, baada ya mashauriano na Kamati, Serikali inapendekeza kuondoa marekebisho hayo yanayohusu hadhi

maalum kwa raia wa nchi nyingine ili yaendelee kufanyiwa kazi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya msamiati *'Medical practitioner'* kwa lengo la kuwajumuisha watu wanaotambuliwa kuwa ni madaktari chini ya Sheria ya Madaktari na Madaktari wa Meno ya Tanzania Zanzibar. Kwa sasa, Sheria ya Uhamiaji inaelekeza kwamba tafsiri ya msamiati *'Medical practitioner'* itakuwa kama ilivyotolewa chini ya Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Wataalamu wa Afya Shirikishi, Sura ya 152.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kifungu hiki kimerekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya misamiati *'Board'*, *'Illegal Immigrant'*, *'Order of Departure'* na *'Smuggling of Immigrants'*. Lengo la marekebisho haya ni kuyafanya masharti yaliyoainishwa katika sheria na yale yanayopendekezwa kuongezwa yaeleweke kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 8B na Jedwali ili kuanzisha Bodi ya Usimamizi wa Chuo cha Uhamiaji cha Kikanda *(TRITA)*. Lengo la marekebisho haya ni kuitambua kisheria Bodi iliyopo na kukidhi matakwa ya uwepo wa Bodi ya Ushauri kwa vyuo vinavyosajiliwa chini ya Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura ya 129. Aidha, marekebisho hayo yanalenga kuweka bayana muda wa wajumbe wa Bodi ya Usimamizi kuhudumu, utenguzi wa wajumbe, mwenendo wa Bodi na masuala mengine yanayohusiana na Bodi ya Usimamizi wa Chuo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 11 kinapendekezwa kufutwa. Kwa sasa kifungu cha 11 kinaainisha mamlaka ya nidhamu kwa Maafisa Uhamiaji kuanzia ngazi ya chini hadi ngazi za juu. Lengo la marekebisho ni kuepusha mgongano kati ya Sheria ya Uhamiaji na Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Idara ya Uhamiaji

Tanzania, Sura ya 241 ambayo ni Sheria mahususi inayosimamia masuala ya nidhamu ya Maafisa Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu hii pia inapendekeza marekebisho katika vifungu vya 20, 23, 28 na 32. Kifungu cha 20 kinaweka masharti kuhusu utaratibu wa kuchukua maelezo ya mtu anayeshukiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mashauriano na Kamati, marekebisho katika kifungu cha 20(2) yameboreshwa kupitia jedwali la marekebisho ili kuruhusu njia mojawapo ya zilizotajwa katika kifungu hicho kutumika tofauti na ilivyokuwa awali ambapo kifungu hicho kilikuwa kinaweka takwa la lazima la kurekodi maelezo ya mshukiwa kwa *video*, picha na teknolojia ya kunasa sauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 23 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (2), ambacho kinamwezesha Kamishna Jenerali kutoa *notice* kwa mhamiaji aliyezuiwa kuingia nchini na mamlaka nyingine zozote zinazohusika. Kwa sasa Kifungu cha 23 kinafafanua maana ya neno *prohibited immigrant* lakini hakifafanui ni wakati gani mtu anahesabika kuwa ni mhamiaji aliyezuiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha marekebisho ya Kifungu cha 23 yanakusudia kuongeza kifungu kidogo cha (3) ambacho kinamwezesha Kamishna Jenerali kutoa amri ya kuondoka nchini kwa mhamiaji aliyezuiwa kuingia nchini hususani katika mazingira ambapo, mhusika ametenda makosa katika nchi yake ya asili. Kwa ujumla lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha utambuzi wa wahamiaji waliozuiwa kuingia nchini na kuimarisha ushirikiano wa jumuiya za kikanda na ushirikiano wa kidiplomasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 32 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta na kuandika upya kifungu kidogo cha pili kwa lengo la kuainisha muda wa ukomo wa juu wa kutumika kwa kibali cha makazi kuwa ni miaka miwili na kibali hicho kinaweza kuuhishwa kwa kipindi kirefu zaidi ya miaka miwili. Kwa sasa Kifungu cha 32 kimeainisha kwamba, muda wa ukomo wa

juu wa kibali cha ukaazi kuwa ni miaka mitatu na muda wa ukomo wa juu kuhusiana na uhuishaji wa kibali hicho kuwa ni miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hicho pia kinaainisha kwamba, muda wa jumla wa uhalali wa kibali cha ukaazi cha msingi na muda wa uhuishaji wake hautazidi miaka mitano. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa ukomo wa miaka mitano kwa kibali cha ukaazi cha msingi na uhuishaji wake kwa ajili ya kuwezesha wageni kukaa na kufanya shughuli zao ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa muda mrefu kulingana na shughuli wanazozifanya ikiwa ni pamoja na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 37 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza wigo wa masuala ambayo mtu anaweza kuyakatia rufaa kwa Waziri. Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kuwa mtu ambaye hajaridhishwa na uamuzi wowote wa Kamishina Jenerali anapata haki ya kukata rufaa kwa Waziri dhidi ya uamuzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 42A kinaongezwa ili kuweka utaratibu wa kuwasilisha maombi mbalimbali chini ya Sheria ya Uhamiaji. Lengo la marekebisho haya ni kutambua maombi yanayofanyika kwa njia ya kielektroniki au njia nyingine ambazo Kamishina Jenerali anaweza kuruhusu ili kuongeza ufanisi wa huduma za uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 46 kinapendekezwa kurekebishwa kwa madhumuni ya kubainisha ukomo wa chini na wa juu wa adhabu. Lengo la marekebisho haya ni kuruhusu Mahakama kutoa adhabu kwa kuzingatia ukomo wa juu na chini wa adhabu kulingana na mazingira ya utendaji wa kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 48 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza maneno ambayo Waziri anaweza kuyatengenezea kanuni ili kujumuisha utaratibu wa rufaa kwa Mheshimiwa Waziri. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ardhi, Sura ya 113. Sheria hii ilitungwa mwaka 1999 na hadi sasa imefanyiwa marekebisho mara 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 19 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kuweka utaratibu wa matumizi ya ardhi kwa mtu aliyepewa hadhi maalum chini ya Sheria ya Uhamiaji. Hata hivyo, baada ya mashauriano ya kina baina ya Serikali na Kamati, Serikali kupitia jedwali la marekebisho hayo inapendekeza kuyaondoa marekebisho ili yaendelee kufanyiwa kazi kwa kina zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70. Sheria hii ilitungwa mwaka 1993 na hadi sasa imerekebishwa mara mbili. Muswada unapendekeza kurekebisha kifungu cha 16A ili kuondoa masharti ya lazima kwa Bohari ya Dawa *(MSD)* kuwekeza katika uwekezaji unaoruhusiwa katika Sheria ya Uwekezaji wa Wadhamini, Sura ya 53 pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa uwekezaji wa *MSD* na kuiwezesha kujiendesha kibiashara kama taasisi ya kimkakati kwa kuzingatia maelekezo yatakayokuwa yanatolewa na Msajili wa Hazina na mamlaka nyingine zozote zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Viwango, Sura ya 130. Sheria hii ilitungwa mwaka 2009 na hadi sasa imefanyiwa marekebisho mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta na kuboresha baadhi ya tafsiri ya misamiati kwenye sheria na kuongeza misamiati mipya. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa misamiati mbalimbali iliyotumika kwenye sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kupanua wigo wa majukumu ya shirika katika masuala ya udhibiti ubora na usalama wa bidhaa, mifumo ya usimamizi wa viwango vya metorolojia na usalama wa bidhaa. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha udhibiti wa viwango vya bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kifungu cha 21A kinapendekezwa kurekebishwa ili kutambua taratibu za kimataifa za uzalishaji wa bidhaa zinazotumika na mashirika ya kimataifa kama vile Shirika la Viwango vya Kimataifa *(ISO)*, Shirika la Afya Duniani *(WHO)*, Shirika la Chakula na Kilimo Duniani *(FAO)* na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani *(WFP)*. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha taratibu za uzalishaji zinazotumika na shirika na taratibu zinazotambulika kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 22 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuliwezesha shirika kuomba sampuli, vifaa na taarifa kutoka kwa mteja mwenye leseni badala ya taarifa hizo kuombwa na bodi ambayo haihusiki na utendaji kazi wa kila siku wa shirika. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 23 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha wakaguzi wa shirika kupewa vitambulisho badala ya vyeti vya uteuzi. Lengo la marekebisho haya ni kuweka utaratibu unaorahisisha utambulisho wa wakaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 24 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa mkaguzi wa shirika mamlaka ya kukamata bidhaa zisizokidhi viwango vilivyoainishwa. Lengo la marekebisho ni kuimarisha utaratibu wa udhibiti ili kuwezesha uzingatiwaji wa viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 27 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha adhabu ya faini kutolewa kwa kuzingatia thamani ya bidhaa isiyokidhi viwango au ambayo

haijasajiliwa. Lengo la marekebisho haya ni kutoa adhabu kwa kuzingatia uzito wa kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu hii pia ilikuwa inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 31A. Hata hivyo kupitia jedwali la marekebisho kifungu hiki kinapenda kuondolewa kwa kuwa masharti yaliyokuwa yanapendekezwa yanaweza kutekelezwa kupitia kanuni zitakazotengenezwa chini ya Kifungu cha 36(3) kama kinavyopendekezwa kurekebishwa katika Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 36 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa Waziri mamlaka ya kutengeneza kanuni zinazoainisha masharti ya utangazaji wa vyakula na vipodozi na kuweka viwango vya juu vya adhabu zitakazoainishwa katika kanuni. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 127. Sheria hii ilitungwa mwaka 2023 na haya ndiyo marekebisho yake ya kwanza. Sheria hii inapendekezwa kurekebishwa kwa ujumla katika masharti mbalimbali kwa kubadili jina la tume kuwa Tume ya Taifa ya Mipango. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha jina la tume na wigo wa majukumu yake ambayo yanajumuisha kusimamia uchumi wa Taifa, mchakato wa upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza idadi ya wajumbe wa tume wanaoteuliwa na Mheshimiwa Rais, kutoka wajumbe sita hadi wajumbe nane. Lengo la marekebisho haya ni kutoa wigo mpana kwa Mheshimiwa Rais, kuteua watu wenye ujuzi na uzooefu katika masuala ya uchumi na mipango ya maendeleo ya Taifa. Aidha, kifungu hicho kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza wajumbe wapya kwenye tume ambao watahudhuria vikao kwa nyadhifa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wajumbe hao ni Katibu Mkuu Kiongozi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu mwenye dhamana ya masuala ya mipango na maendeleo ya Taifa na Katibu Mkuu mwenye dhamana ya masuala ya fedha. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha ubora na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kutoa hoja kwamba, Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.2) Bill, 2024)* ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA MHESHIMIWA HAMZA SAIDI JOHARI (MB.), MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (NA 2) WA MWAKA 2024 (THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO. 2) BILL, 2024) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kwa mara nyingine tena kusimama mbele yaBunge lako tukufu kuwasilisha Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2024 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2024).

Mheshimiwa Spika, niruhusu kwa mara nyingine tena kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri kwa Nchi yetu. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wenzangu kuendelea kumwomba Mwenyezi Mungu amjaalie Rais wetu kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt.

Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe, Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nisharti pamoja na Mawaziri wote kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa uzalendo na uaminifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya marekebisho ya Sheria mbalimbali kama yanavyoonekana kwenye Muswada huu ni ushahidi tosha wa mwendelezo wa jitihada za Mheshimiwa Rais na Viongozi wengine Wakuu wa nchi katika kuendelea kuboresha Sheria za Nchi ili kuongeza ufanisi wa Serikali katika kutekeleza shughuli zake kwa maslahi mapana ya nchi na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huu, ninawashukuru Mawaziri wote kwa ushirikiano wanaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge pamoja na Wabunge wote kwa jinsi mnavyotekeleza majukumu yenu na kuliwezesha Bunge kuisimamia Serikali hususan katika eneo la utungaji wa Sheria. Ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Joyce Mwihambi, (ndc,) na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaoipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipotambua na kushukuru kwa dhati kazi kubwa iliyofanywa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya uongozi wa Mwenyekiti wa Kamati Dkt. Joseph Kizito

Mhagama (Mbunge wa Madaba) na Makamu Mwenyekiti Mhe.

Florent Laurent Kyombo (Mbunge wa Nkenge). Ushahidi wa kazi hiyo unajidhihirisha kwenye Jedwali la Marekebisho la Serikali ambalo kwa kiasi kikubwa ni matokeo ya ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2024 kama ulivyowasilishwa unapendekeza marekebisho katika Sheria Kuu Nane (8) zifuatazo.

(a) Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432 (The Anti-Trafficking in Persons Act, Cap. 432);

(b) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20 (The Criminal Procedure Act, Cap. 20);

(c) Sheria ya Serikali Mtandao, Sura ya 273 (The e-Government Act, cap. 273);

(d) Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54 (The Immigration Act, Cap. 54);

(e) Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 (The Land Act, Cap. 1 13);

(f) Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70 (The Medical Stores Department Act, Cap. 70);

(g) Sheria ya Viwango, Sura ya 130 (The Standards Act, Cap. 30); na

(h) Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 127 (The Planning Commission Act, Cap. 127).

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tisa. Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha Jina la sheria inayopendekezwa kutungwa na namna ambavyo Sheria mbalimbali zimerekebishwa katika Muswada.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu,

Sura ya 432. Sheria hii ilitungwa mwaka 2008 na mpaka sasa Sheria hiyo imeshafanyiwa marekebisho mara tano (5). Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kutatua changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa vifungu mbalimbali vya sheria hii na kuboresha vifungu hivyo ili kuimarisha nyanja zote za kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya msamiati "Sekretarieti". Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa matumizi ya msamiati huo kama ulivyotumika katika Sheria. Kifungu cha 17 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuhamisha jukumu la kutoa ushauri nasaha kutoka kwa Kamishna wa Ustawi wa Jamii na badala yake jukumu hilo litekelezwe na afisa ustawi wa jamii. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kwamba waathirika wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu wanapokea huduma za ushauri nasaha.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 24A kinapendekezwa kuongezwa ili kuanzisha Sekretarieti na kubainisha majukumu yake kulingana na muundo wa kiutendaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Lengo la marekebisho haya ni kubainisha na kufafanua majukumu ya Sekretarieti ili kuwezesha utekelezaji bora wa majukumu hayo pamoja na kuboresha majukumu ya Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu ili kuondoa muingiliano. Aidha, kwa kuzingatia maoni ya Kamati, kifungu hiki kimeboreshwa kupitia Jedwali la Marekebisho ya Serikali ili kuiongezea Sekretarieti jukumu la kuishauri Kamati ya Kitaifa ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu utekelezaji wa Sheria.

Vilevile, Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya 24B, 24C na 24D, ambavyo vinaweka masharti ya uteuzi wa Katibu na Manaibu Katibu pamoja na ajira kwa watumishi wapya wa Sekretarieti. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza uwezo wa Sekretarieti kwa kuhakikisha kuwa ina nguvu kazi ya kutosha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kifungu cha 30 kilikuwa kinapendekezwa kurekebishwa ili kuipa Kamati mamlaka ya kuteua sekretarieti

ambayo itaisaidia katika utekelezaji wa majukumu yake kutoka miongoni mwa watumishi wa Wizara baada ya kushauriana na Waziri. Hata hivyo, baada ya mashauriano na Kamati, kifungu hicho kinarekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho ili Sekretarieti iweze kuratibu shughuli zote na vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumuondoa Mkurugenzi wa Uhamiaji na badala yake kumuweka Kamisha Jenerali wa Uhamiaji. Lengo la marekebisho haya ni kuleta mfanano katika matumizi ya maneno kama yanavyotumika katika Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54. Kifungu cha 32 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta baadhi ya majukumu ya uendeshaji ya Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu kwa kuwa majukumu hayo sasa yanapendekezwa kutekelezwa na Sekretarieti. Lengo la marekebisho haya ni kutofautisha majukumu ya Sekretarieti na majukumu ya Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20. Sheria hii ilitungwa mwaka 1985, na mpaka sasa imeshafanyiwa marekebisho mara thelathini na tano (35). Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuleta ufanisi katika uandaaji wa ripoti ya uchunguzi wa kiforensiki.

Kifungu cha 205A kinapendekezwa kurekebishwa na Jedwali la Tano linapendekezwa kuongezwa kwa kuainisha namna na muundo wa kuandaa ripoti ya uchunguzi wa kiforensiki kwa njia ya mtandao. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha mfumo wa uandaaji wa ripoti ya uchunguzi wa kiforensiki pamoja na kuongeza thamani ya ushahidi wa ripoti hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Serikali Mtandao, Sura ya 273. Sheria hii ilitungwa mwaka 2019 na mpaka sasa haijafanyiwa marekebisho.

Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuweka uwiano wa adhabu na kosa lililotendeka na kuzuia watu kutenda

au kujaribu kutenda kosa husika. Kifungu cha 57 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza adhabu kwa kosa la kuondoa, kuharibu au kubadili data, kumbukumbu za kielektroniki, mifumo au vifaa vya kielektroniki. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha adhabu zinazowekwa kwenye Sheria zinawekwa kwa kuzingatia uzito wa makosa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54. Sheria hii ilitungwa mwaka 1995 na hadi sasa imefanyiwa marekebisho mara kumi na mbili

(12). Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuondoa mapungufu yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji. Vilevile Sheria hii inapendekezwa kurekebishwa kwa ajili ya kuweka masharti yanayohusu hadhi maalum kwa raia wa nchi nyingine mwenye asili ya Tanzania. Hata hivyo, kama inavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho ya Serikali, baada ya mashauriano na Kamati, Serikali inapendekeza kuondoa marekebisho hayo yanayohusu hadhi maalumu kwa raia wa nchi nyingine ili yaendelee kufanyiwa kazi zaidi.

Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya msamiati "medical practitioner" kwa lengo la kuwajumuisha watu wanaotambuliwa kuwa ni madaktari chini ya Sheria ya Madaktari na Madaktari wa Meno ya Tanzania Zanzibar. Kwa sasa, Sheria ya Uhamiaji inaelekeza kwamba tafsiri ya msamiati "medical practitioner" itakuwa kama ilivyotolewa chini ya Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Wataalamu wa Afya Shirikishi, Sura ya 152. Vilevile, kifungu kimerekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya misamiati ""Board", "illegal immigrant", "order of departure" na "smuggling of immigrants". Lengo la marekebisho haya ni kuyafanya masharti yaliyoainishwa katika Sheria na yale yanayopendekezwa kuongezwa yaeleweke kwa urahisi zaidi.

Aidha, Sheria inapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 8B na Jedwali ili kuanzisha Bodi ya Usimamizi wa Chuo cha Uhamiaji cha Kikanda (TRITA). Lengo la marekebisho

haya ni kuitambua kisheria Bodi iliyopo na kukidhi matakwa ya uwepo wa Bodi ya Ushauri kwa vyuo vinavyosajiliwa chini ya Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura ya 129. Aidha, marekebisho hayo yanalenga kuweka bayana muda wa wajumbe wa Bodi ya Usimamizi kuhudumu, utenguzi wa wajumbe, mwenendo wa Bodi na masuala mengine yanayohusiana na Bodi ya Usimamizi wa Chuo hicho.

Kifungu cha 1 1 kinapendekezwa kufutwa. Kwa sasa, kifungu cha 1 1 kinaainisha mamlaka ya nidhamu kwa Maafisa Uhamiaji kuanzia ngazi ya chini hadi ngazi ya juu. Lengo la marekebisho ni kuepusha mgongano kati ya Sheria ya Uhamiaji na Sheria ya Tume ya Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Idara ya Uhamiaji Tanzania, Sura ya 241 ambayo ni Sheria mahsusi inayosimamia masuala ya nidhamu ya maafisa uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, Sehemu hii pia inapendekeza marekebisho katika vifungu vya 20, 23, 28 na 32. Kifungu cha 20 kinaweka masharti kuhusu utaratibu wa kuchukua maelezo ya mtu anayeshukiwa. Baada ya mashauriano na Kamati, marekebisho katika kifungu cha 20(2) yameboreshwa kupitia Jedwali la Marekebisho ili kuruhusu njia mojawapo ya zilizotajwa katika kifungu hicho kutumika tofauti na ilivyo awali ambapo kifungu hicho kilikuwa kinaweka takwa la lazima la kurekodi maelezo ya mshukiwa kwa Video, picha na teknolojia ya kunasa sauti.

Kifungu cha 23 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (2) ambacho kinamwezesha Kamishna Jenerali kutoa notisi kwa mhamiaji aliyezuiwa kuingia nchini na mamlaka nyingine zozote zinazohusika. Kwa sasa, kifungu cha 23 kinafafanua maana ya neno "prohibited immigrantj' lakini hakifafanui ni wakati gani mtu anahesabika kuwa ni mhamiaji aliyezuiwa. Aidha, marekebisho ya kifungu cha 23 yanakusudia kuongeza kifungu kidogo kipya cha (3) ambacho kinamwezesha Kamishna Jenerali kutoa amri ya kuondoka nchini kwa mhamiaji aliyezuiwa kuingia nchini hususan katika mazingira ambapo mhusika ametenda makosa katika nchi yake ya asili.

Kwa ujumla, lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha utambuzi wa wahamiaji waliozuiliwa kuingia nchini na kuimarisha ushirikiano wa jumuiya za kikanda na ushirikiano wa kidiplomasia.

Kifungu cha 32 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufuta na kuandika upya kifungu kidogo cha (2) kwa lengo la kuainisha muda wa ukomo wa juu wa kutumika kwa kibali cha makazi kuwa miaka miwili na kibali hicho kinaweza kuhuishwa kwa kipindi kirefu zaidi ya miaka miwili. Kwa sasa, kifungu cha 32 kimeainisha kwamba muda wa ukomo wa juu wa kibali cha ukaazi kuwa ni miaka mitatu na muda wa ukomo wa juu kuhusiana na uhuishaji wa kibali hicho kuwa ni miaka miwili. Kifungu hicho pia kinaainisha kwamba muda wa jumla wa uhalali wa kibali cha ukaazi cha msingi na muda wa uhuishaji wake hautazidi miaka mitano. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa ukomo wa miaka mitano wa kibali cha ukaazi cha msingi na uhuishaji wake kwa ajili ya kuwezesha wageni kukaa na kufanya shughuli zao ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa muda mrefu kulingana na shughuli wanazofanya, ikiwa ni pamoja na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 37 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza wigo wa masuala ambayo mtu anaweza kuyakatia rufaa kwa Waziri. Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kuwa mtu ambaye hajaridhishwa na uamuzi wowote wa Kamishna Jenerali anapata haki ya kukata rufaa kwa Waziri dhidi ya uamuzi huo. Kifungu kipya cha 42A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka utaratibu wa kuwasilisha maombi mbalimbali Chini ya Sheria ya Uhamiaji. Lengo la marekebisho haya ni kutambua maombi yanayofanyika kwa njia ya kielektroniki au njia nyingine ambazo Kamishna Jenerali anaweza kuruhusu ili kuongeza ufanisi wa huduma za uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 46 kinapendekezwa kurekebishwa kwa madhumuni ya kubainisha ukomo wa chini na wa juu wa adhabu. Lengo la marekebisho haya ni kuruhusu Mahakama kutoa adhabu kwa kuzingatia ukomo wa juu na chini wa adhabu kulingana na mazingira ya ütendekaji wa kosa. Kifungu cha 48 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza maeneo ambayo Waziri anaweza kuyatengenezea kanuni ili

kujumuisha utaratibu wa rufaa kwa Waziri. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ardhi, Sura ya 113. Sheria hii ilitungwa mwaka 1999 na hadi sasa imefanyiwa marekebisho mara kumi na nne (14).

Kifungu cha 19 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kuweka utaratibu wa matumizi ya ardhi kwa mtu aliyepewa hadhi maalumu chini ya Sheria ya Uhamiaji. Hata hivyo, baada ya mashauriano ya kina baina ya Serikali na Kamati, Serikali kupitia Jedwali la Marekebisho hayo inapendekeza kuyaondoa marekebisho ili yaendelee kufanyiwa kazi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70. Sheria hii ilitungwa mwaka 1993 na hadi sasa innerekebishwa mara mbili (2).

Muswada unapendekeza kurekebisha kifungu cha 16A ili kuondoa masharti ya lazima kwa Bohari ya Dawa (MSD) kuwekeza katika uwekezaji unaoruhusiwa katika Sheria ya Uwekezaji wa Wadhamini, Sura ya 53 pekee. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa uwekezaji wa MSD na kuiwezesha kujiendesha kibiashara kama taasisi ya kimkakati kwa kuzingatia maelekezo yatakayokuwa yanatolewa na Msajili wa Hazina na mamlaka nyingine zozote zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Viwango, Sura ya 130. Sheria hii ilitungwa mwaka 2009 na hadi sasa imefanyiwa marekebisho mara moja (1).

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 2 kinapendezwa kurekebishwa kwa kufuta na kuboresha baadhi ya tafsiri ya misamiati kwenye Sheria na kuongeza misamiati mipya. Lengo la marekebisho haya ni kutoa ufafanuzi wa misamiati mbalimbali iliyotumika kwenye Sheria. Kifungu cha 4 kinapendekezwa

kurekebishwa kwa kupanua wigo wa majukumu ya Shirika katika masuala ya udhibiti ubora na usalama wa bidhaa, mifumo ya usimamizi wa viwango vya metrolojia na usalama wa bidhaa. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha udhibiti wa viwango vya bidhaa.

Vilevile, kifungu cha 2IA kinapendekezwa kurekebishwa ili kutambua taratibu za kimataifa za uzalishaji wa bidhaa zinazotumika na mashirika ya kimataifa kama vile Shirika la Viwango vya Kimataifa (ISO), Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP). Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha taratibu za uzalishaji zinazotumika na Shirika na taratibu zinazotambulika kimataifa. Kifungu cha 22 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuliwezesha Shirika kuomba sampuli, vifaa na taarifa kutoka kwa mteja mwenye leseni badala ya taarifa hizo kuombwa na Bodi ambayo haihusiki na utendaji kazi wa kila siku wa Shirika. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Shirika.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 23 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha wakaguzi wa Shirika kupewa vitambulisho badala ya vyeti vya uteuzi. Lengo la marekebisho haya ni kuweka utaratibu unaorahisisha utambulisho wa wakaguzi- Kifungu cha 24 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa mkaguzi wa Shirika mamlaka ya kukamata bidhaa zisizokidhi viwango vilivyoainishwa. Lengo la marekebisho ni kuimarisha utaratibu wa udhibiti ili kuwezesha uzingatiwaji wa viwango. Kifungu cha 27 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha adhabu ya faini kutolewa kwa kuzingatia thamani ya bidhaa isiyokidhi viwango au ambayo haijasajiliwa. Lengo la marekebisho haya ni kutoa adhabu kwa kuzingatia uzito wa kosa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu hii pia ilikuwa inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 31A. Hata hivyo kupitia Jedwali la Marekebisho, kifungu hiki kinapendekezwa kuondolewa kwa kuwa masharti yaliyokuwa yanapendekezwa yanaweza kutelekezwa kupitia kanuni zitakazotengenezwa chini ya kifungu cha 36(3) kama kinavyopendekezwa kurekebishwa katika

Muswada. Kifungu cha 36 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa Waziri mamlaka ya kutengeneza kanuni zinazoainisha masharti ya utangazaji wa vyakula na vipodozi na kuweka viwango vya juu vya adhabu zitakazoainishwa katika kanuni. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 127. Sheria hii ilitungwa mwaka 2023 na haya ndio marekebisho yake ya kwanza.

Sheria hii inapendekezwa kurekebishwa kwa ujumla katika masharti mbalimbali kwa kubadili jina la Tume kuwa Tume ya Taifa ya Mipango. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha jina la Tume na wigo wa majukumu yake ambayo yanajumuisha kusimamia uchumi wa Taifa, mchakato wa upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa.

Aidha, Kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza idadi ya wajumbe wa Tume wanaoteuliwa na Rais kutoka wajumbe sita hadi wajumbe nane. Lengo la marekebisho haya ni kutoa wigo mpana kwa Rais kuteua watu wenye ujuzi na uzoefu katika masuala ya uchumi na mipango ya maendeleo ya Taifa. Aidha, kifungu hicho kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza wajumbe wapya kwenye Tume ambao watahudhuria vikao kwa nyadhifa zao. Wajumbe hao ni Katibu Mkuu Kiongozi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu mwenye dhamana ya masuala ya mipango na maendeleo ya Taifa na Katibu Mkuu mwenye dhamana ya masuala ya fedha. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha ubora na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2024 (the Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2024) ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili

na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

Mheshimiwa Spika, NAOMBA KUTOA HOJA.

Hamza S. Johari (Mb.)
**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**
03 Septemba, 2024

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, hoja imeungwa mkono. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati, Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99, Kanuni ndogo ya tano ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.2) Bill 2024)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 93(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza katika Mkutano wa 15, kikao cha 56 kwenye Bunge la Kumi na Mbili, tarehe 28 Juni, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136(14) na kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Mheshimiwa Spika, alielekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu

kwa kuzingatia Katiba, sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza jukumu hilo Kamati ilikutana na Serikali tarehee 14/8/2024 ili kupokea maelezo yaliyokuwa ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Dkt. Elieza Mbuki Feleshi ambaye alikuwa Mbunge, kuhusu maudhui ya Muswada huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya mikutano ya kusikiliza maoni ya wadau *(public hearings)* kwa siku mbili kuanzia tarehe 15 hadi 16 Agosti, 2024 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka wadau mbalimbali ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao. Kipekee nawashukuru wadau wote waliotoa maoni hayo ili kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua hiyo wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa kuzingatia maoni ya wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 22/8/2024 Kamati ilikutana na Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria ambaye alijibu na kutoa ufafanuzi juu ya hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu Muswada huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua hiyo nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.2) Bill 2024)*. Ukiwa umegawanyika katika Sehemu Tisa na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria nane kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza wakati wa utekelezaji wa sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zilizopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni kama ifuatavyo: -

(a) Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432 *(The Anti-Trafficking in Persons Act, (Cap. 432))*;

(b) Marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 *(The Criminal Procedure Act, (Cap. 20))*;

(c) Marekebisho ya Sheria ya Serikali Mtandao, Sura ya 273 *(The e-Government Act, (Cap. 273));*

(d) Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54 *(The Immigration Act, (Cap. 54));*

(e) Marekebisho ya Sheria ya Ardhi, Sura 113 *(The Land Act (Cap. 113))*;

(f) Marekebisho ya Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70 *(The Medical Stores Department Act, (Cap.70))*;

(g) Marekebisho ya Sheria ya Viwango, Sura ya 130 *(The Standards Act, (Cap. 130))*; na

(h) Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 127.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi inayojumuisha ibara ya kwanza inayohusu jina fupi na ibara ya pili inayoeleza marekebisho yanayopendekezwa kufanywa katika sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunafanya uchambuzi wa Muswada huu pamoja na maelezo ya Serikali, Kamati ilibaini changamoto au mapungufu katika sheria tatu kati ya sheria nane zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kama zilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika ibara ya 3 hadi ibara ya 9 ya Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa marekebisho kwenye sheria hii kwa ujumla wake yanalenga kutatua changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa vifungu mbalimbali vya sheria hii na kuboresha vifungu hivyo ili kuimarisha nyanja zote za kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya Sita inapendekeza kurekebisha Sehemu ya Nne ya sheria kwa kuongeza Sehemu ya Nne A inayoboresha muundo wa Sekretarieti ya kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu na kuongeza Kifungu cha 24A ambacho kinafafanua majukumu ya Sekretarieti hiyo; ambayo inafafanua majukumu ya Sekretari hiyo kuwa ni:-

(a) Kuratibu shughuli za taasisi mbalimbali katika masuala yanayohusu usafirishaji haramu wa binadamu.

(b) Kuchukua hatua kwa kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu kwa kutoa elimu kwa umma, kutoa mafunzo, kufanya uchunguzi wa pamoja na kuvunja mtanadao na njia za usafirishaji haramu wa binadamu.

(c) Kutambua, kuokoa, kulinda, kurekebisha na kuwaunganisha waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu.

(d) Kuhakikisha utekelezaji wa mikataba ya kimataifa kuhusu masuala yanayohusu usafirishaji haramu wa binadamau ambayo Jamhuri ya Muungano ni sehemu ya mikataba hiyo.

(e) Kushirikiana na vyombo vingine katika uchunguzi na uendeshaji wa mashtaka ya biashara haramu ya binadamu.

(f) Kukuza ushirikiano na taasisi za kimataifa, kikanda na kitaifa katika kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu.

(g) Kuanzisha, kuwezesha, kukuza na kusimamia uendeshaji wa nyumba salama kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu.

(h) Kufanya utafiti, kusimamia na kufuatilia matukio ya usafirishaji haramu wa binadamu nchini; na

(i) Kutekeleza majukumu mengine kama itakavyohitajika katika kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu hayo, Muswada unapendekeza kuwa Sekretarieti inaweza:-

(a) Kuanzisha mfumo wa ukusanyaji na usimamizi wa *data* kuhusu usafirishaji haramu wa binadamu katika ngazi ya Taifa;

(b) Kuingia katika jengo lolote kwa madhumuni ya kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu; na

(c) Kuomba taarifa yoyote na kumwita mtu yeyote anayejihusisha na usafirishaji haramu wa binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vifungu vya 24B, 24C na 24D vinaweka utaratibu wa uteuzi wa Katibu na Makatibu Wasaidizi wa Sekretarieti pamoja na utaratibu wa kuajiri watumishi wa

Sekretarieti hiyo. Lengo la marekebisho ni kubainisha na kufafanua majukumu ya Sekretarieti ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, kuongeza uwezo wa Sekretarieti kwa kuhakikisha ina wasaidizi na watumishi wa kutosha katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 7 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 30, kwa:-

(a) Kufuta na kuandika upya Kifungu cha 30(2) ili kuipa Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu mamlaka ya kuteua Sekretarieti baada ya kushauriana na Waziri; na

(b) Kufuta Vifungu vidogo vya (3) na (4) vinavyoweka msingi wa namna Sekretarieti itafanya kazi na Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho ni kuendana na mabadiliko yanayopendekezwa katika Kifungu cha 24B, 24C na 24D.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji, Sura 54. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 15 hadi Ibara ya 28 ya Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 16 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 3 kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya msamiati "*medical practitioner*" yaani daktari wa matibabu kwa lengo la kuwajumuisha watu wanaotambuliwa kuwa ni madaktari chini ya Sheria ya Madaktari na Madaktari wa Meno ya Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa, Sheria ya Uhamiaji inaelekeza kwamba tafsiri ya msamiati "*medical practitioner*" itakuwa kama ilivyotolewa chini ya Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Wataalamu wa Afya Shirikishi, Sura ya 152.

Dhumuni la marekebisho yanayopendekezwa ni kuoanishwa tafsiri ya msamiati huo katika sheria za pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ibara hii inapendekeza kuongeza tafsiri ya misamiati *"Diaspora Tanzanite Card" or "Card", "illegal immigrant", "order of departure", "smuggling of immigrants", "special status", "Tanzania non-citizen diaspora"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho hayo ni kuyafanya masharti yaliyoainishwa katika sheria na yale yanayopendekezwa kuongezwa yaeleweke kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 18 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 20(2) kwa kufuta neno *"shall"* na badala yake kuweka maneno *"may also"* ili kuondoa sharti la lazima kwa Afisa Uhamiaji kunakili ushahidi wa mtuhumiwa kwa kutumia *video,* picha na teknolojia ya kunasa sauti. Lengo la marekebisho ni kuondoa ulazima kwa Afisa Uhamiaji kuchukua maelezo ya mtuhumiwa kwa njia zote zilizotajwa na Sheria na badala yake kumpa uhuru wa kutumia njia mojawapo katika kufanya uchunguzi kadri mazingira yatakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 22, inapendekeza kuongeza vifungu vya 36A, 36B, 36C, 36D, 36E na 36F mara baada ya Kifungu cha 36 kwa lengo la kuweka masharti yanayohusu hadhi maalum "*Special Status*" kwa raia wa nchi nyingine ambaye aliwahi kuwa raia wa Tanzania au mwenye asili ya Tanzania. Maudhui yaliyopo kwenye ibara hii sitayasoma kwa vile Serikali imeshayaondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza Marekebisho ya Sheria ya Ardhi, Sura 113. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 29 hadi Ibara ya 31 ya Muswada. Sehemu hii ya Sita pia sitaisoma kwa sababu Serikali imekubali kuondoa mapendekezo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kwenye Maoni na Ushauri wa Kamati; kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria

Mkuu wa Serikali isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432. Kwenye Ibara ya 6 na 7 ya Muswada Kamati iliishauri Serikali kufanya rejea sahihi katika vifungu kwa kurekebisha makosa ya kiuandishi na kurudisha vifungu vilivyopendekezwa kufutwa ambavyo vinaweka msingi wa namna Sekretarieti ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu itafanya kazi pamoja na Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji, Sura 54. Ibara ya 18 inapendekeza kufanya maboresho kwenye Kifungu cha 20(2) kwa kuondoa ulazima kwa Afisa Uhamiaji anapochukua maelezo ya mtuhumiwa kurekodi maelezo yanayotolewa na mtuhumiwa kwa njia ya *video,* picha na vinasa sauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchakataji wa mapendekezo haya Kamati ilizingatia kwa umakini falsafa ya *4R* za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na jitihada kubwa anazozifanya za kuimarisha mifumo ya Haki Jinai, Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais kwa dhati kwa uongozi wake mahiri kwenye masuala ya haki jinai na nia ya dhati aliyonayo ya kulinda haki za Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina maoni kuwa mfumo ulivyo sasa wa ukusanyaji wa ushahidi unaofanywa na Jeshi la Uhamiaji ni wa usasa zaidi ambao unaimarisha usahihi wa ushahidi, uwazi, uwajibikaji na unalinda haki za mtuhumiwa, mfumo ambao ni ushauri wa Kamati kuwa unapaswa kuzingatiwa na vyombo vingine vya Kiuchunguzi. Kamati iliishauri Serikali kuondoa mapendekezo hayo na kuimarisha zaidi uwezo wa Jeshi

hilo hususani wa kibajeti ili liweze kutekeleza jukumu hilo. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Marekebisho yanayopendekeza suala la Hadhi Maalum "*Special Status*" kupitia *Diaspora;* Ibara mbalimbali za sehemu ya Tano na Sehemu ya Sita ya Muswada huu yanalenga kuwapa watu wasio raia lakini wenye asili ya Tanzania Hadhi Maalum yaani "*Special Status*", hadhi ambayo inaambatana na haki mbalimbali ikiwemo umiliki wa ardhi ya jumla na ardhi ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwenye utoaji wa hadhi hiyo kwa raia ambao sio Watanzania lakini wana asili ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ili kutekeleza azma hiyo kwa ufanisi zaidi Kamati ilishauriana na Serikali kuhusu mambo yafuatayo:-

(a) Umuhimu wa ukamilishaji wa sera mbalimbali za nchi zikiwemo sera ya ardhi na sera ya mambo ya nje (Diplomasia ya uchumi) ili Sheria zitakazotungwa ziendane na sera za nchi;

(b) Takwimu ya idadi ya walengwa ifahamike ili Kamati iweze kupima athari ya mapendekezo hayo; na

(c) Umuhimu wa kuwa na Sheria mahususi itakayofafanua kwa upana wake masuala ya *Diaspora* kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia mjadala mpana na mashauriano ya kina ya Kamati na Serikali, tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati, katika hili Serikali imeondoa sehemu hizo zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tisa ya Muswada huu inafanya marekebisho ya Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 127. Kamati ina maoni kuwa marekebisho ya Sheria zinazotungwa kwa Lugha ya Kiswahili yafanyike kwa Lugha ya Kiswahili sambamba na marekebisho ya Sheria zilizotungwa kwa Lugha ya Kiingereza marekebisho yake yafanyike kwa lugha hiyo. Kwa msingi huo Kamati ilishauri Jina la Sheria kwenye kichwa cha habari cha Sehemu ya Tisa isomeke Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 127 na kufuta maneno "*Planning Commission Act, Cap 127*". Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia masuala muhimu ya Kitaifa, naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu za Kudumu za Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Hamza Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Ndugu Samwel Maneno, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali, Ndugu Onorius Njole; pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya Kamati, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (Na.2) WA MWAKA 2024 *[THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS)* (No.2) *BILL, 2024]* KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

### Maelezo ya Awali na Hadidu za Rejea

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2024)*.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 93 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Muswada huu ulisomwa Bungeni mara ya kwanza katika Mkutano wa kumi na tano, kikao cha hamsini na sita kwenye Bunge la 12, tarehe 28 Juni, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 136 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina.

Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Namna Kamati ilivyotekeleza Jukumu la Uchambuzi wa Muswada**

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 14 Agosti, 2024 ili kupokea maelezo ya aliyekua Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Eliezer Mbuki Feleshi (Mb) kuhusu maudhui ya Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika Ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mikutano ya Kusikiliza Maoni ya Wadau *(Public Hearings*) kwa siku mbili kuanzia tarehe 15 hadi 16 Agosti 2024 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya mtandao kutoka wadau mbalimbali ambao hawakuweza kufika mbele ya Kamati kuwasilisha maoni yao. Kipekee Niwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao ili kuuboresha muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa kuzingatia maoni ya Wadau. Mnamo tarehe 22 Agosti, 2024 Kamati ilikutana na Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb) Waziri wa Katiba na Sheria ambae alijibu na kutoa ufafanuzi juu ya hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati kuhusu Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, nilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kukujulisha rasmi kwamba Kamati imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

### 2.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2024 *[The*

*Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2024]* ukiwa umegawanyika katika sehemu tisa (9) na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria nane (8) kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizo. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo: -

(a) Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432 (*The Anti-Trafficking in Person Act, (Cap 432));*

(b) Marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 *(The Criminal Procedure Act, (Cap 20))*;

(c) Marekebisho ya Sheria ya Serikali Mtandao, Sura ya 273 *(The e-Government Act, (Cap 273))*;

(d) Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54 *(The Immigration Act, (Cap 54))*;

(e) Marekebisho ya Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 *(The Land Act, (Cap 113))*;

(f) Marekebisho ya Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura ya 70 *(The Medical Stores Department Act, (Cap 70))*;

(g) Marekebisho ya Sheria ya Viwango, Sura ya 130 *(The Standards Act, (Cap 130))*; na

(h) Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 127.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu masharti ya utangulizi, inayojumuisha **Ibara ya 1** inayohusu jina fupi na **Ibara ya 2** inayoelezea marekebisho yanayopendekezwa kufanyika katika sheria mbalimbali.

## 2.2 Sheria Zinazofanyiwa Marekebisho na Maudhui yake

**Mheshimiwa Spika**, Wakati tunafanya uchambuzi wa Muswada huu Pamoja na Maelezo ya Serikali, Kamati ilibaini changamoto au mapungufu katika sheria tatu kati ya sheria nane zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho kama zilivyo wasilishwa na mtoa hoja.

**2.2.1 Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza **Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432.** Marekebisho hayo yanayofafanuliwa katika Ibara ya 3 hadi Ibara ya 9 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa Marekebisho kwenye Sheria hii kwa ujumla wake yanalenga kutatua changamoto zilizojitokeza wakatii wa utekelezaji wa vifungu mbalimbali vya sheria hii na kuboresha vifungu hivyo ili kuimarisha nyanja zote za kuzuia usafirishaji haramu wa Binadamu.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 6 inapendekeza kurekebisha Sehemu ya Nne ya Sheria kwa kuongeza Sehemu ya Nne A kubwa inayoboresha muundo wa Sekretarieti ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu na kuongeza kifungu cha 24 A kubwa ambacho kinafafanua majukumu ya Sekretarieti hiyo kuwa ni:

a) kuratibu shughuli za taasisi mbalimbali katika masuala yanayohusu usafirishaji haramu wa binadamu;

b) kuchukua hatua kwa kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu kwa kutoa elimu kwa umma, kutoa mafunzo, kufanya uchunguzi wa pamoja na kuvunja mtandao na njia za usafirishaji haramu wa binadamu;

c) kutambua, kuokoa, kulinda, kurekebisha na kuwaunganisha waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu;

d) kuhakikisha utekelezaji wa mikataba ya kimataifa kuhusu masuala yanayohusu usafirishaji haramu wa binadamu

ambayo Jamhuri ya Muungano ni sehemu ya mikataba hiyo;

e) kushirikiana na vyombo vingine katika uchunguzi na uendeshaji wa mashtaka ya biashara haramu ya binadamu;

f) kukuza ushirikiano na taasisi za kimataifa, kikanda na kitaifa katika kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu;

g) kuanzisha, kuwezesha, kukuza na kusimamia uendeshaji wa nyumba salama kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu;

h) kufanya utafiti, kusimamia na kufuatilia matukio ya usafirishaji haramu wa binadamu nchini; na

i) kutekeleza majukumu mengine kama itakavyohitajika katika kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu hayo, Muswada unapendekeza kuwa Sekretarieti inaweza;

a) kuanzisha mfumo wa ukusanyaji na usimamizi wa data kuhusu usafirishaji haramu wa binadamu katika ngazi ya taifa;

b) kuingia katika jengo lolote kwa madhumuni ya kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu; na

c) kuomba taarifa yoyote na kumuita mtu yeyote anayejihusisha na usafirishaji haramu wa binadamu.

**Mheshimiwa Spika**, Vifungu vya 24B, 24C na 24D vinaweka utaratibu wa uteuzi wa Katibu na Makatibu Wasaidizi wa Sekretarieti pamoja na utaratibu wa kuajiri watumishi wa Sekretarieti hiyo. Lengo la marekebisho ni kubainisha na kufafanua majukumu ya Sekretarieti ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, kuongeza uwezo wa Sekretarieti kwa

kuhakikisha ina wasaidizi na watumishi wa kutosha katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 7 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 30, kwa –

a) kufuta na kuandika upya kifungu cha 30 (2) ili kuipa Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu mamlaka ya kuteua sekretarieti baada ya kushauriana na Waziri; na

b) kufuta vifungu vidogo vya (3) na (4) vinavyoweka msingi wa namna Sekretarieti itafanya kazi na Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la marekebisho ni kuendana na mabadiliko yanayopendekezwa katika Kifungu cha 24B, 24C na 24D.

**2.2.2 Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza **Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji, Sura 54**. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 15 hadi Ibara ya 28 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 16 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 3 kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya msamiati "*medical practitioner*" yaani daktari wa matibabu kwa lengo la kuwajumuisha watu wanaotambuliwa kuwa ni madaktari chini ya Sheria ya Madaktari na Madaktari wa Meno ya Tanzania Zanzibar.

**Mheshimiwa Sasa,** Kwa sasa, Sheria ya Uhamiaji inaelekeza kwamba tafsiri ya msamiati "*medical practitioner*" itakuwa kama ilivyotolewa chini ya Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Wataalamu wa Afya Shirikishi, Sura ya 152. Dhumuni la marekebisho yanayopendekezwa ni kuoanishwa tafsiri ya msamiati huo katika Sheria za pande mbili za Muungano.

Vilevile, Ibara hii inapendekeza kuongeza tafsiri ya misamiati *"Diaspora Tanzanite Card" or "Card", "illegal immigrant", "order of departure", "smuggling of immigrants", "special status", "Tanzania non-citizen diaspora"*.

**Mheshimiwa Spika,** Lengo la marekebisho hayo ni kuyafanya masharti yaliyoainishwa katika Sheria na yale yanayopendekezwa kuongezwa yaeleweke kwa urahisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 18 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 20 (2) kwa kufuta neno *"shall"* na badala yake kuweka maneno *"may also"* ili kuondoa sharti la lazima kwa Afisa Uhamiaji kunakili ushahidi wa mtuhumiwa kwa kutumia video, picha na teknolojia ya kunasa sauti. **Mheshimiwa Spika**, Lengo la marekebisho ni kuondoa ulazima kwa Afisa Uhamiaji kuchukua maelezo ya mtuhumiwa kwa njia zote zilizotajwa na Sheria na badala yake kumpa uhuru wa kutumia njia moja wapo katika kufanya uchunguzi kadri mazingira yatakavyoruhusu.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 22 inapendekeza kuongeza vifungu vya 36A, 36B, 36C, 36D, 36E na 36F mara baada ya kifungu cha 36 kwa lengo la kuweka masharti yanayohusu hadhi maalumu *"Special Status"* kwa raia wa nchi nyingine ambaye aliwahi kuwa raia wa Tanzania au mwenye asili ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 36A kinapendekeza kuweka utaratibu na masharti ya maombi kwa mtu anayetaka kuomba hadhi maalumu kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji.

**Mheshimiwa Spika**, Mapendekezo hayo yanalenga kumuwezesha Kamishna Jenerali atakaporidhika na utimilifu wa vigezo hivyo kutoa hadhi maalumu na kumpa mwombaji Kadi ya Tanzanite ya Diaspora yaani "*Diaspora Tanzanite Card*".

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 36B kinapendekeza kumpa mamlaka Kamishna Jenerali baada ya kuridhika kwamba mwombaji ana taaluma adimu, ya kipekee au adhimu, kipaji au ujuzi ambao ni wa umuhimu kwa Jamhuri ya Muungano, kutoa hadhi maalumu na kutoa kadi ya Diaspora Tanzanite kwa

mwombaji, bila kujali kuwa mtu huyo atazingatia au atakuwa na maadili au utamaduni wa Mtanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 36C kinaweka muda wa uhalali wa kadi ya mtu mwenye hadhi maalum kuwa miaka kumi na inaweza kuhuishwa kwa kipindi kingine.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 36D kimempa mamlaka Kamishna Jenerali kwa kuzingatia masharti yalioanishwa katika kanuni, kutoa pasi tegemezi kwa wategemezi wa mwenye kadi kwa maombi yaliyofanywa kwa niaba ya mtu aliyepewa hadhi maalumu. Aidha, masharti ya kifungu cha 39 yatatumika kwa maboresho kwa kuzingatia maudhui ya kuisha kwa muda wa pasi tegemezi. Vilevile, kifungu kimetoa fasili ya neno "*dependant*" kuwa ni mwenza, mtoto au ndugu wa mtanzania asiyeraia na mkaazi wa nchi nyingine.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 36E kinaweka masharti ya kuzingatia kwa mtu aliyepewa hadhi maalumu. Masharti hayo ni:

a) kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Sheria nyingine;

b) kuzingatia masharti ya hadhi maalumu kama yalivyotolewa chini ya sheria; na

c) kuwa na maadili mema.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 36F kinampa mamlaka Kamishna Jenerali kufuta hadhi maalumu kama akijiridhisha kuwa:

a) mtu aliyepewa hadhi maalumu amekiuka masharti yoyote ya hadhi maalumu;

b) hadhi maalumu ilipatikana kwa njia ya ulaghai, udanganyifu au kwa kuficha ukweli wowote;

c) mtu amejionesha kwa kitendo au maneno kuwa si mwaminifu au hana mapenzi na Jamhuri ya Muungano;

d) mtu amefanya biashara au mawasiliano kinyume cha sheria na adui wa Jamhuri ya Muungano au amekuwa akijihusisha na shughuli yoyote inayofanywa kwa namna ya kumsaidia adui;

e) mtu anaejihusisha na kitendo chochote ambacho ni kinyume na maadili ya Jumhuri ya Muungano; au

f) haadhi hiyo haifai kwa manufaa ya umma kwamba mtu huyo aendelee kushika hadhi hiyo maalumu.

Aidha, mapendekezo hayo yanafafanua kuwa kufutwa kwa hadhi maalumu kutajumuisha ubatilishaji wa moja kwa moja wa Kadi na mmiliki atatakiwa kurudisha kadi hiyo kwa mamlaka husika. Mtu ambaye hadhi yake imefutwa, anaweza, ndani ya mwezi mmoja kuanzia tarehe ya kufutwa, kuomba kwa Kamishna Jenerali hadhi nyingine ya uhamiaji kama ilivyobainishwa kwenye sheria.

**2.2.3 Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza **Marekebisho ya Sheria ya Ardhi, Sura 113**. Marekebisho hayo yanafafanuliwa katika Ibara ya 29 hadi Ibara ya 31 ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 30 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 2 kwa kuongeza katika mpangilio wa kialfabeti, tafsiri ya neno "*special derivative right*". Lengo la marekebisho ni kutoa tafsiri ya neno hilo ambalo limetumika katika marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 31 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 19(1) kwa kuongeza vifungu vidogo vya (1A), (1B), (1C), (1D) na (1E). Lengo la marekebisho ni kumwezesha raia wa kigeni mwenye asili ya Tanzania kumiliki au kuondosha miliki aliyoipata kwa njia mbalimbali ikiwemo urithi au umiliki wa kununua.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu kidogo cha (1A) kinapendekeza kumpa haki maalumu ya kumiliki na kutumia ardhi mtu au kampuni ambayo wanahisa walio wengi wana hadhi maalumu kwa mujibu wa Sheria ya Uhamiaji, na wanahisa wachache waliobakia ni raia wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu kidogo cha (1B) kinapendekeza kumpa uhuru Kaminishna wa Ardhi kutoa haki maalumu ya umiliki wa ardhi inayotokana na ardhi ya jumla yaani "*general land*" au ya ardhi Vijiji "*village land*" baada ya maombi kwa masharti yaliofafanuliwa kwenye Sheria.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, Kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuuboresha Muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata: -

### 3.2 Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432 (*The Anti-Trafficking in Person Act, (Cap 432)*).

**Mheshimiwa Spika,** Kwenye Ibara ya 6 na 7 ya Muswada Kamati iliishauri Serikali kufanya rejea sahihi katika vifungu kwa kurekebisha makosa ya kiuandishi na kurudisha vifungu vilivyopendekezwa kufutwa ambavyo vinaweka msingi wa namna Sekretarieti ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu itafanya kazi pamoja na Kamati ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.3 Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji, Sura 54 (*The Immigration Act, (Cap 54)*).

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 18 inapendekeza kufanya maboresho kwenye kifungu cha 20(2) kwa kuondoa ulazima kwa Afisa Uhamiaji anapochukua maelezo ya mtuhumiwa ku rekodi maelezo yanayotolewa na mtuhumiwa kwa njia ya Video, picha na vinasa sauti.

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchakataji wa mapendekezo haya Kamati ilizingatia kwa umakini **falsafa ya 4R za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** na jitihada kubwa anazozifanya za **kuimarisha mifumo ya Haki Jinai**, Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais kwa dhati kwa uongozi wake mahiri kwenye masuala ya haki jinai na nia ya dhati aliyonayo ya kulinda haki za Watanzania wote.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa mfumo ulivyosasa wa ukusanyaji wa ushahidi unaofanywa na Jeshi la Uhamiaji ni wa usasa zaidi ambao unaimarisha usahihi wa ushahidi, uwazi, uwajibikaji na unalinda haki za mtuhumiwa, mfumo ambao ni ushauri wa Kamati kuwa unapaswa kuzingatiwa na vyombo vingine vya Kiuchunguzi. Kamati iliishauri Serikali kuondoa mapendekezo hayo na kuimarisha zaidi uwezo wa Jeshi hilo hususani wa kibajeti ili liweze kutekeleza jukumu hilo. Tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.4 Marekebisho yanayopendekeza suala la Hadhi Maalum

**Mheshimiwa Spika,** Ibara mbalimbali za sehemu ya Tano na Sehemu ya Sita ya Muswada huu yanalenga kuwapa watu wasio raia lakini wenye asili ya Tanzania Hadhi Maalum yaani "*Special Status*", Hadhi ambayo inaambatana na haki mbalimbali ikiwemo umiliki wa ardhi ya jumla na ardhi ya vijiji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwenye utoaji wa hadhi hiyo kwa raia ambao sio Watanzania lakini wana asili ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kutekeleza adhma hiyo kwa ufanisi zaidi Kamati ilishauriana na Serikali kuhusu mambo yafuatayo: -

i. Umuhimu wa ukamilishaji wa sera mbalimbali za nchi zikiwemo sera ya ardhi na sera ya mambo ya nje (Diplomasia ya uchumi) ili Sheria zitakazotungwa ziendane na sera za nchi;

ii. Takwimu ya idadi ya walengwa ili Kamati iweze kupima athari ya mapendekezo haya; na

iii. Umuhimu wa kuwa na Sheria mahususi itakayofafanua kwa upana wake masuala ya Diaspora kwa ujumla wake.

**Mheshimiwa Spika**, Kufuatia mjadala mpana na mashauriano ya kina ya Kamati na Serikali, tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

### 3.5 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tisa ya Muswada huu inafanya marekebisho ya Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 127, Kamati ina maoni kuwa marekebisho ya Sheria zinazotungwa kwa lugha ya Kiswahili yafanyike kwa lugha ya Kiswahili sambamba na marekebisho ya Sheria zilizotungwa kwa lugha ya Kingereza marekebisho yake yafanyike kwa lugha hiyo. Kwa msingi huo Kamati ilishauri Jina la Sheria kwenye kichwa cha habari cha sehemu ya Tisa isomeke Sheria ya Tume ya Mipango, Sura ya 127 na kufuta maneno "*Planning Commission Act, Cap 127*". tunaipongeza Serikali kwa kukubali ushauri na kuleta marekebisho kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb | **M/ Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo,Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Omar Issa Kombo, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe.Seif Khamis Said Gulamali, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe.Aziza Sleyum Ally, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe.Suma Ikenda Fyandomo, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe.Joseph Anania Tadayo, Mb | Mjumbe |
| 22. | Mhe.Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Hamza Johari (Mb) Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ndg. Samwel Maneno Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali Ndg. Onorius Njole,

pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa ushirikiano wao wa dhati katika kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* na kwa upekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**4.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya Kamati naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb)
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
03 Septemba, 2024

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; Wageni Waheshimiwa Wabunge; wageni 36 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; Wanafunzi 61 na Walimu watano wa Shule ya *Ridhwaa Seminary* kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni. *(Makofi)*

Wanafunzi 19 na viongozi sita wa Chama cha Skauti Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa, sasa tunaanza mjadala, tunaanza na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, wajiandae Mheshimiwa Pauline Gekul na Mheshimiwa Abeid Ighondo.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi na kuwa mchangiaji katika Miswada hii miwili, lakini nitachangia zaidi Muswada mmoja wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ambao umewasilishwa leo hapa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maudhui mengi katika Muswada huu na zipo sehemu nyingi ambazo zimeletwa mbele yetu, lakini kimsingi nichukue nafasi hii kama alivyosema Mwenyekiti wetu wa Kamati Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama kwamba, Serikali hii sikivu inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, lakini humu ndani chini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wamesikia na kuelewa mawazo na maoni ya Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria katika utunzi wa Sheria hizi ambazo zimekuja kurekebishwa katika Kamati yetu lakini zije katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia kwa jumla sana kwa sababu baadhi ya mambo ambayo nilikuwa nimejipanga nayo Serikali imeyaondoa, lakini baadhi ya mambo ambayo tunapaswa kuyazungumza na kuonesha ni kwa nini, tunapaswa kutunga Sheria ambazo zinaishi, lakini ziwe na maslahi mapana na nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Bunge kama ilivyo kazi yake ni kutunga sheria, lakini sheria ambazo zitaenda kutekelezeka kirahisi zaidi lakini ziwe na tija na ufanisi mkubwa katika kuzitekeleza hizo sheria ambazo zitatungwa na Bunge lako Tukufu. Tunazo sera mbalimbali ambazo zinatakiwa zitangulie ili sheria nyingine zije, tunayo changamoto mpaka sasa hivi sera ya ardhi bado haijawa tayari. Kwa hiyo, ndio maana unakuta baadhi ya mambo ambayo ilikuwa inataka kuchakatwa yalikuwa yanawahisha shughuli mapema zaidi kuliko ambavyo ingepaswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hatuna sera nzuri ya biashara kwa nini? Unamkuta Kariakoo Mchina anauza biashara ndogo sana ambazo si za wawekezaji, lakini migahawa ambayo ingeweza kufunguliwa na Tanzania inafunguliwa na wageni. Kwa hiyo, yalipokuwa yanakuja haya yanaonesha ni namna ambayo

pengine kungekuwa na mkanganyiko mkubwa wa hii kadi ya *Tanzanite Card* kwa raia ambao wangepewa watu waliokuwa wanalengwa na sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Uraia ndio ilikuwa inapaswa kulishughulikia sana jambo hili kuliko Sheria ya Uhamiaji; Sheria ya Uhamiaji inahusika tu na wale raia au watu wageni waonaoingia nchini au raia wa Tanzania wanaosafiri nchi nyingine kwa maana wao ni ukaguzi uhalali wa nyaraka mbalimbali lakini na kuhakikisha watu wanaingia nchi hii wana nyaraka zinazohusika na pengine usalama wao au namna ambavyo wanapita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo lilikuwa na ukakasi mkubwa kwa namna ambavyo limeletwa, lakini kuna vitu vingi ambavyo vilikuwa vinataka viingie humu ikiwemo haki ambayo ya umiliki wa ardhi ambazo zinapita *TIC,* lakini kadi hii ilikuwa inampa mtu namna ambayo angeweza kuitumia. Pia kulikuwa na hoja kubwa kwamba *derivative right* ambayo angepewa huyu mtu ambaye ana *Tanzanite Card,* ile *title deed* anayemiliki ni nani? Maana yake *derivative right* ambayo wanapewa watu kupitia *TIC* mwenye umiliki wa hati ile kubwa *title deed* ni *TIC,* sasa hapa kulikuwa na mkanganyiko mkubwa wa sheria. Kwa hiyo, ndiyo maana Kamati imeona ni vizuri basi jambo hili likarejeshwa ili lije katika utaratibu ambao ni sahihi na bora zaidi kwa ajili ya utekelezaji wa sheria lakini na Bunge lako Tukufu mbele ya jamii lionekane limefanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo ambalo limetajwa hapa la *MSD, MSD* ni Taasisi ambayo inahusika na usalama wa dawa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni Taasisi ambayo utendaji wake unadhibitiwa na Sheria ngumu kidogo, sasa hapa wanataka kuweka ulaini kidogo ili kuifanya *MSD* iweze kufanya biashara, lakini iweze kujitanua na iweze kuwekeza mtaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe *MSD* wamepewa kazi katika ukanda huu wa Afrika Mashariki, katika ukanda wa *SADC,* kuweza kuagiza dawa na baadhi ya nchi zime-*respond.* Sasa Sheria zetu zilikuwa zimeifunga *MSD,* kwa maelekezo ya Msajili wa

Hazina itaenda kufungua milango ambayo *MSD* itafanya biashara na maeneo mengine ya nchi hii, lakini usalama wa dawa katika Jamhuri ya Muungano umezingatiwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mabadiliko ambayo kidogo yameibadilisha Tume ya Mipango na sasa itaitwa Tume ya Taifa ya Mipango. Kuna viongozi ambao kwa nafasi zao wametajwa na Sheria hii ikiwemo Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu mwenye dhamana ya masuala ya uwekezaji na Katibu Mkuu mwenye dhamana ya masuala ya fedha pia, wametajwa katika mabadiliko haya. Kwa hakika na sisi, kamati pamoja na maoni ya wadau ambao wamekuja mbele ya kamati yetu, tumeridhia na kuona jambo hili ni zuri na lina tija kama taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 21 ilikuwa inalengwa kurekebisha Sheria ya Ushahidi ya Uhamiaji. Sheria ya Ushahidi ya Uhamiaji inamtaka mchukuwa maelezo aidha achukuwe maelezo ya karatasi, lakini ayarekodi kwenye chombo ambacho kinachukuwa sauti, lakini pia, arekodi picha za video. Hii faida yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sisi Wabunge na Bunge hili ni mashahidi, tumeona aliunda tume ambayo inaenda kuangalia Tume ya Haki Jinai chini ya Jaji Chande. Moja ya vitu ambavyo tunaviona, tume inaviona, ni kuboresha, lakini dhamira ya Mheshimiwa ni kuboresha haki jinai katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunapoenda kufifisha uchukuwaji wa ushahidi badala ya kuwa na maeneo mapana kuwe na video, kuwe na sauti na maandishi. Tunapoenda kupunguza baadhi ya vitu tunaenda kufifisha haki jinai katika Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania. Kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, yaliyokuwepo miaka 20 nyuma, 2004 ndiyo ilitungwa hii Sheria. Leo, miaka 20 baadaye tuone kwamba, kuchukua huu ushahidi wa *video* ni jambo baya. Kwa kweli, haikufaa na haikupendezwa na ndiyo maana Kamati imeliona hili kwa kweli, halifai kuwa miongoni mwa mambo ambayo yanapaswa kubadilishwa katika sheria hii. Kwa hiyo, ninaunga mkono hoja hii na ninaliomba Bunge Tukufu lipitishe

mapendekezo haya ya mabadiliko ya sheria mbalimbali kama yalivyokuja pamoja na *schedule of amendments* zilizokuja mbele ya Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Pauline Gekul, atafuatiwa na Mheshimiwa Abeid Ighondo na Mheshimiwa Salome Makamba ajiandae.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi. Pia, nimshukuru Mwenyezi Mungu kutupa afya sote tuendelee kutimiza wajibu wetu wa kuwakilisha wananchi wetu na kuisimamia Serikali, ikiwemo kushauri pamoja na kutunga Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wetu, Mheshimiwa Jafo na Baba yangu Mheshimiwa Kabudi kwa Mheshimiwa Rais kuendelea kuwaamini na kuwapa majukumu haya. Serikali yetu imekuwa sikivu, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu pia, nikupongeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wajumbe wa Kamati tunapokuwa tunakutana na Serikali wamekuwa wakitusikiliza na wamekuwa wapo *open minded*, wanatusikiliza vizuri, wanachukua hoja zetu na wanajadili kwa uhuru kabisa maoni ya wanakamati. Nimefarijika kuona kwamba, kwenye Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali hili jambo ambalo Mheshimiwa Mwenyekiti Mhagama amelishauri na Kamati yake, la hadhi maalum kwa wenzetu ambao wanaishi nje ya nchi, Serikali imelizingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Kamati ambao umetolewa ni mzuri sana kwamba, hata hawa watu ambao tunataka kuwapa hiyo haki ya kumiliki ardhi kwanza wapo wangapi na hizi sera za ardhi za biashara pia, zikiangaliwa na tukajua kama nchi tunataka kuwapa hadhi maalum Watanzania wenzetu ambao wapo nje ya nchi, kwanza ni wangapi, lakini

wana kitu gani wanataka kufanya kwenye ardhi hii ambayo wangetamani kumilikishwa? Sio tu idadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani pia, kama Mbunge, niongezee kwamba, sio tu idadi, tufahamu wapo wangapi kama ambavyo kamati imeshauri. Ninaunga mkono, lakini pia, ni *value* gani wanahitaji ku-*add* ambayo imeshindikana kwa dirisha la uwekezaji, wao wanataka kufanya kwa dirisha hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo pia, kwa sababu, ukifahamu idadi sio wote tu ambao wanastahili kupewa hiyo hadhi maalum. Ni kitu gani *special* wanataka ku-*add*, ili pia, waweze kuzingatia, lakini pia, niwapongeze kwa jinsi ambavyo mmepokea maoni ya Kamati na Wabunge na kuweza kuondoa Muswada huu na kipengele hicho, ili wakifanyie kazi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze sasa kwenye Muswada wa Sheria ya Ushindani ambao kamati yetu imeushughulikia kwa asilimia kubwa. Ni Muswada mzuri, ni marekebisho mazuri kwenye *angles* zote ambazo Serikali imetuletea na ni suala zuri tunapofanya biashara, suala la kampuni hizi na ku-*control* ushindani kwamba, mmoja asihodhi soko, ili Watanzania wasiathirike kwa kuhodhi kwake. Ni jambo jema na hata hizi *percentage* kutoka *35-40* za kuhodhi soko ni jambo jema, ili na wengine pia, waweze kuchangia uchumi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tume kuchunguza moja kwa moja na pia, kusikiliza rufaa zile ambazo zinakatwa kutoka huko ambako wenzetu wameshindwana wakaenda kwenye Tume ya Ushindani. Serikali kuona hili kwamba, tume iwe na *final decision* inaweza ikawa inanyima haki ya wananchi kutumia haki yao ya Kikatiba ya kwenda mahakamani kupata hiyo haki badala ya kushidwana na tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kuliona hili kwamba, tuna Ibara ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inataka yeyote ambaye yupo *aggrieved,* ambaye ameona hajaridhishwa na maamuzi fulani aweze kwenda kwenye Mahakama, ili aweze kusikilizwa na Mahakama

iwe ni chombo cha mwisho kutoa haki. Kwa hiyo, hili nimpongeze kabisa Mheshimiwa Waziri Jafo kutuletea marekebisho haya na kuona ni kwa kiasi gani Mahakama inaweza ikashiriki katika kutoa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Ibara ya 13 ambayo inafuta Kifungu cha 17 cha Sheria na inaandika upya, sasa tunaleta masharti ya wafanyabiashara ku-*display prices* za biashara zao ambazo wanazifanya, hili ni jambo jema sana, kwamba, sasa tunatambulisha bei kwa kila mfanyabiashara anayefanya biashara na wauzaji wa biashara mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali mwanzoni ilikuja na adhabu ya kwamba, ambaye hajafanya *display* ya *prices* katika bidhaa au huduma anayotoa, basi faini kuanzia shilingi 300,000 mpaka shilingi 1,000,000. Kamati yetu imefanya kazi na Serikali imepokea ushauri wetu kwamba, tuna wafanyabiashara wakubwa na wadogo. Kwenye *price display* ni jambo ambalo tunaliunga mkono, lakini nishukuru kwamba, wamepunguza pia, hii adhabu. Wameshauri kwamba, iwe faini sasa, itoke badala ya shilingi 300,000 ishuke iwe shilingi 10,000 mpaka shilingi 1,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nitaendelea kuishauri Serikali yangu sikivu kwamba, kiwango cha juu kiendane na aina ya wafanyabiasha tulionao. Wale ambao wanafanya kazi katika *Local Government,* wale wafanyabiashara wadogo wadogo, bado shilingi milioni moja hawatoimudu kwa sababu, kuna mmachinga ambaye anatembeza bidhaa zake, ni kweli ata-*display*, tumekubaliana ata-*display.* Mimi kama Mbunge ambaye nawawakilisha wananchi wa Jimbo la Babati Mjini, wengi ni wafanyabiashara wadogo wadogo. Jambo hili kama mwakilishi wao pia, nitawaomba na nitashiriki katika kuwaelimisha wakubali kwa sababu, kama kuna jambo nchi hii bado halijakaa vizuri ni suala la walaji kwenda kununua vitu ambavyo ukienda wewe utauziwa shilingi 10,000 mwingine shilingi 2,000 na mwingine shilingi 1,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walaji wanaathirika kwa hiyo, ninaipongeza Serikali. Watu wana biashara zao wanamiliki, *let say* duka lako umemwachia kijana wa kazi yeye ndiye anapanga bei kwa sababu, wewe haupo. Akienda aliyevaa suti atapewa shilingi 100,00, mtu anatathminiwa, muuzaji anaamua kwenye duka lako apange bei amuuzie nani kitu gani kwa bei gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawapongeza Serikali kwa dhati kwamba, tumeamua kufanya price *display,* kwamba, bei tutaweka iwe ni mama lishe pale nje, kwanza wameshaanza wanaweka baadhi. Kwa hiyo, Muswada huu utakwenda kuhakikisha kwamba, watu wanaweka hizo bei, lakini hii faini Mheshimiwa Waziri huwezi kuniambia kwamba, mama lishe mwenye mtaji wa shilingi 50,000 atalipa faini mpaka ya shilingi 1,000,000. Sawa, umeshatoa *room* ya shilingi 10,000,000, kwa nini usifanye ikawa labda *special group,* ikawa mpaka shilingi 50,000 isizidi shilingi 50,000 badala ya shilingi 1,000,000?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naungana na wewe kabisa, nakupongeza kwa usikivu, lakini kwenye faini hii shilingi 10,000 mpaka shilingi 1,000,000, hebu shuka. Umekubali kushuka kutoka shilingi 300,000 mpaka shilingi 10,000, sasa kile kiwango cha juu kishushe kulingana na aina ya wafanyabiashara ambao tunao katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la rufaa pia, Mheshimiwa Waziri nikupongeze kwamba, sasa hii kesi ya rufaa hizi za wafanyabiashara wetu itaenda kwenye Mahakama ya Rufaa kwenye ngazi ya Mahakama Kuu kwa jopo la Majaji watatu. Nilikuwa nakushauri Mheshimiwa Waziri, bado uangalie pia, hili jambo lishuke kwenye Mahakama za Wilaya za Mwanzo kwa sababu, si umeshawa-*include* hata wale ambao kwa mujibu wa Wizara ya Fedha ambao mitaji yao haifiki shilingi milioni nne na wao pia, wana-*contribute* pale ambapo wanakuwa hawajafanya *price display* pia na wao wanahusika na jambo hili la hizi faini.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi *listening* yao na *referral* zao ziende kwenye Mahakama zao zile ambazo siku zote wanafanya

nazo kazi badala ya kuwaachia tu Mahakama Kuu kwenye majopo ya Majaji watatu washughulike mpaka na muuza karanga, ambaye haja-*display price* ambayo ilitakiwa kuwa-*displayed according to* Sheria hii na Muswada huu ambao tunaupitisha. Pia, nimwombe Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Jafo, aangalie kuwatumia wenzetu wa *TCCIA (Tanzania Chamber of Commerce)*. Wale sasa hivi *membership* kwenye *TCCIA* ni *optional*. Ninashauri pia, *TCCIA* waangalie *compulsory membership* kwenye taasisi yao kwa sababu, wale ndiyo watakusaidia *enforcement* ya Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Ushindani sasa yenyewe iangalie iwe ni taasisi ya *referral.* Suala la *price* halijawa *displayed,* basi iende kwa *TCCIA* kwa kuwa, wao wanafanya kazi katika *locality* zetu na wapo mpaka katika ngazi za Mikoa, lakini pia, *FCC* ishuke, isibaki kwenye *National level*. *FCC* ishuke kwenye Mikoa, ifike kwenye Wilaya, ili wanapofuatilia na hizo *referrals* halafu ndiyo ziende Mahakamani wafanye kazi sambamba na *TCCIA*. Kwa hiyo, kwa kuwa, umeshaanza, umeongeza nguvu ya *referral* kwenda kwenye Mahakama nimwombe pia *inclusion* ya *TCCIA* na *inclusion* ya Mahakama zetu za Mwanzo na za Wilaya, jambo hili litakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, *otherwise* niwapongeze, huu ni Muswada mzuri, walaji wa Tanzania wamekuwa wakipangiwa bei *according to their appearance*. Unakwenda unaambiwa kwamba, hii *price* ipo hivi, lakini pia, wamiliki wa biashara hizo wamekuwa wakipunjwa na wale wanaouza hizo biashara yeye anafaidika, utaona siku ya pili amefungua biashara nyingine kwa kuwapunja wateja wako, lakini wamekuwa wakishiriki kufukuza wateja katika biashara hizi ambazo watu wamezianzisha wakiwa na mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri. niwapongeze Serikali, ni kazi nzuri tutafanya pamoja na mwisho kabisa na Madiwani pia wapewe semina na viongozi na watendaji wapewe hizo semina, tufanye kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Igondo ameomba dharura, Mheshimiwa Salome Makamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma na Mheshimiwa Yustina Rahhi.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia kwenye marekebisho ya Sheria hizi, kwa maana ya Sheria ya Ushindani na Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Namba Mbili ya mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kwa kuchangia mabadiliko ya Sheria ya Ushindani ya mwaka 2024. Kwa utangulizi ninaomba nianze kwa kutoa ushauri, Sheria yetu ya Ushindani ya mwaka 2024 inasimamia ushindani huru, kwa maana ya *fair competition* na wakati huohuo inasimamia Sheria mbalimbali zinazohusika na kumlinda mlaji kwa maana ya *consumer protection.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye zama hizi ambazo biashara imetanuka, teknolojia imeongezeka, tunaingiza bidhaa nyingi nchini, kama ambavyo tunatoa bidhaa nyingi, kuunganisha Sheria za Ushindani wa Kibiashara na Sheria za Kumlinda Mlaji tunajiweka katika ufinyu wa kupanua mawanda ya kusimamia sheria hizi mbili. Kwa Taifa linalokwenda kwa kasi kimaendeleo, kama Tanzania, Mataifa mengi yanayofanana na sisi leo hii yametenganisha sheria hizi mbili ili kuweza kuimarisha namna ambavyo tunaweza kumlinda mlaji na namna ambavyo tunaweza kuzilinda biashara zetu ziweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona hata katika mabadiliko ya sheria hizi mbili tumejibana sana katika kuelezea namna gani tutaweza kumlinda mlaji. Tunajikuta wakati huohuo tume inayohusika au baraza linalohusika na *fair competition* kwa upande mmoja linataka ku-*promote* biashara na kwa upande mwingine linashusha chini *spirit* ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano mdogo, kwa mfano, sheria hii ambayo tunaifanyia marekebisho leo inasema tunakwenda kushusha na kuimarisha mabaraza haya katika ngazi za kanda na mikoa kwa kuyaongezea watumishi na kuongezea vitendea kazi, ili waweze kusimamia, waweze kukagua, waweze kufanya uchunguzi na waweze kutenda haki kwa wafanyabiashara, lakini sheria hiihii kwa upande mwingine inamlazimisha mfanyabiashara ambaye anatoa huduma kwa mlaji aweze kufanya *display,* aweze kuonesha gharama ya bidhaa anayouza kwa wananchi bila kujali mfanyabiashara huyo ana mtaji wa kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii inakwenda mbali zaidi, inakwenda kutoa adhabu ya jumla kwa mfanyabiashara atayeshindwa ku-*display,* kuonesha wazi gharama ya bidhaa zake. Inakwenda kutoa adhabu ya jumla bila kujali kuna mfanyabiashara ambaye ni mtu binafsi ana mtaji wa shilingi 50,000 na kuna mfanyabiashara ana mtaji wa shilingi 2,000,000, kama bodaboda, kuna mfanyabiashara ana mtaji wa shilingi 200,000, kama mama ntilie, haijali. Inatoa adhabu ya jumla kwamba, ikitokea mfanyabishara huyu ameshindwa kuonesha gharama ya bidhaa anazoziuza kwa maana ya ku-*display* kama ni muuza genge aoneshe machungwa haya yanauzwa shilingi mia tano, maembe yanauzwa shilingi mia mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, akishindwa kuweka hivyo vibao pale, atatozwa adhabu isyopungua shilingi 300,000 na isiyozidi shilingi 1,000,000. Sasa unajiuliza *spirit* ya Serikali ilikuwa ni kumfanya mfanyabiashara huyu aweze kuimarika na kukua kibiashara au kumrudisha chini kibiashara?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye sheria hii, mfanyabiashara huyu licha ya kuwekwa katika kundi ambalo hastahili, analazimishwa kufanya biashara kwenye mazingira ambayo Serikali hiihii haijamtengenezea mazingira bora ya kufanya biashara. Tujiulize leo, hivi unavyosema machinga aweze kufanya *display,* aweke bei ya vitu vyake, yaani anauza mikanda, tochi, sijui betri, atazitundika wapi hizo bei, ili kusudi uweze kuziona? Atajibandika kwenye mwili wake anavyotembeza zile

bidhaa zake? Ataandikaje na anauza mabeseni humohumo, chaja za simu…

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe Taarifa wakili msomi, Mheshimiwa Salome kwamba, Serikali imezingatia, adhabu hiyo ilikuwa shilingi 300,000 kwenye Muswada wa awali, lakini Kamati tulivyochakata tulishusha, ikazingatia hao machinga ambao anawataja, ikashusha adhabu mpaka shilingi 10,000. Kwa hiyo, kima cha chini kimezingatiwa.

**NAIBU SPIKA:** Hoja sio hiyo, machinga anatembea na *varieties* mkononi, bei anaziwekaje?

Mtu ana machungwa tenga, kuna vitu watu wana-*negotiate,* unakwenda kwa machinga pale, vitu vile vinauzwa kwa ku-*point*. Nataka hiyo, una-*negotiate* pale. *That's the issue,* tazameni na hawa watu wa chini. Nilikuwa sipendi kuingilia haya mambo lakini vitu vina, nendeni kwa machinga pale Kariakoo au nendeni machinga, Ilala pale wanapouza vitu, unanyanyuliwa shati unali-*point* hilo au hilo; *that's how they sell things.* Kwa hiyo, mimi nahisi kuna *level* ya *scope* ya biashara, lakini nafikiri hii, mama ntilie leo ugali shilingi 2,000, maharage shilingi 2,000, hajaweka. Jamani hebu lifikirieni upya hili suala. *(Makofi)*

Haya endelea Mheshimiwa Salome. *(Makofi)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunisaidia na ninamwongezea tu dada yangu Mheshimiwa Gekul, Kamati ilipendekeza adhabu angalau ianze shilingi 10,000 na isizidi shilingi 50,000 lakini Serikali inasema ni shilingi 10,000 mpaka shilingi 1,000,000. Bado adhabu hii ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakushukuru kwa kusaidia kutuongoza kwenye hilo. Hili suala tusipotenganisha sheria hizi mbili za kusimamia wafanyabiashara na kusimamia mradi, tutajiingiza kwenye mkakanganyiko ambao tutashindwa kuwasimamia hawa watu wawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na changamoto kubwa japokuwa Katiba yetu ya nchi Ibara ya 107A, inatoa *inherent power* kwa Mahakama kuweza kusimamia masuala yote. Ndiyo chombo cha mwisho kinachotoa haki japokuwa sheria hii ilikuwa inakinzana na Katiba kwa kiasi ambacho watu wengi kesi zao zilikuwa zinaishia kwenye baraza hili ambalo mwisho wa siku wakionekana hawajatendewa haki, kama hajapata haki ya uwakilishi kwa maana ya wakili, haki yake inakuwa imepotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kufungua mwanya huu, kama mtu hajaridhishwa na maamuzi ya *tribunal,* anaweza kwenda kwenye Mahakama Kuu. Pia, tuone haja ya kutibu jeraha ambalo tumelitengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Na.2 ya Mwaka 2024. Katika Ibara ya 16A, wanabadilisha kuitoa *MSD* chini ya Sheria ya Uwekezaji wa Wadhamini na kuipeleka katika Sheria ya Uwekezaji *(Tanzania Investment Act)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema, wameipeleka kule kwa sababu wanataka *MSD* iweze kujiendesha yenyewe, iweze kufanya uwekezaji na kukuza mtaji wake. Hapa hakuna ombwe la kisheria, hapa kuna ombwe la mtaji na ombwe kubwa la mtaji linasababishwa na Serikali yenyewe. Tusipotumbua jipu hapa tutakuwa tunaleta matamanio ambayo hayatekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya *CAG* ya mwaka jana, inasema *MSD* inaidai Serikali shilingi bilioni 315 na Serikali hii kwenye vituo vya huduma ya afya peke yake *MSD* inaidai Serikali shilingi bilioni 135.7. Hivi kwenye mazingira haya, hata tukiitoa *MSD* kutoka kwenye sheria ambayo tunasema

imepitwa na wakati, tukaipelekea kwenye sheria hii mpya ya *Tanzania Investment Act*, unadhani itasaidia *MSD* kusonga mbele?

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo sababu na ipo haja ya Serikali kulipa madeni kwenye mashirika ya umma. Tusipolipa madeni hatuwezi kuyasaidia mashirika haya kujiendesha kibiashara. Nimeona liko tamanio kubwa sana la kujaribu kumpa Mweka Hazina wa Serikali nguvu kubwa ya kusimamia mashirika, lakini kama Serikali halipi madeni, tutakuwa tunazunguka mbuyu pale pale na hatuwezi kutatua tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ya mwisho ni Ibara ya 18 ambayo inahusiana na Afisa Uhamiaji. Ibara hii ikuwa inamlazimisha afisa uhamiaji ambaye anachukua maelezo ya mtuhumiwa, kuchukua maelezo yale kwa maandishi, kuhakikisha anachukua *video* na picha za mnato, lakini sasa hivi sheria imeleta hapa mapendekezo; wanasema katika kuchukua maelezo ya mtuhumiwa, afisa uhamiaji anaweza kufanya hivyo na siyo lazima atumie njia zote hizo tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitunga hapa Sheria ya Serikali Mtandao, tulikuja hapa tukajinasibu kwamba Serikali yetu inakwenda kwenye Serikali Mtandao, kwa nini tunarudi nyuma? Kwa nini tunarudi nyuma kumruhusu afisa kwenye mazingira haya ambayo wahamiaji haramu *everywhere* ni tatizo na kwenye mazingira ambayo sheria ya ushahidi inaruhusu mtu kuchukuliwa *video* na maandishi, Serikali ijitafakari inaturudisha nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, ajiandae Mheshimiwa Rahhi.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye miswada hii. Kwanza kabisa, niweze kuwapongeza

Waheshimiwa Mawaziri akiwepo Dkt. Jafo pamoja na Profesa Kabudi kwa kutuletea miswada hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwenye Muswada wa Ushidani. Muswada huu wa marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa mwaka 2024, mimi mwenyewe nauona ni Muswada mzuri sana kama utatendewa haki. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge nikiwa ni Mjumbe wa Kamati tuweze kuusikiliza vizuri na kuchambua na tuweze kuupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa kama Mjumbe wa Kamati, tuliweza kuwaita wadau na tukaweza kukaa na Serikali tukapitia vifungu kwa kifungu kwanzia Ibara ya 1 ambayo inasema kuhusu jina mpaka ya mwisho. Tulishauriana mambo mengi na kweli Serikali ilitusikiliza na sisi kwa kushauriana tuliweza kukubaliana mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niweze kuongelea Ibara ya 13. Ibara ya 13 ambayo tulikuwa tunaiongelea inafuta Kifungu cha 17 cha Sheria na kukiandika upya na hasa sana sana inahusu faini zinazowekwa hasa kwa wafanyabiashara na wajasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kilisema kuwa kwa hawa wafanyabiashara kima cha chini kiwe shilingi 300,000 na kima cha juu kiwe shilingi 1,000,000. Ni kweli na wewe mwenyewe ukiangalia ni jambo gumu sana hasa kwa kuchukua wajasiriamali wadogo wadogo na sana sana nikisema wadogo wadogo, hapa naongelea mama lishe, ambapo wengi tunajua ni mama lishi ni wakina mama ambao wanauza vyakula vyao na ambao hawawezi kupata hela nyingi ambazo zinaweza kuletwa kwa shilingi 300,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naongelea bodaboda, mikokoteni na machinga ambao wana biashara ndogo ndogo. Pia, nashukuru sana Serikali, tulikaa ndani ya Kamati kwanza sisi wenyewe tukashauriana kuwa kima cha chini kiwe shilingi 50,000 na kima cha juu kiwe shilingi 1,000,000. Baada ya kukutana na

Serikali tukakaa tena tukajadiliana, tukachakata, tukaona hapana haiwezekani kwa sababu bado hela iko nyingi kwa mama ntilie. Hapo hapo unamweka na mama anayeuza mchicha kama atakiuka unakuta kuwa faini itakuwa juu sana. Ndiyo tukashauriana na Serikali, tukakubaliana pamoja na Serikali kuwa kima cha chini kama umekiuka, kumbuka ni kama umekiuka iwe ni faini ya chini iwe ni shilingi 10,000 na isiyozidi shilingi 1,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo ikashauriwa kuwa, lazima kiwepo kifungu ambacho kitaweza kuwabaini hawa wafanyabiashara na wajasiriamali wako *level* gani ili kusudi kanuni iweze kuwekwa ambayo itawatambua hawa wajasiriamali kufuatana na *level* yao waliyonayo. Kwa hiyo, hiyo imekaa vizuri na tukasema kuwa waweke bei. Bei siyo kazi hata kwa machinga huyo huyo au hata kwenye tochi inaweza ukabandika karatasi; hata kwenye mchicha unaweza ukaweka karatasi na hata kwenye mpunga/mchele tunaona wanaweka vibao kuwa ni shilingi fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu hii mimi mwenyewe naipenda, Kamati tumeipenda na Serikali wameipenda kwa sababu itapunguza na *bargaining* kwa sababu utaiona bei iko hapo. Huwezi kuombaomba kuwa naomba unipunguzie, naomba unipunguzie kwa sababu bei itakuwa imewekwa, utaiona bei iko hapo hapo imewekwa na wewe utanunua kufuatana na bei. Tusonge mbele, mwisho tulisema hivi ni vigumu ndiyo lakini hebu tuanze tuone tutafika wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kusema jambo lingine ambalo ni Ibara ya 20. Ibara ya 20 inarekebisha Kifungu cha 83 cha sheria kwa lengo la kumwezesha mwenyekiti pamoja na wajumbe wake wawili kwa kukaa kwenye baraza kwa miaka minne na wengine watatu kwa kukaa kwenye baraza kwa miaka mitatu. Tuliona kuwa hiyo iambatanishwe kwenye barua zao wakati wa uteuzi kuhusu kutoa mgongano, ni nani akae miaka minne na nani akae miaka mitatu lakini tukaona hii italeta ufanisi kwa sababu kuna wazoefu. Hata humu Bungeni kuna wazoefu ambao wataweza kuwasaidia wale wapya

kuwaelekeza kuwa ni kanuni gani na ni mambo gani ya Baraza yaweze kufuata ushauri jinsi ilivyo na hivyo italeta ufanisi wa utendaji kazi chini kwenye baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na machache, lakini jambo la muhimu ni kutoa elimu kabla ya kuanza kutekeleza hii sheria ili kusudi watu wote (wajasiliamali na walaji) waweze kuelewa ni jambo gani litumike. Pia, kanuni chini ya Mheshimiwa Waziri ziweze kuletwa kwa wakati hasa ndani ya kipindi cha miezi sita ili kusudi sheria iweze kutumika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa sababu mengi tulishauriana na Serikali na tulikubaliana. Ahsante sana kwa kunipatia nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rahhi.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia muswada huu. Pia, kwa namna ya pekee nampongeza sana Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Jafo. Kwa kweli unafanya kazi kubwa sana katika Wizara hii na kwamba kwa kweli tumeanza kuona mapinduzi mbalimbali na mageuzi katika Wizara ya Biashara na Viwanda. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina michango michache. Kwanza, naomba niendelee kuchangia hiyo Ibara ya 13 ambayo inafuta kifungu cha 17 kuhusu habari ya kuonesha bei ya vifaa. Jambo ambalo linataka wafanyabiashara wote na watoa huduma wote kuonesha bei ya bidhaa wanazouza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni bora sana na ni muhimu kwa sababu kwa kweli Watanzania wengi wameibiwa au wamefanyiwa nini na wafanyabiashara. Mwenzangu pia kwamba wafanyabiashara wengi siku hizi wanauza kwa kuangalia hali ya mtu na ninafikiri na sisi huku ni mashahidi kabisa, ukifika dukani kwa kweli wanaangalia hali ya mtu. Kama suti ilikuwa inauzwa kwa shilingi 100,000, mtu akaingia pale kutokana

na hadhi yake akafikiria labda huyu ni mkurugenzi au Mheshimiwa Mbunge kwa kweli suti ya shilingi 100,000 itaunzwa shilingi 400,000 au shilingi 500,000 labda wewe u-*bargain* hapo. Kwa kweli hiyo siyo sahihi kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukipita barabarani wanapouza vitu mbalimbali, ukipita pale na *V8* utauziwa bei yako tofauti na mtu anayepita na bajaji. Kusema ukweli, habari ya kutokuonesha bei siyo jambo jema. Tuwafanyie *fair* Watanzania, wafanyabiashara wazi-*display* bei. Hata kwa akina mama ntilie, ukifika pale kwanza ni faida kwao hawapotezi muda kuendelea kuelezea bei. Hata kwenye huduma ni hivyo hivyo, akienda mtu huyu atapata huduma kwa bei tofauti lakini ukienda wewe hata kama labda ni huduma ya hoteli au jambo lingine, unaweza ukafanyiwa bei tofauti au kutokana na hadhi ya mtu atapewa bei tofauti na mwingine bei tofauti. Kwa hiyo, hili la kuweka bei mimi nali-*support* sana na nafikiri ni *fair* na niwaambie tu wafanyabiashara waliangalie hili la kuweka bei ya bidhaa wanazozitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, mchango wangu ni kuhusu hili la adhabu. Kwa kweli adhabu iliyokuwa imetolewa ni kubwa na mapendelezo ni mengi. Kwamba, adhabu ilingane na biashara ipi? Huwezi kwenda kwa mama sokoni pale amepanga vitunguu vyake, nyanya na viazi, hakuweka bei halafu unaenda kumpiga faini ya shilingi 300,000 sijui shilingi 1,000,000. Tofauti na kampuni kubwa kabisa pengine hawaja-*display* bei, ukaenda kutoa adhabu inayofanana. Kwa hiyo, kama Kamati tumependekeza hili la adhabu ndiyo liangaliwe na adhabu hii inaanza na faini ya shilingi 10,000 mpaka shilingi 50,000 kulingana na biashara inayofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kabla ya kwenda kutoa adhabu hii, kwa kweli tuwe *fair* kwa watu, elimu ya kutosha itolewe kwa Watanzania, waelewe kwanza umuhimu na faida ya kuweka bei. Je, ni nani sasa anaenda kukagua wafanyabiasha? Tusipeleke taharuki, wakaenda sijui watu wa halmashauri au mgambo kwenda kukagua bei huko kwenye biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Tume hii bado ifanye kazi ya kwenda kukagua bei hizi na kwenda kufanya *supervision* na nina wasiwasi tu kwamba tume iko *centered* makao makuu. Kwa hiyo, huko kwenye ngazi ya mikoa na wilaya bado Tume ya Ushindani haijafika. Sasa wafanye utaratibu aidha kwa kushirikiana na *TCCIA* au wao wenyewe sasa waajiri watu hao waongeze nguvu, tume hii wawe na watu kwenye *level* ya mikoa na wilaya ili kuweza kuwatembelea wafanyabiashara, kuendelea kutoa elimu na kuwakagua kama wameweka bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine mchango wangu sasa ni kuhusu Ibara hii ya 18 na 21 kuhusu haki inayotolewa kwa mfanyabiashara ambaye shauri lake limejadiliwa na Tume ya Ushindani lakini hakuridhika, haki inatolewa kwenda Mahakama Kuu. Kwa kweli ni utawala bora kama unampa mtu haki na hajaridhika na Tume ya Ushindani, aende Mahakama Kuu ni utawala bora na haki ya kila mtu inapatikana Mahakamani. Jambo hilo ni zuri lakini sasa anaweza asiweze kutumia haki vizuri kwa sababu kanuni na taratibu za mtu anakataje rufaa bado hazijaweza kuletwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kumwomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, hebu tuletee hizi kanuni, kwamba mtu kama hajaridhika na shauri lake lililoamuliwa na Baraza la Ushindani, ni hatua zipi anatakiwa kuchukua ikiwepo muda, gharama pamoja na taratibu zingine? Kwa hiyo, hizi kanuni natarajia zitaletwa mara baada ya kupitisha hii sheria ili mtu aone kwamba shauri lake limejadiliwa na Tume ya Ushindani na hajaridhika, ni namna gani sasa anaenda kukata rufaa aende Mahakama Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huyu ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho mchana huu. Jioni tutakuwa naye Mheshimiwa Abeid Ighondo, Mheshimiwa Francis Mtinga, Mheshimiwa Dkt. Kaijage na Mheshimiwa Mohamed Issa.

Nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.55 mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 *(The Fair Competition [Amendment] Bill, 2024)***
**na**
**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) ya Mwaka 2024 *(The Written Laws [Miscellaneous Amendments No.2] Bill, 2024)***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Muswada ulio mbele yetu wa *Fair Competition Amendment Act* wa 2024. Tunashukuru Serikali kwa kuleta Muswada huu, kuna maeneo mengi ambayo kama tulivyosema kwenye taarifa yetu ya Kamati yanaonyesha maboresho ya namna gani Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan katika suala zima la kuvutia wawekezaji na kutengeneza mazingira mazuri ya biashara linazidi kujidhihirisha katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, moja ya vifungu ambavyo vimefanyiwa maboresho ni Kifungu cha Muunganiko wa makampuni kwa kuongeza *threshold* kutoka 35 kwenda 40 ambayo inakuwa *inline* na nchi nyingine za Afrika Mashariki na ya Kati na hivyo kuifanya nchi yetu iweze kuwa na yenyewe *competitive*. Ningependa niongelee Kifungu kimoja kwa mahsusi ambacho baadhi ya Wajumbe wachangiaji wamekiongelea na Kifungu hicho ni Kifungu cha Ibara ya 13 ambayo imekwenda imefuta Ibara ya 17 ya *Principal Act* inayohusiana na masuala mazima ya *price display*.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa kuanza kusema uandishi wa Kifungu hiki upya haujakiandika upya kwa maana ya kufuta kila kitu kuna baadhi ya maneno yamekuwa *retained* katika kifungu hiki kipya lakini kuna maneno yameingezwa na moja ya masharti yaliyoongezwa kwenye kifungu hiki ni sharti ambalo linazungumzia kwamba kuanzia sasa wauzaji wa huduma na bidhaa wataonesha bei za biadhaa zao na huduma ambazo wanazitoa.

Mheshimiwa Spika, naelewa nia ya Serikali kujaribu kutengeneza mazingira ya kuondoa au kufanya biashara ya wafanyabiasha wengi waweze kufanya biashara kwa kuonesha bei zao, tunaitwa kwa Kiingereza *move into informality*. Kwenye Kamati yetu jambo hili kama tulivyosema kwenye taarifa ilitusumbua, lilitupa wasiwasi na hasa kwa sababu katika muktadha wa sheria ilivyotungwa inamtamka mtu kama mfanyabiashara, hakuna *definition* ya mfanyabiashara hasa ni nani, mtu yoyote anaefanya biashara ni mfanyabiashara, anaweza kuwa mdogo, mfanyabiashara wa kati na mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo basi, Kamati yetu ilipoliangalia jambo hili haikukubaliana kwamba kila mfanyabiashara katika mazingira ya Tanzania atatakiwa afanye *price display*. Kwenye sheria ya zamani ilikuwa na hiyo *requirement* lakini iliweka mazingira kwamba katika *circumstance* fulani p*rice display* inaweza ikatakiwa lakini siyo katika mazingira yote, kwa hiyo ilitambua kwamba kunaweza kukawa na ugumu

wa kuwa na *price display* kwa bidhaa na ukija kwenye huduma inakuwa *more complicated*.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira kama hayo Muswada ulikuwa unaongelea mtu ambaye atavunja sharti la kufanya *price display* atalipa *fine* ya shilingi 300,000 jambo ambalo hatukukubaliana nalo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu ilitoa mapendekezo kwamba adhabu ya kutofanya *price display,* namba moja, kama kutakuwa na adhabu basi adhabu hiyo kama ni lazima kuwe na *price display* na hoja iliyojengwa ilionyesha kwamba *price display* ni nzuri kwa ajili ya kuwa-*protect* walaji walio wengi.

Mheshimiwa Spika, tatizo likaja kwenye adhabu na kwa kweli sisi kama Kamati tulitaka adhabu iwe katika Sifuri na Shilingi 50,000 kwa maana ya kwamba wale wafanyabiashara ambao haiwezekani katika mazingira ya Kitanzania wao kupewa adhabu kwa kutofanya *price display* kwa sababu *nature* ya biashara zao huwezi kufanya *price display*.

Mheshimiwa Spika, tunajua bodaboda ni wafanyabiasha, mama lishe ni wafanyabiasha, lakini kuna wafanyabiashara wadogo wadogo wanauza mitumba, wanauza nguo, wanauza maji wanatembea katika maeneo ya barabara kwenye stesheni hawana mahali maalum wanapoishi, hakuna mahali ambapo wamekuwa-*registered*, hawatambuliki kwa maana ya kulipa kodi ya aina yoyote au *fee* yoyote.

Mheshimiwa Spika, maoni yetu ilikuwa ni kwamba Muswada huu usiwaguse wafanyabiashara wadogo wadogo, wamachinga, mama lishe na biashara zote zile za watu ambao hawana mazingira, unaweza ukamwona kesho yupo pale anafanya biashara. Mtu ambaye leo yupo Mbagala, kesho yupo Chang'ombe, keshokutwa yupo Mbezi haitakuwa *intention* ya Bunge lako Tukufu kuwafanya hao wawe ni sehemu mojawapo ya kuwa katika Kifungu ambacho kinaongelewa Kifungu cha 13 ambacho kinataka kuwa-*introduced* katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira kama hayo tulichokubaliana na Serikali tuliwataka watunge mwongozo au kanuni ambazo zitahakikisha kwamba jambo hili halitawa-*affect* wafanyabiashara wadogo wadogo kinyume na matarajio ya Kamati kama ambavyo tuliisema kwenye maongezi yetu na kama ambavyo tumeiongea katika taarifa yetu tuliyoitoa siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, ni mategemeo yangu kwamba jambo hili litashughulikiwa hivyo, nafurahi kusema nimepata hapa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri mabadiliko ambayo yanaashiria kwamba wazo hilo limekubalika na kutengeneza hizo Kanuni ambazo tulizisema katika ukurasa wa 10 wa taarifa yetu unaweza ukarejea ukakuta tulichoishauri Serikali. Ninashukuru kwamba Serikali imelisikia na imeleta hapa mapendekezo ambayo ninaamini sasa yatatuondoa kwenye sintofahamu na hali ya kuona kwamba nia ilikuwa ni kumfanya kila mmoja, nia haikuwa kumfanya kila mfanyabiashara aweze kuingia kwenye *category* hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru kwa nafasi na ninaomba kuunga mkono hoja.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage ajiandae.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia kuhusu Miswada yetu hii ambayo ipo mbele yetu. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu ambaye kimsingi ndiyo mtekelezaji wa mambo haya maana yake tunapotunga sheria yeye pamoja na Serikali wanaenda kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, mahsusi kabisa nianze na haya marekebisho ya Kifungu Namba 16A cha Sheria ya *MSD*, hapa lazima tumpongeze Mheshimiwa Rais wetu kwa sababu marekebisho haya yanakwenda kusaidia *MSD* kuongeza wigo wa uwekezaji hasa katika viwanda vinavyozalisha vifaatiba pamoja na dawa. Tunafahamu gharama kubwa ya dawa pamoja na

vifaatiba hapa nchini kwa hiyo haya marekebisho yanakwenda kuiongezea wigo sasa mpana wa *MSD* kufanya uwekezaji ambao kwa kiasi kikubwa marekebisho haya yanaenda kusaidia kupunguza gharama za matibabu, gharama za dawa, bei za dawa zitapungua hapa lazima tumpongeze Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ule Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.2 ambao unahusu Muswada wa Sheria ya Uhamiaji, Sheria ya mambo ya *Diaspora* pamoja na mambo yaliyomo humo ndani, hapa Mheshimiwa Rais wetu kama Mwanadiplomasia namba moja aliona umuhimu mkubwa sana alipoenda kuongea na *diaspora* kule, akaona umuhimu wa kuona namna ya kuweza kunufaika, ama nchi yetu kupata fursa ya wenzetu wale ambao wameenda huko nje wakapata fursa kule waweze kupewa hadhi maalum ili waweze kuongeza tija katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, hapa napo nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali kwa kuja na mapendekezo haya pia mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Utawala, Katiba na Sheria tumekuwa na majadiliano marefu na mapana ya kina kuhusu jambo hili na kimsingi tumekubaliana Serikali na Kamati zimekubaliana lakini ni maeneo machache tu ambayo yanahitaji kuboreshwa kama ilivyoonekana.

Mheshimiwa Spika, kwanza kuna suala hili la ile sera yetu ya ardhi, masuala ya ardhi yawekwe vizuri ili sasa ile *special status* inapokuja ikianza utekelezaji wake iweze kuendana na sheria zetu za ndani za nchi yetu. Pia kwenye ile sera yetu ya mambo ya nje ambayo tunasema inakwenda kwenye diplomasia ya uchumi iweze sasa na yenyewe ku-*fit* mazingira yetu ya ndani ya nchi lakini na mazingira ya nchi za wenzetu kule nje.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais hapa na niseme kwamba hapa Serikali kwa maana ya Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Ardhi na ya Mambo ya nje washirikiane ili haya mapendekezo waliyokuja nayo na maoni ya

Kamati ambayo tumeshauri yafanyiwe kazi kwa haraka ili tuweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, *diaspora* wetu kuna watu ambao ni wataalam wabobezi wa mambo mbalimbali, kuna madaktari, kuna mainjinia, lakini hatuwatumii hapa nchini kwa sababu walishaenda huko, wamepata uraia kule na Sheria zetu zinawabana, kwa hiyo tunapowapa hii hadhi maalum tutapata kipato kikubwa kutokana nao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ighondo nieleweshe vizuri.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Kama nimepitia vizuri taarifa ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kwamba hiyo sehemu imeondolewa siyo? *(Makofi)*

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli imeondolewa lakini tumesema kwamba kuna vitu ambavyo Serikali inatakiwa ivifanyie kazi irudishe, kwa hiyo ndiyo nilikuwa nashauri sasa itakaporudisha yale maoni ambayo Kamati imeyafanyia kazi na imesema yaletwe yasichukue muda mrefu ili itakapoyaleta sasa yale maono ambayo Mheshimiwa Rais alikaa na wale *diaspora* akawaahidi kwamba ata-*include* yale maoni yao yafanyiwe kazi yasichelewe ili ile ahadi ya Mheshimiwa Rais itimie kwa wakati. Ilikuwa ni hilo Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Wazo lako zuri maadam Kamati baada ya kushauriana na Serikali ndicho ambacho kimekubalika basi tuipe Serikali muda, sasa tukiiambia tena isichelewe ikileta Bunge lijalo na likawa pale pale na wewe ni Mjumbe wa Kamati mkairejesha tena itakuwa balaa, kwa hiyo tuipe muda Serikali maana unasema usiwe muda mrefu sasa watajua uwe muda gani.

Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa maelezo yako mazuri na ndiyo hasa *line* ambayo mimi nipo huko.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye eneo la usafirishaji wa binadamu pia hapa naipongeza Serikali kwa marekebisho ambayo wameyaleta, haya pia yatasaidia kulinda hadhi ya watoto wetu ambao huwa wakati mwingine wanakwenda huko nje wanapata matatizo, kwa hiyo sasa kutakuwa na utaratibu wa namna gani tunaweza tukachukua hatua inapotokea haya matatizo yamejitokeza, kwa sababu wakati mwingine inakuwa ni vigumu kuweza kuwahudumia ama kuchukua hatua kwa matatizo yanayojitokeza wakiwa huko kwenye nchi za wenzetu.

Mheshimiwa Spika, kimsingi ninaendelea kupongeza na kushukuru na kuunga mkono maoni yote yaliyowekwa na Kamati, sina mambo mengi ya kusema kwa jioni hii nilikuwa na hayo machache, niombe kuunga mkono na kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mheshimiwa Waziri ujiandae.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Namshukuru Mwenyezi Mungu pia nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia.

Mheshemiwa Spika, katika Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 ya 2024, naomba nijielekeze kwenye Sehemu ya Saba ya Muswada inayopendekeza marekebisho ya Sheria ya Bohari ya Dawa, Sura Namba 70.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara hii ya 33 ya Muswada huu inapendekeza marekebisho ya Kifungu Namba 16A ambacho kilikuwa kimeitaka bohari ya dawa iendelee kufanya uwekezaji wake ikiongozwa na masharti ya Sheria ya Uwekezaji wa wadhamini peke yake.

Mheshimiwa Spika, hii Ibara ya 33 ya Muswada huu sasa inakwenda kurekebisha kifungu hiki na hivyo inaenda kuwapa *MSD* wigo mpana wa kujiendesha kibiashara na kama taasisi ya kimkakati kwa kuzingatia maelekezo ya Msajili wa Hazina na kuzingatia mamlaka mbalimbali zinazohusika. Sheria hii ya Uwekezaji ya Wadhanini pekee ni sheria ya siku nyingi mwaka 1976 tuliirithi kutoka kwa wakaloni, imekuwa ikiifanya *MSD* ijiendeshe katika masharti ambayo imejibana sana ukizingatia na uhitaji wa matakwa ya Watanzania katika eneo la afya kwa uzalishaji wa dawa pamoja na vifaatiba, hivyo imeifanya *MSD* iendelee kujiendesha kizamani kwa kuzingatia Sheria ya Wadhamini peke yake katika uwekezaji wake, kwa hiyo, sheria hii inaenda kuifanya *MSD* sasa inafunguka kibiashara na kujiendesha kama taasisi kamili.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Bohari ya Dawa ilirekebishwa kama mara mbili, mara tatu, ilianza kufanya kazi mwaka 1993, lakini 2021 na 2023 waliibadilisha Sheria ya Bohari ya Dawa. Katika mabadiliko hayo, mbali ya kuifanya Bohari ya Dawa kuwa taasisi ya kujitegemea maana hapo nyuma ilikuwa idara ndogo tu chini ya Wizara ya Afya, lakini sasa hivi kwenda katika marekebisho ya 2023 waliipa uwezo kuwa taasisi inayojitegemea. Mbali ya kuipa uwezo huo sheria iliitaka Bohari ya Dawa kuongeza uzalishaji wa bidhaa za afya ambazo ni madawa na vifaa tiba na katika kufanya juhudi hizo *MSD* sasa imeweza kuanzisha kampuni tanzu. Hiyo kampuni tanzu sasa itakuwa na uwezo wa kuanzisha viwanda na kuingia ubia na viwanda mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pia *MSD* sasa hivi inamiliki viwanda viwili; Kiwanda cha *Gloves* kule Iringa na Kiwanda cha Barakoa pale Dar es Salaam. Si hivyo tu, *MSD* sasa hivi wameweza kuingia mkataba na kuchukua maeneo kwa ajili ya kuanzisha Kampuni ya Dawapamba. Tunazalisha pamba wenyewe hatuna haja ya kuagiza pamba nje ya nchi. Pia, katika Mkoa wa Simiyu wamechukua ardhi pale Kibaha Vijijini kwa ajili ya kuanzisha kampuni ya dawa ambayo itazalisha dawa maalum, dawa mbalimbali ikiwa ni pamoja na *antibiotics.* Naipongeza *MSD. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri, kwa vile sasa hivi ina kampuni tanzu na naipongeza imejiunga na kampuni ya dawa ya Keko imeingia ubia, lakini tumekuwa tukitumia pesa nyingi sana kununua dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI kutoka Uganda. Kwa vile sasa ina kampuni tanzu, tunaomba imshauri vizuri Mheshimiwa Rais ili kile Kiwanda chetu cha Arusha ambacho kina vifaa vya kisasa kikiimarishwa kina uwezo wa kuzalisha dawa hizi muhimu za kufubaza Virusi vya UKIMWI na kuweza kuuza hata nchi jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tuna soko kubwa huku *SADC,* tusione uzito kuingia ubia na kiwanda hiki cha kule Arusha. Kwa hiyo, kwa sababu sasa wamepewa hiyo mamlaka, kifungu tunakwenda kukipitisha, najua Wabunge wenzangu hatutapinga, basi iende kwa mapana zaidi iingie ubia na hiki kiwanda izalishe dawa za kutosha kwa Watanzania na wenzetu wa jirani. Tuache kupoteza dola nyingi kuchukua dawa Uganda ambapo tunaweza kutengeneza dawa zetu sisi wenyewe hapa Tanzania. Kwa hiyo, nashauri baada ya kupitisha kifungu hiki wajiangalie wajitathmini eneo hili, wamshauri vizuri Mheshimiwa Rais hawezi kukataa eneo hili, mama ni msikivu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijielekeze pia kwenye sehemu ya tano ambayo inapendekeza kuboresha Sheria ya Uhamiaji, Sura Na. 54. Katika Ibara ya 18 ya Muswada kwenye Sheria hii ya Uhamiaji inapendekeza marekebisho kwenye kifungu cha Sheria mama Kifungu 20A, inapendekeza kuondoa ulazima wa Afisa Uhamiaji wakati anapochukua maelezo kwa mtuhumiwa kutumia video, kutumia picha na kurekodi sauti, achukue maandishi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Kamati tumeona kwamba suala hili halijakaa sawasawa. Kama kifungu kitakuja hivyo, hakika kitakuwa kinaenda kabisa kinyume na juhudi za dhati za Mheshimiwa Rais ambazo anazisemea za kupambana na kulinda haki za Watanzania. Kitakuwa inakwenda kinyume kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, wote tumeshuhudia mwaka jana Januari Mheshimiwa Rais ameunda Tume ya Haki Jinai imebobea

wabobezi, nia yake thabiti ili kwenda kuendelea kulinda haki za Watanzania. Sasa unapomhoji mtuhumiwa ukasema tuondoe kurekodi sauti, tuondoe kupiga picha, tuondoe kuchukua sauti, tubaki na maandishi, hivi kweli tutakuwa tunamuunga Mheshimiwa Rais katika juhudi zake za kutetea haki za Watanzania?

Mheshimiwa Spika, tunaamini kwamba Kifungu cha Sheria kilichopo kipo kisasa zaidi, hatukubaliani na marekebisho hayo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais baada ya kuunda hii Tume ilizunguka nchi nzima ikachukua maoni ikamrudishia Mheshimiwa Rais Samia ripoti na ikaonesha kwamba kuna baadhi ya sheria za haki jinai zinakandamiza haki za Watanzania. Kwa hiyo, alishauri, alitoa maelekezo Mheshimiwa Rais kwamba vyombo husika vifuatilie hizi sheria vizipitie vione jinsi ya kurekebisha.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa sasa hivi kwa muda mfupi ameonesha ushirikiano mkubwa na Kamati. Tunaamini Mwanasheria Mkuu utaendelea kufuatilia sheria hizi ambazo zimeelekezwa kufuatiliwa na kubadilishwa ili ziendane na haki za Watanzania, ili ziendane na maelekezo yaliyotolewa na Tume ya Haki Jinai na ili ziendane na ushauri wa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika Kifungu hiki tunaona kabisa kwamba hatukubaliani na suala hilo. Tunaona maoni yale ya mwanzo ni ya kisasa yanaendana na uwazi, uwajibikaji na yana ushahidi wa kutosha. Pia, kifungu kile na mawazo yale ya mara ya kwanza yanaendana kabisa na falsafa ya *4R* ya Mheshimiwa Rais, lakini pia yanaendana na mawazo ya Mheshimiwa Rais ya suala zima na jitihada zake kubwa za uimarishaji wa utendaji na mifumo ya utoaji wa haki. Kwa hiyo sisi naomba Wabunge wenzangu watuunge mkono kwenye suala hili la kifungu hiki.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mohamed Said Issa, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ajiandae.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Miswada hii miwili ambayo iko hapa mbele yetu leo. Nitachangia sehemu moja tu ya Muswada wa *Fair Competition Amendments Act* ya 2024. Ibara ya 4 na ya 5 imerekebishwa katika Muswada huu katika Kifungu cha 5, 6 na 8(3) ambapo katika kuunganisha biashara, muunganiko wa makampuni ulikuwa una ukomo wa 35% ndio ambao wa kuhodhi soko. Katika *amendment* hii mimi kama mjumbe wa Kamati tulishauriana na tukaona kwamba sisi tuko nyuma ukilinganisha na mataifa ambayo yametuzunguka. Hivyo, makampuni yale makubwa ambayo yanataka kuhodhi soko ambayo yanataka kufanya biashara na sisi tukaona kwamba haivutiki kuja kuwekeza Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sisi tuliishauri Serikali na tunashukuru Mheshimiwa Waziri na timu yake walivyokuja walitukubalia kwamba 35% ipande mpaka 40% ambayo sasa wawekezaji kutoka nje, kwa sababu tujue kwamba wawekezaji wanapokuja sio wote wanakuja na kitu kipya. Wakati mwingine wanakuja kuungana na makampuni mengine kufanya biashara na wengine wananunua makampuni. Sasa wakiona kwamba ile kampuni ambayo tayari ilikuwa ina soko yaani ina *good will* katika masoko yaani iko zaidi ya 35% wanakuwa hawawezi kuingia pale kwa sababu watakutana na hii sheria. Tukaona kwamba tusogee mbele mpaka 40% ili kuvutia wawekezaji wetu waweze kufanya biashara vizuri.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Ibara ya 13. Hii inaelezea suala la *price indicator and display*. Wajumbe wengi wamechangia hapa na mimi kama mjumbe wa Kamati nilikuwepo kwenye majadiliano na Serikali na jambo hili tulilijadili vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwanza ieleweke wazi Sheria hii ilikuwepo kama ilivyo. Wakati ule ilikuwa inatekelezwa lakini baada ya

kuonekana kwamba haina uhitaji tena, utekelezaji wake ukawa hauna nguvu; wakati ule tunapanga mawe kutafuta sukari, mchele na vitu vingine muhimu. Kwa hiyo, Sheria hii inalenga zaidi kwanza kwa vile vitu muhimu, bidhaa adimu lakini pia kwa wale wenye biashara kubwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii sio kwamba inamlinda mlaji tu, Sheria hii pia inamlinda hata *owner* wa biashara kwa sababu, nitoe mfano mmoja. Mwenye biashara hayupo amemuachia mtu labda anauza nguo, amemwachia uza shilingi 10,000 anauza shilingi 15,000; biashara haiendi na biashara pia zinakufa. Kwa hiyo, jambo hili tukaona kwamba ni vizuri liwepo la *price display*. Wakati tunajadili jambo hili la biashara ndogondogo lilikuja na sisi tuliishauri Serikali kwamba biashara hii ndogondogo kama mamantilie, machinga na watu wengine ambao wana mitaji midogo itakuwaje katika ku-*display* jambo hili? Hili litakuwa sio sahihi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tulikubaliana na Serikali kwamba katika Sheria huwezi ku-*exclude* hii, awemo huyu, huyu asiwemo. Sheria ni msumeno inakata huku na huku. Kwa maana hiyo tukakubaliana iwepo hii lakini kwa haraka sana Waziri atunge kanuni ambayo itakuja kumweka kwamba mfanyabiashara mwenye mtaji kuanzia zero mpaka shilingi milioni tano awe haguswi na Sheria hii, ndivyo tulivyokubaliana. Serikali ilivyokuja hapa ilikubali na wakasema watatunga Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, sasa ni jambo la kushangaza kwamba watu wanafikiria kwamba mpaka machinga ambaye ameshika vitu vyake kule. Hivi Mama Samia ameamua kumtua mwanamke ndoo kichwani leo aje alete *disaster* kwa mamantilie na kwa machinga ambao hao ndio anawalenga kuwaletea maisha mazuri? Jambo hili siamini kwamba hata Mama Samia angeweza kwenda kusaini Muswada huu. Naamini kwamba Serikali yetu hii ina mpango bora wa kumlinda mlaji pamoja na…

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Said Issa, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba.

**TAARIFA**

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nimpe taarifa kaka yangu, pamoja na mchango mzuri anaoendelea nao. Kwanza, taratibu za utungaji wa kanuni hazimruhusu Waziri kuanzisha jambo ambalo halijaanzishwa kwenye sheria mama. Kwa hiyo, anavyosema kwamba wafanyabiashara wataenda kuwa *categorized* kwenye kanuni, kama sheria mama haijawa-*categorize* kwamba hawa hawatakuwemo, Waziri hawezi kuwa na mamlaka ya kuwaondoa wafanyabiashara baadhi akawaacha wengine. Kwa hiyo, kama hilo ndio lilikuwa wazo lao kama Kamati, lilitakiwa liwe *established* kwenye sheria mama ambayo ndio tunaipitisha leo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Said Issa, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata taarifa hii, lakini hii taarifa siipokei, kwa sababu hii taarifa inajibiwa na mchango wa Mwenyekiti wangu pale, Deo kwa kuonesha kwamba tayari Serikali imeshaleta *Schedule of Amendments* ambayo inakuja kuingia sasa kwenye sheria mama. Inawezekana hakuwepo au alikuwa hasikilizi wakati Mheshimiwa Deo anachangia. Kwa hiyo siipokei ili muda wangu usiende kule.

Mheshimiwa Spika, kiukweli jambo hili lina mawazo mazuri na ku-*display*, kwa mfano kuna bidhaa kama sukari, tunategemea kutakuwa na *price indicator* ya bidhaa muhimu. Sasa kama tukimkuta mtu ana biashara pale hakufanya *indicator* na ukisema anafanya ulanguzi utakuwa huwezi kumkamata yule. Hata hivyo tunasema kwamba kuna bidhaa muhimu lazima ziwe na *price indicator and display* na ndio kinafanyika, lakini kwa hawa wafanyabiashara wadogo wadogo kama Machinga, mamantilie na bodaboda, hawa *Schedule of Amendments* itakuja kuwa-*exclude* hapo ambayo ni sheria mama kama alivyosema Mheshimiwa Salome Makamba.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nichangie ni kwenye Ibara ya 17 katika Kifungu cha 59 na 60. Hiki kimeweka adhabu katika makosa ya biashara, masharti ya kukiuka biashara. Jambo hili…

Ni kengele ya ngapi hiyo?

**SPIKA:** Kengele ya kwanza.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, jambo hili sisi tuliliona na Serikali ilikuja na adhabu ya makosa haya kwamba kuna watu wa kawaida ambao ni wale wafanyabiashara wa kawaida ambao hawakuwa *registered* au hata kama ni *registered* kama *sole proprietor,* lakini ni mtu wa kawaida wakaleta mapendekezo yao. Sisi kama Kamati tukaona kwamba mapendekezo ya mtu wa kawaida, adhabu ya shilingi 10,000,000 mpaka shilingi 30,000,000 ni sahihi kabisa na wale wa kampuni shilingi 30,000,000 mpaka shilingi 50,000,000.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tunasema hivyo? Kwa sababu hii kazi ya kuharibu biashara za watu wengine ni biashara ambayo inaua biashara kubwa. Hata tulivyokuwa kwenye Kamati walikuja wauzaji wa bia wanasema mtu amekamatwa, wao wamepeleka kesi, lakini mwisho wamekuja kutozwa *fine* ya shilingi shilingi 5,000,000 wakati yeye faida yake tu ni zaidi ya shilingi shilingi 50,000,000 ya ile biashara. Kwa hiyo, wakaona kwamba ni lazima kwanza adhabu iwe kubwa, lakini pia kuna kipengele mwisho kule kinaendelea; asilimia 1.5 ya gharama ambayo atatozwa mtu. Sasa jambo hili tukaona kwamba ni sawa na ninashukuru Serikali ilikubaliana nalo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kuna kitu hapa ambacho mwathirika huwa hashirikishwi kwenye ile *plea bargaining.* Jambo hili liingizwe kwenye sheria au kanuni kwamba mwathirika ashirikishwe kwenye ile *plea bargaining* kwa sababu inapofanyika mwathirika hajui kwamba nini kimeonekana, haonyeshi kile ambacho yeye amepata athari gani ya jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, pia, katika jambo hili kuna suala ambalo lilitokea hapa mwaka wa nyuma kwamba makampuni haya ya simu, sisi hatuna makampuni ya simu tuliyochukua *agent*. Kwa mfano hatuna *Nokia* hapa lakini walikwenda kukamatwa watu Kariakoo pale, hii *fair competition* ni ya nini ukasema hii ni *copy*, hii ni nini? Sisi hatuna. Kwa hiyo, zikachukuliwa simu za watu na hazikujulikana zimekwenda wapi. Mambo haya *Fair Competition* watende haki wasijiingize katika mitego ya biashara za watu wengine.

Mheshimiwa Spika, wakija tutalinda biashara zao, lakini kwa vile hawapo, kwa nini unaenda kuwasumbua watu pale Kariakoo wanauza biashara zao na wao wenyewe wamenunua huko nje? Waende wakakamatwe huko, lakini sio hapa kwa sababu jambo hili wamenunua wamelipa kodi na wao wanalipa kodi.

Mheshimiwa Spika, mchango wa mwisho, naomba nimalizie kidogo tu hapa, kwenye hili suala la Tume ya Haki Shindani, tunaipongeza Serikali kwa kutusaidia kurekebisha hii kwa sababu mwanzo ilikuwa ndiyo yenyewe tu inatoa adhabu lakini sasa tumebadilisha kwa sababu Katiba ya Tanzania, Ibara ya 107A ndiyo ambayo inampa mtu haki asiporidhika aende akakate rufaa, sasa ilikuwa hakuna haki hiyo. Kwa hiyo, sisi tulipendekeza hiyo na Serikali imekubaliana nalo kwa hiyo tunaishukuru Serikali kwa kuleta Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, sasa katika jambo hili, hii Tume ilisema kuna jambo ambalo lilikuwa ni mwiba sana ambao ilikuwa inapendekeza kusiwe na ukomo wa kushughulikia jambo hili. Kwa mfano, kama kampuni imenunua hisa lakini baada ya miaka 100 ikaonekana ile hisa alinunua kimakosa zichukuliwe zirudishwe kule ambayo ilikuwa sio sahihi. Sasa sisi kama Kamati tulipendekeza na tunashukuru Serikali walilipokea kwamba kuwepo na *interval,* mwanzo ilikuwa ukomo ni miaka mitatu lakini tukasema tuongeze mpaka miaka 10 na hilo limekubalika.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kulipokea hili na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, Waziri wa Viwanda na Biashara uje uhitimishe hoja yako, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ujiandae.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza awali ya yote ningependa kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mola ambaye toka asubuhi ametuwezesha wakati wa kuwasilisha Muswada huu, lakini halikadhalika Wajumbe kuchangia kwa kina.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe kwa kuongoza Bunge letu hili Tukufu vizuri na kwa weledi mkubwa sana na hakika sisi tunajivunia kwamba wewe ni Spika wa viwango ndio maana dunia imekuona kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana wa Kitanzania wanajifunza sana kutoka kwako na sisi tunazidi kukuombea weledi huo na maarifa hayo Mungu aendelee kuyaasisi zaidi katika kichwa chako na maisha yako, lengo kubwa Watanzania waendelee kupata faida.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu yeye kwa uongozi wake mahiri ambao Muswada huu umepita katika ngazi mbalimbali leo hii tunaumaliza katika Bunge lako Tukufu. Maelekezo yake yametoa weledi wa hali ya juu kuhakikisha kwamba Muswada huu kwa lengo kubwa kwamba walaji wa Tanzania waweze kupata nafuu kupitia Muswada huu ambao baadaye itakuwa Sheria yetu ya *Fair Competition Act.*

Mheshimiwa Spika, niishukuru Kamati hii ambayo imefanya kazi kubwa sana. Bahati nzuri Mwenyekiti wa Kamati hii ni mwanasheria, Kaka yangu Deo Mwanyika na wajumbe wake wamefanya kazi kubwa sana, wametoa maelekezo mengi sana na ndiyo maana hata *schedule of amendment* tuliyoi-*move* ilikuwa ikiakisi katika kuhakikisha kwamba tunatekeleza maelekezo ya Kamati. Lilibakia lile moja tu dogo la wale wafanyabiashara wadogo.

Mheshimiwa Spika, kwa maelekezo sisi ni lazima tuwe watiifu wa Bunge hili, Kamati yetu na Wabunge wote. Tume-*move schedule of amendment* kuhakikisha kwamba wafanyabiashara wadogo hawataguswa kwenye eneo hilo. Siyo hivyo tu, baadaye nitatengeneza kanuni ambayo lengo kubwa ni kwamba tukiona *group* la aina yoyote ni lazima tulilinde (lazima tufanye hivyo).

Mheshimiwa Spika, hata humu ndani ya Bunge kuna wafanyabiashara, lakini inawezekana mtu ukafungua biashara yako ukamweka pale mtu akuuzie ile biashara. Kitu ambacho wewe umeona kiuzwe kwa shilingi 10,000, saa nyingine mtu kwa kutokuwa muadilifu akakiuza kwa shilingi 25,000; wateja wakija pale wanakosa kununua biashara yako. Inawezekana wakati mwingine unaweza ukamweka mtu kama muuzaji, lakini akawa na duka lake hapo pembezoni, anashindwa kuuza anasema nenda duka la pili pale utakuta bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, hii maana yake ni kwamba inalinda wateja. Kwanza mtu ananunue kile kitu ambacho anaona hiki sawasawa na asiporidhika atakwenda sehemu nyingine ambayo *price list* inaonesha bei ni *reasonable*, lakini mwisho wa siku ni kwamba hata kuwalinda wale wafanyabiashara. Siyo vizuri kwamba, mtu amewekeza halafu aje kufilisika. Kwa kweli sisi Watanzania tuna kila sababu za kumlinda na hasa upande wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimesema eneo hili halitowagusa wale wamachinga wetu wanaotembea mitaani. Eneo hili halitogusa wale akina mama wanaouza nyanya mitaani (halitogusa). Eneo hili siyo mtu ametengeneza biashara yake ya kawaida; kwa mfano pale Jijini Mbeya, hapana. Eneo hili linakwenda kufanya *categorization* kwa wafanyabiashara wakubwa ambao tumewalenga katika eneo hili. Ndiyo maana tumeweza *ku-move schedule of amendments,* kwamba eneo hili halitogusa wafanyabiashara wadogo. Waziri atatengeneza kanuni ili kuliweka jambo hili vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba litawasaidia sana Watanzania.

Kwa bahati mbaya wengine wakimwona mtu amevaa suti nzuri, akienda sehemu kitu cha shilingi 30,000 anamwambia 150,000, si haki. Hii sasa itaonekana kwamba mtu atanunua kitu alichokiona katika *price display* iliyoko pale na yeye akiridhika ataweza kununua katika eneo hilo. Vilevile, kama nilivyosema ni kwamba, hili halitowagusa wafanyabiashara wadogo na ndiyo maana *tume-move schedule of amendment* kwa mujibu wa maelekezo ya Kamati. Kamati ilielekeza hili na tumeamua kulitekeleza; na kwa bahati nzuri Wabunge wamechangia hapa.

Mheshimiwa Spika, tumeamua *ku-move schedule of amendment* kwa ajili ya kuhakikisha; lengo ni kuhakikisha ya wananchi na siyo kuwakandamiza wananchi. Ndiyo maana nimesema Kamati imetutendea haki. Hata mwanzo Muswada wa Sheria ulikuwa unasema kwamba faini kwa anayeshindwa ni kuanzia 300,000 mpaka 1,000,000. Kamati imeelekeza na ndiyo maana imeshuka hadi shilingi 10,000 kwa mtu wa kawaida. Hili ni kutokana na maelekezo ambayo Kamati imetoa. Ninaomba niwashukuru sana Kamati, wametupatia maelekezo, Serikali tumetekeleza.

Mheshimiwa Spika, wajumbe wamechangia vya kutosha. Dada yangu Pauline Gekul, alipendekeza upande wa semina na hili ni jukumu letu. Baada ya Sheria hii tumemwagiza Mtendaji Mkuu wetu, Dkt. Erio wa *FCC*, tumemwagiza kwamba baada ya sheria jambo kubwa liwe ni kutoa elimu kupitia vyombo mbalimbali vya habari na mitandao ya kijamii ili Watanzania wapate uelewa wa kutosha katika utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kuna wengine walikuwa na mashaka kwamba sheria hii itakwenda kusimamiwa na Mgambo. Hapana, *FCC* yetu itaweka utaratibu wa utekelezaji wa sheria hii, ninaomba Waheshimiwa Wabunge wasiwe na mashaka ya aina yoyote katika upande huo.

Mheshimiwa Spika, Mama Ishengoma naye alitoa mawazo katika kuhakikisha ni jinsi gani suala la utoaji wa elimu tunakwenda kulitekeleza kama nilivyosema. Pia, dada yangu Salome Makamba alichangia hasa *concentration* kubwa ilikuwa ni katika

eneo hilo na hili ninaomba; sisi kwa upande wetu wa Serikali kazi yetu ni kuchukua maoni na kwenda kuyatekeleza. Hili ndilo jambo la msingi ambalo sisi tunaona ni wajibu wetu kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, alipendekeza suala la kutenganisha Sheria ya *FCC* na Sheria ya Kumlinda Mlaji. Mawazo yamechukuliwa, tutaangalia mchakato wa Serikali wa jinsi ya kufanya. Lengo kubwa ni kwamba Watanzania wanufaike na nchi yao na hasa utekelezaji wetu wa sheria katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, dada yangu Nusrat alizungumza kwamba, suala zima la kubainisha utaratibu wa ukataji rufaa. Bahati nzuri Kamati ilisisitiza mchakato huu, wameweka *timeframe* kwamba ni jinsi gani Kanuni *(regulation)* zetu zitengenezwe ndani ya miezi sita. Naomba nilihakikishie Bunge hili kwamba mchakato umeanza, lakini bahati mbaya ni kwamba lazima kwanza sheria ikamilike ndipo twende katika upande wa *regulation*.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba eneo hili la ukataji wa rufaa tutaweza kulisimamia vizuri, na ninaomba niwatoe mashaka kabisa kwamba hakuna matatizo yoyote katika suala hilo.

Mheshimiwa Spika, kaka yangu Mheshimiwa Mwanyika alikandamizia tu palepale, pamoja na dada yangu Mheshimiwa *Alice* alizungumza kwa ujumla, Mheshimiwa Mohammed Issa alikuja kuelezea ni jinsi mchakato ulivyokuwa katika Kamati.

Mheshimiwa Spika, kikubwa zaidi ambacho ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge ni kwamba sheria hii tutakwenda kuhakikisha tunalisimamia vizuri. Kubwa zaidi kwanza tutaanza na ile *package* ya elimu, watu wapate elimu ya kutosha na mwisho wa siku tuweze kuitekeleza sheria yetu vizuri.

Mheshimiwa Spika, sina mashaka kwamba, kwa usimamizi wa Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa weledi wake na sisi tukiungana kwa pamoja, naomba niwatoe mashaka Wabunge wote kwamba, sheria hii itawasaidia hasa walaji na

vilevile wafanyabiashara kuhakikisha kwamba biashara zao wanazifanya katika mazingira rafiki.

Mheshimiwa Spika, hii si sheria ya kuwakomoa Watanzania; sheria hii ni ya kuwasaidia Watanzania na hasa kujua maeneo mbalimbali. Pia, kama tulivyoeleza katika mujibu wa kufanya hizi *amendments* zetu kwa lengo kubwa la kwamba, Watanzania waweze kunufaika katika maeneo yote ambayo wanaona ni lazima walindwe kama walaji wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya machache, nikushukuru sana wewe kwa mara nyingine, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa sababu asubuhi aliendeleza mchakato huu vizuri. Hakika niwashukuru Wabunge wote kwa kuhakikisha kwamba Muswada huu wa Sheria unajadiliwa vizuri. Baada ya hayo machache naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Saidi Johari aje ahitimishe hoja yake.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho ya mjadala kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) ya Mwaka 2024 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.2) Bill, 2024)*.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwa kukushukuru wewe kwa uongozi wako mahiri wa kuongoza Bunge hili. Pia, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa uongozi wake wakati wa vikao vya asubuhi kabla hatujaahirisha mchana. Tumekuwa na mijadala mizuri ambayo imekuwa na lengo la kujenga katika muktadha wa Muswada huu ambao tunaujadili.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa nipende kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, kwa uongozi wake mzuri pamoja na wajumbe wote wa Kamati ambao waliwezesha wakati wa vikao vya Kamati kujadili Muswada huu vizuri katika mazingira haya ya ushirikishaji na kuridhiana. Pia, maeneo yote ambayo tulikuwa tunaona yanahitaji kuboresha tulikuwa tunakubaliana na matokeo yake. Tumekuwa na hoja chache sana tunapokuja kwenye Bunge lako Tukufu tunapohitimisha hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema na kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati, ili tuweze kuandika sheria nzuri ambazo zitaakisi hali halisi iliyoko sokoni, ni vizuri tukashirikishana kwa kina na kuhakikisha kwamba changamoto zote ambazo tunazibaini tunazifanyia kazi kwa moyo mkunjufu kwa lengo la kuboresha.

Mheshimiwa Spika, napenda kukuarifu kwamba katika majadiliano haya tumekuwa na wachangiaji watatu ambao wote walijikita zaidi katika hoja inayohusu *MSD*. Nikianza na Mheshimiwa Salome Makamba, yeye alisema kwamba hakuna ombwe la kisheria, isipokuwa Serikali iipatie *MSD* mtaji ili kuiwezesha kufanya biashara. Aidha, Serikali ililipe deni la shilingi bilioni 135 inazodaiwa. Serikali imepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeanza kulipa madeni ya *MSD* ambapo kwa mwaka 2023/2024, Serikali imeshalipa shilingi bilioni 100. Aidha, jitihada za kumaliza deni zinaendelea kadri ya upatikanaji wa fedha unavyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Salome Makamba pia alikuwa na hoja kuhusu afisa uhamiaji kutokulazimika kuchukua ushahidi kwa kutumia picha jongefu, picha mnato na kurekodi kwa sauti. Naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba kifungu hiki tayari kimeshafanyiwa maboresho kupitia kwenye jedwali la maboresho kwa kuweka sharti la lazima na tumeweka neno "*shall*" kwa afisa uhamiaji kuchukua ushahidi wa

mtuhumiwa na mashahidi kwa kutumia picha jongefu, picha mnato au kwa kurekodi sauti kulingana na mazingira. Maana wakati mwingine wanaweza wakawa wako porini huko, sasa anaweza kutumia vitu vyote hivyo kulingana na mazingira. Akiwa mjini anaweza kutumia kulingana na mazingira yaliyopo. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Salome Makamba, kwamba suala hili tumeliweka vizuri kwenye jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, pia Dkt. Kaijage yeye aliunga mkono zaidi suala la *MSD* kujiendesha kibiashara na ni kwa sababu ni mambo tuliyoyajadili wakati ule katika ngazi ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kufanya kazi kwa karibu na Wabunge pamoja na Kamati zako katika kuhakikisha kwamba Miswada inayopendekezwa inajadiliwa kwa *spirit* ile ile ya maridhiano na kukubaliana katika maeneo ambayo tunaamini kwamba, changamoto hizi tukizitatua kwa pamoja tutakuwa na Muswada ambao ni mzuri na ambao unaakisi hali halisi na siyo kuzua changamoto zaidi.

Mheshimiwa Spika, nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, hakukuwa na wachangiaji wa maandishi zaidi ya hao wachache kwa Muswada huu uliopo mezani. Pia, nichukue nafasi hii kuwashukuru wote kwa michango yenu mizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nichukue nafasi hii kukushukuru tena kwa uongozi wako mzuri. Kwa namna ya kipekee pia niishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa mawazo yao mazuri hasa katika lile suala la *diaspora* na maoni yao waliyoyatoa kuhusiana na suala hili. Sisi kama Serikali tumeyachukua na tutayafanyia kazi na kuhakikisha kwamba tunaporudi mara ya pili tunarudi kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa ili iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaendelea na utaratibu wetu, Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi. Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 *(The Fair Competition (Amendment) Bill, 2024)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 8

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 13

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwenye hiki kifungu kwanza kina makosa ya uchapaji, badala ya *(d)* siyo inatakiwa kusomeka *(b)?* kwa sababu umeleta *further amendment* maana yake umetokea kwenye zile *amendment* ulizokuwa umeleta mwanzo, umeleta nyingine juu ya ile uliyo-*amend*. Sasa tuko sawa? Kuna makosa badala ya (*d)* ni *(b)?* sawa.

Badala ya *(d)* ni *(b),* halafu na juu ilipoandikwa *(c)* napo itasomeka (b), si ndiyo? Haya sawa. Wakati huo huo hapa kwenye Muswada hiki kifungu 17(1) inasema *"A person who sell goods or services"* ilikusudia kusema "*who sells?*" *"s" ina-miss* hapo? Kwa hiyo *"s"* inabidi iongezeke hapo.

Halafu kuna hii *further amendment* uliyoleta ambayo ina hoja pia ya Mheshimiwa Mohamed Said na ile ambayo alikuwa anazungumzia Mwenyekiti wa Kamati hapa umesema kitaongezeka sasa kifungu kwamba *"this section shall not apply to small traders or such other categories of business as the Minister may determine*". Huyu "*Small Trader*" yeye yuko *defined* mahali popote kwenye sheria? Tunamjua yaani *"Small Trader"* ni nani au hatumjui?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi tunataka tum-*define* wakati tunatengeneza *regulations* zetu.

**MWENYEKITI:** Sawa wakati huo ili tuwe wote kwenye picha moja na hapa Katibu anaangalia kama kuna maana yoyote tunayoijua. Kwa sasa hivi "*Small Trader*" ni nani? Huyu ambaye tuko naye yaani kichwani ni nani?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi "*Small Trader*" hawa ni *category* kama hao wa Machinga wanaotembeza nguo, wauza matunda, hao wauza mbogamboga hawa wote ni "*Small Trader*".

**MWENYEKITI:** Tunaangalia kiasi cha mtaji au tunaangalia aina ya biashara anayofanya?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi tunaangalia *both,* sawa, mtaji wake lakini vilevile na aina ya biashara anayoifanya, lakini sasa tukija katika kanuni zetu tutaweza ku-*describe* eneo hili la "*Small Traders*".

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri nia ya Serikali kwa kweli ni njema sana hasa kwenye kuleta kifungu hiki ili wasiwemo wale ambao walikuwa Wabunge wanawazungumzia, lakini sasa kwa sababu huu utengenezaji wa Kanuni kwa namna ambavyo Bunge limekasimu hayo Madaraka kwa Waziri kwenda kutengeneza kanuni sisi wenyewe tumejiwekea utaratibu hatuzitazami zile Kanuni kabla hazijaanza kutumika.

Kwa hiyo, upo uwezekano wa Kanuni kutengenezwa zikaendelea ndio zinakuja kwenye Kamati yetu Ndogo na tulishalisema hilo kwa sababu hatutaki tuzuie utekelezaji upande wa Serikali tukisema tunasubiri mpaka Bunge likae lizitazame hizo Kanuni la sivyo maana yake tutakuwa tunatunga sisi wenyewe wakati kazi tumekupa wewe.

Sasa kwa sababu tumewahi kupata changamoto huko nyuma za Kanuni zinaanza huko nje halafu lawama inakuja Bungeni. Kama hatuna mahali ambapo tumesema "*Small Trader*" ni nani, tukisema sisi neno *small trader* hapa ni Waziri ndio akaseme ni nani huyo "*Small Trader*" ambaye sisi tumetunga Sheria hapa, hii kidogo inaleta changamoto kwa sababu wewe ndio unaenda kuamua nani ndio "*Small Trader*"

Sasa kama wewe ndio unayeenda kuamua na huko nyuma tulishawahi kupata changamoto na "*Small Traders*" ndio kundi kubwa kwa namna sisi tunavyojua, sasa hatujui utaenda kutumia kigezo kipi, wewe umesema *both*. Kule tena umesema vizuri, hapo umeitaja Mbeya. Mbeya wako wengi sana hawa lakini wako wengi katika maeneo ya majiji yote na hata vijijini wapo.

Sasa sisi kwa sababu tuna wasiwasi kidogo na hilo eneo, siyo tuna wasiwasi na wewe hapana, tuna wasiwasi na eneo, kile kifungu kilichopo sasa, ni *mischief* gani ambacho hakiwezi kushughulikia ili wewe hiki kifungu ukakitafakari utuletee huyo "*Small Trader*" ni nani, tukupitishie kifungu ukatengeneze Kanuni yaani kile kifungu kilichopo kwamba madhaifu yake ni makubwa sana ambayo yanaleta madhara kwa jamii na kwa hiyo tunahitaji hiki kifungu tukibadilishe sasa hivi.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika lile eneo la mwanzo kifungu kilikuwepo kweli, lakini ukiangalia hata masuala ya *enforcement* hayakuwa vizuri na ndio maana tumeleta hata upande wa *enforcement*. Sasa kwenye *enforcement* lazima tuweke *categorization* jinsi gani mtu tunaweza tukam-*force* na ndio maana tukaamua, sasa tuweke nini watu wa "*Small Trader*" ili mradi tuweze kuwa-*exempt*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nikuhakikishie kwamba kwa sababu una Kamati makini naomba nikwambie Kamati yako hili jambo imelidadavua vizuri na mimi imenipa *timeframe* ya kutengeneza huu Muswada, hizi *regulation* ndani ya miezi sita. Naomba nikuhakikishie japokuwa utaratibu wa kanuni Waziri ndio anamaliza halafu inaenda inakuwa *gazette,* naomba nikuhakikishie kwamba Kanuni hizi kwa muktadha wa jambo hili kabla hazijawa *gazette,* mimi kama Waziri wa Viwanda na Biashara nitahakikisha kwamba Kamati imejiridhisha katika suala hili kwa sababu hili lina maslahi mapana ya wananchi wote. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Hivi Mwenyekiti wa Kamati yupo hapa? Kile kifungu Mheshimiwa Waziri ninakubaliana naye kwa sababu kile kifungu kilichopo sasa hivi hakina *penalty,* yaani kimeweka tu *obligation* lakini hakijaweka mtu ambaye hajafanya hilo jambo anafanywa nini. Si ndio hoja yako Mheshimiwa Waziri na mimi nilivyokisoma kwa kweli naona kina hiyo changamoto.

Hoja yangu ni kwamba hiki kifungu kwa namna kilivyo kikipita leo halafu tukaenda kusubiri utekelezaji kwamba hiki kifungu hakita-*apply* kwa "*Small Trader*" huyu "*Small Trader*" kwa

sasa hivi hajijui yeye ni nani na huku 17(1) tumesema *"a person who sales goods or services shall indicate or display in a conspicuous manner the price of goods or service"* tumeshasema hivyo huku chini huyu "*Small Trader*" hajijui kesho akiambiwa na *someone* yaani kesho siyo maana ya tarehe 4, kwa maana ya kwamba hii sheria sisi tukishapitisha tunampelekea Mheshimiwa Rais ikaanza kazi huko ama hiki kifungu kitazuiliwa mahali kwamba jamani sheria hii imeingia kwenye sheria za nchi lakini utekelezaji wake unasubiria mpaka tum-*define small trader*.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia wakati namalizia hapo kwamba *other categories of business as the Ministers may determine* maana yake ni kwamba eneo la kifungu hiki ina maana mpaka Kanuni inapotoka ndio itaweza kufanya kazi.

**MWENYEKITI:** Hapa unaenda kutengeneza kuhusu "*Small Trader*" na hao wengine wanaofanana na nani na "*Small Trader*" sasa saa hizi wakati hujatengeneza hiki kifungu kitasubiria? Ndio swali kwa sababu "*Small Trader*" hawajijui, yaani kwa mfano Machinga kesho wakasema tumetungiwa Sheria na Bunge, kesho kwa mfano.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki hakitafanya kazi mpaka Kanuni zitakapotengenezwa ambazo zitakuja ku-*define* eneo hili.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Yuko wapi anayesema Mheshimiwa Mwenyekiti? Mheshimiwa Mohamed said

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili hata sisi tulipokuwa kwenye Kamati tulijadiliana na tukaona kwamba lina utata na siyo tu la suala la ku-*define* hiyo mitaji midogo pia katika utekelezaji wake kuna suala pia la utekelezaji wa hii sheria kwamba kuna baadhi ya bidhaa hata *labelling* yake iko *original* kwa maana ya kwamba bei imekuwa *printed* moja kwa moja wakati wa *production.* Sasa jambo hili tuliishauri Serikali

na tukakubaliana kwamba utekelezaji wa Sheria hii lazima utoe muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nakubaliana na msemaji mwanakamati mwenzangu, lakini nataka niongezee kwamba tunapotunga sheria, aidha kuna jambo la haraka tunataka kulishughulikia au kuna suala ambalo pengine tumeliona kwa muda mrefu tungependa kulishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kamati tulihoji na mimi sikuona na Kamati haikuona kama hili ni jambo la *crisis* kwa hiyo tumepata *proposal* ya Mheshimiwa Waziri hapa ambayo inajaribu ku-*cure the problem* lakini haimalizi kwa maana hiyo unayoisema ambayo nakubaliana kabisa na wewe kwa sababu "*Small Trader*" ni nani? Je, ni yule ambaye hana leseni, hana *TIN,* hana mahali maalum anapofanya biashara au ni yule ambaye hata kama ana hivyo vitu lakini kama ni mdogo bado ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni neno ambalo bado linataka kutathminiwa vizuri kabla haijawa sheria, kwa hiyo tuna-*option* mbili moja, ni kama nilivyosema sioni *crisis* ya kubakia na kifungu kilichokuwepo kabla wakati huo tukatafuta muda wa kujiridhisha vizuri zaidi na kuwa na kifungu ambacho tutakuwa wote tumeridhika ndani ya sheria yetu. Kwa hiyo, siyo *amendment* ambayo lazima ifanyike leo au kesho, naomba hicho kifungu tungekifuta tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri tukifuata ushauri kwamba tubaki na

kifungu kile cha zamani tunataka kujua itakuwa na maana gani? Lakini kama alivyoeleza mtoa hoja ukweli kabisa ni bahati mbaya tu imetokea sasa baada ya kuandika kumbe na wadogo wote wameingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana hii lengo lilikuwa hasa ni kuwapata wale wafanyabiashara wakubwa, unaingia kwenye *super market* ukute *price* imeandikwa, umeingia kwenye maduka yale ya nguo yaani waweze ku-*display* hizo, yaani lengo lilikuwa linawalenga wale wakubwa. Sasa kwa namna ya ku-*draft* kwa bahati mbaya tukajikuta kumbe wameingia na wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirudi kwenye hiki cha zamani na hakina *offense* hutashangaa kuona kesho umeingia baadhi ya maduka makubwa makubwa wameondoa hizo bei, maana wanasikiliza mijadala hii. Kwa hiyo, ninachoshauri kwa kuwa lengo ni kuwapata wale wakubwa, lakini hawa wadogo tukawaondoa na tumejaribu kuja na tiba hii lakini kwa bahati mbaya hatujaweza kuwa na tafsiri ya "*Small Trader*" huwezi ukawa nayo hapa unataka kutafiti vizuri je, utatumia mitaji utatumia nini, Waziri ana kazi hiyo ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa kushauri pamoja na kwamba *regulations* hizi haziji kwenye Bunge labda utumie *power* zako ulizonazo kama Spika, *regulations* hizo zije kwa sababu Wabunge wamejaribu jaribu kidogo kum-*define* huyu "*Small Trader*" wakati wanachangia asubuhi wamewataja taja pengine watamtajirisha mtoa hoja Mheshimiwa Waziri ili aweze kutafsiriwa vizuri na kwa sababu ilizaliwa humu iweze kurudi na tuweze kujua hivi sasa huyu "*Small Trader*" ametafsiriwaje na hizo *categories* zimewekwaje kuliko ku-*drop* na kurudi kwenye ile ya mwanzo tutafungua milango kwa wale wafanyabiashara wakubwa kuanza kujitanua, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Eenh! Hii *Fair Competition* hebu wote tusome kwa haraka kama kuna mahali ambapo kuna ile *blanket creation* ya adhabu. Ile ambayo huwa tunaweka kwamba popote ambapo kifungu hakijasema adhabu, adhabu yake ni hii ipo au

hakipo kwenye hii *Fair Competition*. Hebu tuangalie sote kwa haraka haraka, naam! Nini umesema tena?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kumi ambayo ni *offenses penalties and remedies*.

**MWENYEKITI:** Ngoja nifike hapa kumi enhee! Halafu 57 *a person shall not conspire directly an offense against the act by any person.* Tunatafuta ile ambayo inasema kama kwingine kote haijasema tunayo humu kwenye hii sheria? Hii ya 57 haisemi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna zaidi ya hii.

**MWENYEKITI:** Sasa kama hatuna hiyo itakuwa ni *offenses.*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Ngoja Mheshimiwa au umepapata samahani, karibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hapa sijapapata ila ushauri wangu kwa sababu tuna Kamati ya Sheria Ndogo ambayo mara nyingi sana hizi Kanuni zote inapaswa zipite huko. Kwa muktadha wa Sheria hii naomba ikikupendeza hizi r*egulation* kabla hazijaenda zipite kwenye Kamati ya Sheria ndogo kama utaratibu unavyoruhusu.

**MWENYEKITI:** Samahani kidogo Mheshimiwa Waziri, hii ni *part three* au? Ambayo inasema "*a person commits an offense against this act other than parts*" kwa hiyo, ile haipo "*or is involved in such the commission may impose on that person*" kwa hiyo, labda hii hapa. Mheshimiwa Waziri hebu eleza ulichokuwa unasema samahani.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha wa eneo hili napendekeza katika hizi Kanuni kabla hazijakuwa *gazetted* ikikupendeza na ukiona kama

inafaa zipitie katika Kamati husika, Kamati yetu ya Bunge inayosimamia viwanda na biashara, lakini na Kamati ya Sheria Ndogo ambayo inaangalia utaratibu wa Kanuni hizi zote.

**MWENYEKITI:** Sawa ni wazo zuri isipokuwa litavunja ile Kanuni yetu yaani ama tuseme Kanuni ya Bunge kuipa mamlaka nyingine mamlaka ya kutengeneza sheria. Kwa sababu ukileta kabla maana yake sisi sasa ndio tunaotunga hiyo Kanuni, ukileta kabla maana yake tutakuwa tume-*approve before*, sasa sisi hatutaki huo utaratibu kwa sababu utakuwa unaizuia Serikali kuendelea na shughuli zake.

Sisi tunataka utengeneze Kanuni ziendelee na kazi halafu tuje tuangalie imefuata haijafuata, ikija mapema sawa, haikuja mapema sawa, lakini uwe umeshamaliza utaratibu kwa sababu ukileta kabla maana yake sisi ni sehemu ya kutengeneza ile sheria kwa sababu sisi tume-*delegate* kwako, hatuwezi tena kuchukua madaraka hayo ambayo tume-*delegate* kwa mlango huu wa nyuma, sasa keti tu nataka niliweke vizuri, nilikuwa naangalia hii *section 60*.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *section 60* inasema "*where person commit an offense against this act other than part six, seven or section 58, 59 or 88 or is involve in such an offense the commission may impose on that person a fine of not less than five percent of his annual turnover and not exceeding ten percent of his annual whatever*".

Hapa labda ndio anaweza kuingia yule kule kuliko pale kwenye ile *section* ya mwanzo kabisa kwa sababu hapa ile *section* yetu na ile *part* haipo. Kwa hiyo anaweza kuingizwa hapa kwa hiyo adhabu yake kubwa kabisa anaweza akapewa, kwa nini? Kwa sababu ile *section* ambayo ipo sasa ime-*create obligation.* Kama ime-*create obligation* hatuwezi kusema kwamba wale watu wa maduka sasa hivi kwa sababu wanafuatilia wataacha na wao kufanya, lazima wafanye, kwa nini? Kwa sababu *section 17* ime-*create obligation* kwao ya kufanya hivyo na kama hawakufanya tunaenda huku kwingine sasa kuwakaba, si ndio?

Waheshimiwa Wabunge, nia ni nini, ni kwamba yale mawazo waliyoyasema Wabunge hapa yana-*reflect* wazo yaani yana-*reflect* wananchi wanakionaje kifungu hiki wanaona kila mtu yumo. Sasa wakiona kukishakuwa na hiyo hofu ya kwamba kila mtu yumo sisi tutamwondoa kwa Kanuni ambazo wao sasa hivi hawazijui na tutazisubiri kwa muda kwa sababu hatujaweza kusema nani ni "*Small Trader*" ili wajijue hawamo. Kwa hivyo kifungu hiki cha 17 kilichopo sasa ambacho kinawabana bado wale wakubwa kwa maana ya *obligation* waende kule kwenye adhabu kule mbele kama ulivyotuongoza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, hiki kifungu kipya mlichokileta kwa nia njema kabisa kirejee kwetu kikiwa na maelezo ya huyo "*Small Trader*" ili sisi tuwe tumeridhika kwamba wale wadogo humu hawamo. *(Makofi)*

Niko radhi kurejea maelezo kwa sababu wataalam walikuwa wana *consult* sijui kama umenielewa vizuri au nirejee ndiyo ujue?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwako nimekuelewa vizuri sana na nimekisoma hiki cha 60 na *fine* inazoweka kiko vizuri. Watalaam walikuwa wameniletea hiki lakini sijapata muda wa kukiangalia, wao wamejielekeza zaidi kwenye *Cap One,* lakini sijapata nafasi ya kuangalia, lakini kwa hiyo uliyosema na yenyewe ni nzuri, yaani tunaweza kutokea kwenye *60(1)*.

**MWENYEKITI:** Sawa, lakini hebu tazama labda ya kwao ni njia rahisi zaidi ya kutoka hapa tulipo. Huenda njia wanayopendekeza wao ni nzuri au bora zaidi, kama haijakamata nisonge. *(Kicheko)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Sasa hii shida yangu, adhabu yake ni ndogo sana.

**MWENYEKITI:** Basi sawa, tuachane nayo Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sasa tukubaliane kwamba, Kifungu kile kwenye Muswada kwa sababu, sasa hivi tunashughulika na Muswada hatuko kwenye ile Sheria Mama. Kwenye Muswada, Kifungu cha 13 ambacho kilikuwa kinafuta Kifungu cha 17 na kuleta mabadiliko kadhaa ambayo ndiyo

yameleta huu mjadala kwenye huu Muswada ndiyo tunachokiondoa siyo kule kwenye *main Act*.

Tunakiondoa hapa, ili kikafanyiwe kazi vizuri. Tumjue *small trader* ni nani, halafu kirejee kwetu, si ndiyo? Sawa kwa hiyo, Kifungu cha 13 hapa kilipokuwa, sasa kwa sababu, kuna *amendments* zilikuja juu ya hiki nafikiri sasa zote tunaziondoa. Sisi tunabaki na kwamba, Kifungu cha 13 kwenye Muswada kimefutwa, ili kikafanyiwe kazi, si ndiyo? Kinabaki kile cha zamani. Sawa. Ahsante sana.

Katibu, sasa Kifungu cha 17 pamoja na kwamba, tulikuwa tumependekeza yale mambo mengine ya kuingiza hapa na kutoa nadhani yatafanyiwa kazi pamoja. Kwa hiyo, Kifungu cha 10 na, samahani siyo 17, Kifungu cha 13 kwenye Muswada kinafutwa.

Katibu.

Kifungu cha 13

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Kifungu cha 14

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha15

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 16
Kifungu cha 17

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 18

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 19

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 20

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 21

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 22

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 23
Kifungu cha 24

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Kupangilia upya Kifungu cha 22 mpaka cha 24 kuwa Kifungu cha 23 mpaka cha 25.

**MWENYEKITI:** Sasa baada ya kufuta kile Kifungu cha 13 hapa, hebu angalia vifungu vitakaaje kwa namba. Maana yake ni vyote vinarejea kwenye namba zake.

Hiki Kifungu cha 13 kikiondoka, maana yake ni Kifungu cha 14 kinakuwa cha 13, cha 15 kinakuwa cha 14, vinarudi namba moja moja. Maana yake ni hiki cha 22 Kipya kinakuwa ni cha 21, ama?

Ndiyo, Kinakuwa ni cha 21, halafu hiki cha 22 kilichopo sasa kinakuwa ni cha 22, hivyohivyo. Kwa hiyo, maana yake ni *renumbering* inaanzia huko nyuma kuliko hapa ambapo imependekezwa sasa. *Renumbering* inaanzia Kifungu cha Kumi na?

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kumi na Tatu tulichokifuta.

**MWENYEKITI:** Ee kinaanzia Kifungu cha 13 kuja huku chini, Kinaishia cha 21, ama? Kinaishia cha 20? Huku mbele kumeongezwa Kifungu kipya, Kinakuwa cha 21, *renumbering* inaishia ngapi, 21? Kwa sababu, hiki si ni Kipya, Kinaishia cha 21 kwa sababu, cha 22 Kinabaki kama cha 21, umeelewa Katibu?

*Renumbering* inaanzia Kifungu cha 13 mpaka cha 21 kwa sababu, Kifungu cha 22 kilichopo sasa kinaendelea kuwa cha 22. Kile kilichopendekezwa, Kipya kama cha 22 kinakuwa cha 21. Halafu cha 22 kinaendelea kama kawaida, ndiyo kina Marekebisho ya Serikali na cha 23 kinaendelea, si ndiyo? Ni kimoja ndiyo kinakuwa kimepungua.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunapangilia sasa hivi au?

**MWENYEKITI:** Kuanzia cha 13 mpaka cha 21. Soma sasa. *(Kicheko)*

Katibu

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Kupangilia upya Kifungu cha 22 mpaka cha 24 kuwa kifungu cha 13 mpaka cha 21.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mabadiliko hayo ya namba za vifungu, tunaafiki?

*(Upangaji upya wa Namba za Vifungu ulipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa Taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Mtoa hoja, Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, napenda kutoa Taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 *(The Fair Competition (Amendment) Bill 2024)* Ibara kwa Ibara na kuukubali, pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 *(The Fair Competition (Amendment) Bill 2024),* kama ulivyorekebishwa katika Kamati yako ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara ya Muswada wa Sheria ya

Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa mwaka 2024 *(The Fair Competition (Amendment) Bill 2024)*.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

*Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho wa Sheria ya Ushindani ili kutatua baadhi ya changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wake (A Bill for An Act to Amend the Fair Competition Act with a view of making better provisions for its effective implementation)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 (The Fair Competition (Amendment) Bill, 2024) Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya Muswada Kusomwa Mara ya Tatu maana yake ni Bunge limemaliza kazi yake ya Kutunga Sheria hii. Tutampelekea Mheshimiwa Rais, kama ambavyo Katiba yetu inatutaka. Hivyo, nitumie fursa hii kutangaza rasmi kwamba, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 *(The Fair Competition (Amendment) Bill, 2024)* umepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Nitumie fursa hiikumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote chini ya Wizara hii na tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa yale yote ambayo Bunge limeyapitisha, kama marekebisho. Pia, nimshukuru sana Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati yetu ambao wamefanya kazi kubwa sana ya kupitia Muswada huu na kuhakikisha unaweka maoni yote ya wadau na Waheshimiwa Wabunge.

Wabunge wote mlioshiriki ahsanteni sana kwa mawazo yenu, yamesaidia kuboresha Muswada huu na wakati huo huo kuipa Serikali mawazo ambayo wanaweza kwenda kuendelea kuyafanyia kazi, ili kuboresha utendaji kazi wa tume yetu na pia, utendaji kazi wa jumla wa Wizara hii.

Baada ya kusema hayo, tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Bunge Zima.

**SPIKA:** Kamati ya Bunge Zima.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi. *(Kicheko)*

Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2024)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 6
Kifungu cha 7

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 08
Kifungu cha 09
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 16

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 17

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 18

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 18, kina Marekebisho ya Serikali. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, haya mabadiliko yaliyoletwa hapa mbona kama yapo sawa na kwenye *Principal Act?*

Kwa maana nyingine ilitakiwa tu kufuta kwenye Muswada kubaki na kile Kifungu kwa namna kilivyo kwa sababu, haya mabadiliko yako ni sawa na kile Kifungu ambacho kipo kwenye *Principal Act.* Haya ya kurekodi kwa sababu, mwanzoni ilikuwa muweke neno '*may*' badala ya '*shall*'. Sasa limerejeshwa neno '*shall*' ama kuna kitu cha ziada kimeingia hapa? Maana Kifungu kinasomeka sawa na kule kwenye ile Sheria Mama?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwenye Sheria Mama ilikuwa imeyaweka yote. Ilitumia *'and'* na hapa tunatumia *'or',* kule kwenye Sheria Mama tumesema *'and'*. Kwa hiyo, Afisa Uhamiaji alikuwa akienda kule ilikuwa lazima ayafanye yote; hawezi kuchagua kulingana na mazingira atakayoyakuta kule.

**MWENYEKITI:** Sasa kama ndivyo, maana yake ni mabadiliko pekee ambayo yamewekwa ni kwamba, huu Muswada unabadilisha hilo neno *'and'* kufanya kuwa *'or',* si ndiyo? Sawa, lakini tukifanya marekebisho ya sura hiyo Muswada si ulipaswa kusema hivyo kwamba, ni *'or'* badala ya kuonesha kama ni Kifungu kipya? Ili tujue namna ya kutoa haya, yaani kwamba, Bunge Zima limesema nini kwenye Kifungu hiki? Ni kubadilisha neno *'and'* kuweka *'or',* sawa? Ama tukiache hivyo hivyo, kwa maana ya kwamba, namna kinavyosomeka hapa kwa sababu, kwenye hii *Miscellaneous Amendments* huwa tunaandika kinachobadilika kwenye kile Kifungu. Sasa hapa tumeandika, yaani Kifungu kama vile kinabadilika kumbe ni neno dogo, ndiyo hicho kinachonipa shida. Yaani tukisemeje, ili kwenye Muswada wetu kiwe kimekaa sawa. *(Kicheko)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** *'Shall'* imebaki, ni neno *'or'* tu, Mheshimiwa Salome.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, naomba unisaidie kidogo hapo, ulikuwa umeniacha. Wakati Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu anahitimisha hoja yake, alijibu hoja yangu kwamba, iwe ni lazima kwa Afisa wa Uhamiaji kuweka neno *'shall',* iwe ni lazima kumhoji mtuhumiwa kwa maandishi, picha ya mnato na *video* pale anapomchukua maelezo. Akasema pia amekubaliana na hilo na wame-*move schedule of amendment,* lakini sasa hivi ukisoma kwenye *schedule of amendment* yake inaonekana atatumia hiki au hiki au hiki; kati ya hivyo vitatu atatumia kimojawapo kutokana na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nijue Mwanasheria Mkuu wa Serikali anakubaliana na hoja yangu au amekataa? Kwa sababu, alichokisema kwa maneno hakiendani na kile ambacho amekiandika kwenye *schedule of amendment*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kabla sijatoa maelezo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anapokuwa yuko *site* anaweza kutumia vyote au chochote kati ya hivi kulingana na mazingira. Kama nilivyosema anaweza kuwa, kule walikomkamata/walikomkuta ni porini, sasa kile Kifungu cha zamani kilikuwa kinamfanya lazima atumie vyote, akishindwa hataweza kuchukua ushahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi yeye anaweza kufanya vyote *if possible,* au anaweza kimoja kati ya hivyo. Tumeweka hiyo *'or'* hapo ndiyo unaona *gist* ya ile ya mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tulichokuwa tunajaribu kufanya ni ku-*substitute* ile *section 20(2)* na ku-*substitute* na hiki ambacho kina *'or'* ndani yake.

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa twende pale kwenye Muswada wako Mheshimiwa. Twende kwenye ile *clause 18* ya Muswada wako, uko pale?

*The principal Act is amended in section 20(2) by deleting the word 'and' and substituting for it the word 'or'*, tumemaliza si ndiyo?

Ngoja kwanza Mheshimiwa, uko hapo? Kwa sababu neno pekee kwa sasa hivi lililobadilika kwenye kile kifungu cha *principal legislation* ni neno *'or'*. Kwa hivyo, tukija hapa tunasema hivi; *The Principal Act is amended in section 20(2) by deleting the word 'or' and substituting for it the word 'and'* si ndiyo?

*'And'* si ndiyo mliyoondoa mmeweka *'or'*. *Deleting the word 'And' and substituting for it with the word 'or'*.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa *more precise*, kuna *'and'* mbili. Tungependa kisomeke; *The Principal Act is amended in section 20(2) by deleting the word 'and' appearing between the words still pictures and audio and substituting it for the word 'or'*.

**MWENYEKITI:** Ewaaa! Ahsante sana. Hayo ndiyo maneno yaliyopasa kuwepo hapa. Kwa hivyo, ndiyo hayo umesoma hapa? Hebu naomba hayo, kwa sababu hayo sasa hayamo kwenye *amendment* inabidi yawe yametoka kwa Mwenyekiti maana yakitoka kwingine tena Kanuni hapa zisije zikasema Waziri alileta *amendment* wakati tunatunga sheria. *(Kicheko)*

Haya jamani, kwenye ile *amendment* iliyokuwa *moved* na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *'d'* ambayo inahusu *amendment of section 20* ambayo inazungumzia *clause 18* kwenye Muswada itakuwa inasomeka hivyo; *The Principal Act is amended in section 20(2) by deleting the word 'and' appearing between the words still pictures and audio and substituting for it the word 'or'*.

Waheshimiwa Wabunge, Kifungu cha 18 kwa kadri tulivyokisoma hapa mbele, kinaafikiwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 19

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 20

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 21

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 22

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Kifungu cha 23
Kifungu cha 24

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 25

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 26

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 27

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 28

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Sehemu ya Sita

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefuta Sehemu yote ya Sita.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Serikali imefuta Sehemu yote ya Sita, tunaafiki?

*(Sehemu iliyotajwa hapo juu ilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39
Kifungu cha 40
Kifungu cha 41
Kifungu cha 42

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 43

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kifungu cha 43 kimefutwa na Serikali, tunaafiki?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilifutwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Kifungu cha 44

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tupo wengi humu ndani, lakini sijui.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imerekebisha jina la Sehemu ya Tisa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, marekebisho hayo ya jina la Sehemu ya Tisa.

Kifungu cha 45

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 46
Kifungu cha 47

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kubadili mpangilio wa sehemu kutoka Sehemu ya Saba mpaka Sehemu ya Tisa kuwa Sehemu ya Sita mpaka Sehemu ya Nane.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mabadiliko hayo ya majina ya Sehemu kwa sababu namba zimebadilika, tunaafiki?

*(Mabadiliko ya Sehemu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima)*

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, re*numbering* ya vile vifungu vilivyorekebishwa ambavyo ni 23 mpaka 47 kuwa vifungu 22 mpaka 42.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, marekebisho hayo ya vifungu tunaafiki?

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi. Mtoa Hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2023, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2024)* ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2024]* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusiana na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2024)*.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote mmeafiki kwa hiyo Muswada umepita. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali zipatazo Nane kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza wakati wa Utekelezaji wa baadhi ya Masharti katika Sheria hizo *(A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws in order to Keep the Laws Updated with some Challenges Observed in its Implementation)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2024 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2024) Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa mara ya tatu kuashiria kwamba Bunge tumemaliza kazi yetu ya kutunga sheria hii na kama ilivyo ada tutampelekea Mheshimiwa Rais ili na yeye afanye kwa sehemu yake kama anavyotakiwa na Katiba. Kwa kusema hivyo basi nitangaze rasmi kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2024)* umepitishwa rasmi na Bunge.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na viongozi wote ambao wako chini yako na viongozi wote wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria tunawashukuru sana kwa kushirikiana vizuri mpaka tumefikia mwisho mzuri wa Muswda huu. Tunawatakia kila la kheri kwenye utekelezaji wa yale ambayo mliyaonesha kwa Kamati na sasa kwa Bunge kwamba yana changamoto kwenye utekelezaji mkitaka marekebisho na sasa Bunge limefanya marekebisho hayo, tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wote wa Kamati zote hizi mbili tunawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya. Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote kwa kweli tunawashukuru, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo jambo moja kisha nitaleta tangazo kwenu. Mtakumbuka siku ya Tarehe 27 Agosti, 2024 wakati wa maswali na majibu Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, Mbunge wa Jimbo la Ilemela, alipata fursa ya kuuliza swali la nyongeza katika swali namba tatu ambalo lilikuwa limeulizwa na Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea. Swali lake liliuliza; "Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Sangabuye kilipandishwa hadhi mwaka 1999 kutoka zahanati na kuwa kituo cha afya. Kituo hicho mpaka leo kina wodi moja ambayo inatumika na wanawake, wanaume pamoja na watoto. Je, ni lini Serikali itakamilisha miundombinu pale ikiwa ni pamoja na kujenga uzio?"

Waheshimiwa Wabunge, baada ya swali hilo la nyongeza, mimi kabla sijampa nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye wakati huo alikuwa hapa mbele tayari kwa ajili ya kujibu maswali, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, nilimhoji Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kwa namna gani wanawake, wanaume na watoto wote wanalala sehemu moja ama kwenye wodi moja. Mheshimiwa Mbunge akasema kwamba hiyo ndiyo hali halisi iliyopo.

Nilivyompa nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri akasema hilo jambo katika hali ya kawaida au kwa utaratibu uliopo haliruhusiwi lakini atafuatilia ili aone ni nini kinachoendelea huko. Mimi kwa sababu ni jambo ambalo kwa kweli lilielezwa kwa uzito nikasema kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri akimaliza kujibu maswali aende akafuatilie jambo hili kisha alete taarifa.

Kabla hatujaahirisha Bunge Mheshimiwa Naibu Waziri akawa ameleta ushahidi ambao ulikuwa ni wa maelezo na picha ya hali halisi ya kituo hicho. Sikumpa Mheshimiwa Naibu Waziri nafasi ya kutoa yale maelezo, niliyatoa mimi kwa sababu aliniletea ushahidi wa maandishi. Kwa hiyo, nikampa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba haya ndiyo maelezo ya Serikali kwa maana ipi? Kwa maana ya kwamba kwanza hicho kituo cha afya hakina wodi kabisa lakini Serikali kwa kutambua hilo wale watumishi wamejiongeza, wameweka vyumba vitatu kwa ajili ya kulala watoto chumba kimoja, chumba kingine wanaume na chumba kingine wanawake na wakawa wamepiga picha vile vibao

vinavyoashiria kwamba kuna hizo sehemu tatu za kulaza wagonjwa. Hata hivyo, ile taarifa ilionesha kwamba hakuna wodi isipokuwa vyumba ambavyo vingetumika kwa ajili ya shughuli nyingine hapo hospitali sasa vinatumika kwa ajili hiyo wakati wanasubiri ujenzi wa wodi.

Baada ya kutoa maelezo hayo Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula alisimama kuomba mwongozo kwamba yale maelezo yaliyotolewa kama ushahidi wa kile kinachoendelea pale kwenye kituo cha afya hakuna uhalisia kwa sababu yeye amefanya ziara kwenye hilo eneo hivi karibuni na amekuta kwamba hao wanawake, watoto na wanaume wanalala sehemu moja.

Sasa, kwa sababu nilikuwa nimeshaletewa ushahidi hapa mbele, nikamhoji Mheshimiwa Mbunge ikiwa alikuwa anazungumza kwamba Waziri au Naibu Waziri au Serikali inasema uongo Bungeni. Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula akasema kwamba kile alichokisema ndiyo hali halisi. Sasa, kwa sababu Kanuni yetu ya 70 ukiisoma kwa ujumla wake inataka yule anayetoa tuhuma ndiye athibitishe basi nikamtaka Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula alete ushahidi kwa mujibu wa Kanuni hii.

Sasa, mtakumbuka wakati huo nikimwambia alete ushahidi sikuwa nimesema alete lini Ushahidi, kwa hivyo tulivyorejea tena Bungeni nikamwambia sasa ushahidi aulete siku ya Tarehe 20 Agosti, 2024. Mheshimiwa Dkt. Mabula alitekeleza agizo hilo kwa hiyo alileta ushahidi ambao yeye aliona unathibitisha jambo lake. Sasa, katika huo ushahidi aliouleta tumeupitia, moja ni kutoka kwenye Ofisi ya Mbunge ambayo ni ofisi yake, hilo Jimbo la Ilemela. Ushahidi mwingine aliouleta unatokana na muhtasari wa kikao cha Kamati ya Siasa ya Kata ya Sangabuye ambao unaonesha kwamba wakati wakijadili jambo hili ambalo ni changamoto kwenye kata yao kwa maana ya kwamba kituo cha afya na changamoto zilizopo, maelezo yaliyochukuliwa kwenye huo muhtasari yanaashiria kwamba mjadala ulisema kwamba wodi ya wanaume hakuna, kwa hivyo kwa kuwa hakuna wakati mwingine wanapelekwa kwenye chumba cha wanawake.

Sasa, acha niyasome hayo maneno yanavyosema; "Kituo cha Afya cha Sangabuye hakina wodi ya wanaume, wagonjwa wanapozidi wanahamishiwa kwenye chumba cha wanawake kwani chumba cha wanaume kilichopo ni kimoja tu chenye vitanda viwili." Maana yake ukisoma haya maneno hayapingani na majibu aliyokuwa ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ushahidi kwamba chumba cha wagonjwa wanaume kipo kwa sababu wanasema wakizidi, maana yake wasipozidi wana chumba chao kama maelezo yalivyokuwa yametolewa.

Hapa waliposema wanapelekwa kwenye chumba cha wanawake ni kwa sababu zile siyo wodi, ni vyumba ambavyo vimetengwa kwa ajili ya kuhudumia hawa wagonjwa wanapokuwa na hizo changamoto na kwa kweli hawa wagonjwa huwa hawachanganywi na hata haya maelezo yanayotolewa kwenye huu muhtasari wa kikao cha Kamati ya Siasa ukiusoma wote kwa pamoja unaashiria kwamba siyo kwamba kule kunakuwa na wanawake halafu ndiyo wanapelekwa ila unaashiria kwamba ikiwa chumba kile kiko wazi hakina wanawake ila wanaume ndio wagonjwa wengi, basi wanapelekwa kule, lakini siyo kwamba wanalazwa wote kwa pamoja.

Ushahidi mwingine ulioletwa ni kiambatisho ambacho ni taarifa ya maadhimisho ya kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi miaka 47 ambayo inaonesha wodi katika Kituo cha Afya cha Sangabuye hazipo kabisa jambo ambalo linaungana na maneno aliyoyasema Mheshimiwa Waziri.

Sasa, katika kuchambua ushahidi wote huu unaashiria kwamba alichokisema Mheshimiwa Mbunge ni kwamba kile kituo cha afya kina changamoto za miundombinu. Pengine kilichoongezeka hapo ni kwamba wagonjwa wanalala wote sehemu moja, lakini kwa maana ya kwamba kituo cha afya kina changamoto za wodi huu ushahidi wote unaonesha kwamba kuna changamoto. Hata hivyo, hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba wagonjwa wote wanalala pamoja hiyo sasa ndiyo siyo kweli kwa sababu hoja ilisimama hapo kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri ushahidi aliouleta uliashiria kwamba hawa wagonjwa

hawalazwi pamoja yaani watoto, wanawake na wanaume wakati Mheshimiwa Mbunge alikuwa anasisitiza kwamba wote hawa wanalala pamoja.

Sasa, ushahidi huu unaashiria nini? Kwa sababu Taarifa zetu Rasmi za Bunge ziliweka hiyo kumbukumbu kwa hiyo lazima tufunge hilo jambo kwa sura ifuatayo:

Kwa sababu Kanuni yetu ya 70 inataka aliyesema kwamba mwingine anasema uongo au Mbunge mwingine anasema uongo ndiye athibitishe, sasa vile vithibitisho vilivyoletwa vyote nikivipitia kwa pamoja havina mahali ambapo vinaashiria kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, alisema uongo kwa Bunge. Kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri alisema kuna vyumba vitatu kwa maana ya kwamba kuna chumba ambacho wanalaza wanaume na wameandika wodi ya wanaume lakini siyo wodi na yeye alisema hivyo kwenye taarifa yake na chumba wanacholazwa wanawake kipo na chumba wanacholazwa watoto pia kipo.

Kwa hiyo, kwa sehemu Mheshimiwa Mbunge ukweli wake ni kwamba kuna changamoto kwenye kituo cha afya hakuna wodi, uongo ni kwamba wale wanalala wote pamoja, hiyo ndiyo changamoto. Upande wa Serikali hakuna mahali ambapo walipingana na hoja ya kwamba kituo cha afya kina changamoto na kinahitaji kuboreshwa.

Kwa hivyo, nampa nafasi Mheshimiwa Mbunge kwa sababu Kanuni yetu ya 70 inataka aidha Mbunge athibitishe kwa maana ya kuliridhisha Bunge au kama sivyo basi apewe fursa ili aweze kuomba radhi na kama haikuwa hivyo, basi Kanuni nyingine tena inasema pale nini kinaweza kufuata. Kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula yuko hapa nitampa fursa kwa mujibu wa Kanuni zetu na Kanuni ya 70 inanitaka nimpe fursa ili aweze kusema maneno hayo ambayo atakuwa anayasema kwa muktadha wa haya ambayo nimeyasema hapa.

Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, karibu.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa kuweza kusema maneno machache baada ya kuwa umetoa maelezo kuhusiana na namna ulivyopitia ushahidi wote ulioletwa. Nashukuru ya kwamba pamoja na maelezo uliyosema utambuzi ni kwamba bado pana changamoto na bado pale wamezungumzia habari ya kwamba wanapozidi bado wanaingia kule. Kwa hiyo, kama ilileta mtafaruku kwa namna ambavyo niliwasilisha hali halisi, naomba kufuta hayo maneno, lakini changamoto inabaki ile ile kwamba bado hakuna miundombinu.

Mheshimiwa Spika, naomba radhi kama limeleta mtafaruku katika kuelewa hoja halisi niliyokuwa naitoa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo inafungwa kwa sura hiyo kwa hivyo yale maneno ambayo yalizungumzwa siku ile yakiashiria kwamba Serikali au Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, hajazungumza jambo lenye uhalisia basi yanafutwa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama Mheshimiwa Mbunge alivyozungumza hapo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa nina tangazo moja. Tangazo linatoka kwa Mwenyekiti wa Bunge Bonanza, Mheshimiwa Festo Sanga, anawatangazia Wabunge wote matokeo ya Bunge Bonanza lililofanyika Jumamosi, tarehe 31 Agosti, 2024 likishirikisha Wabunge, watumishi wa Ofisi ya Bunge na Maafisa wa Benki ya *NMB* ambapo Benki ya *NMB* walikuwa wadhamini wa bonanza hilo lililobebwa na kauli mbiu...

Mheshimiwa Tabasam sauti yako inasikika mpaka huku mbele halafu mimi nimesimama.

... lililobebwa na kauli mbiu ‘Shiriki Uchaguzi kwa Maendeleo ya Taifa Letu’

Aidha, bonanza hili pia lilishirikisha wadau kutoka Wizara ya Maji, *TANESCO*, *TANAPA*, Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Bunge na vikundi vya mazoezi *(jogging clubs)* kutoka jijini Dodoma. Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka

Biteko ambaye ni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:

Mpira wa Miguu walicheza *NMB* na Bunge na hapa naona Mheshimiwa Sanga hajasema nani alishinda. Mpira wa Miguu, *NMB* walishinda dhidi ya Bunge. *(Makofi/Kicheko)*

Mpira wa Pete, Bunge waliishinda *NMB*. Mpira wa Kikapu, wanaume, Bunge walishinda dhidi ya *TANAPA*. Mpira wa Kikapu wanawake, watumishi walishinda dhidi ya Bunge. Mpira wa Wavu wanaume, watumishi walishinda dhidi ya Wabunge. Mpira wa Wavu wanawake, watumishi walishinda dhidi ya Wabunge. Kuvuta Kamba wanaume, *TANESCO* walishinda dhidi ya Bunge, hawa walipendelewa kidogo kwa sababu ya mgeni rasmi. Kuvuta Kamba, wanawake, Bunge iliwashinda Wizara ya Maji, hii ilikuwa ni halali kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

Washindi wa medali; medali zilitolewa kwa washindi watatu kwa kila mchezo wa ushindani wa mmoja mmoja na burudani. Waheshimiwa Wabunge waliopata medali za dhahabu ni wafuatao:-

Riadha mita100, wanawake, Mheshimiwa Saada Monsour Hussein. Karata wanawake, kundi *A*, Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage. Karata wanawake, kundi *B*, Mheshimiwa Neema William Mgaya. *Draft* wanaume, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao. *Draft* wanawake, Mheshimiwa Grace Victor Tendega. Kurusha tufe wanaume, Mheshimiwa Juma Hamad Omar. Kurusha vishale wanaume, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare. Kurusha vishale wanawake, Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula. *(Makofi)*

Kunywa soda kwa haraka wanaume, Mheshimiwa Flatei Gregory Massay. Kula chakula kwa haraka wanaume, Mheshimiwa Salum Mohammed Shaafi. Kukimbia na gunia wanaume, Mheshimiwa Juma Hamad Omar. Kukimbiza kuku wanawake, Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba. Kupenya kwenye pipa wanaume, Mheshimiwa Maulid Saleh Ali. *Pool table* wanaume, Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu. Mchezo wa rede,

Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba. Kuruka Kamba wanaume, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga. Kuruka Kamba wanawake, Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu na kushindana kuvaa soksi wanawake, Mheshimiwa Zainab Athman Katimba. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Hongereni wote ambao mlishiriki katika michezo hii, lakini pia wale ambao mlishinda medali tunawapongeza sana na tunawatakia kila la kheri. Tunaamini medali mlizozipata mtaenda kutuletea heshima hata mtakapoenda kushindana na wenzetu wa Afrika Mashariki, tunawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.06 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 4 Septemba, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*